# Nipashe

Jumatano Februari 12, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580152

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Maalim aibua madai watu 50,000 kukosa vitambulisho ukaazi Pemba

UKURASA 3





UKURASA 15

# Magufuli atikisa mawaziri vigogo

**WALE** ambao hawajawahi kuguswa tangu 2015, awatwisha majukumu mazito ya kutekeleza...

*Endelea uk. 2*



Rais Magufuli



William Lukuvi



Ummy Mwalimu



Jenister Mhagama

## ...Aagiza aliyedaiwa kuchana Qur'an kufukuzwa kazi

UKURASA 2

## YALIYOMO


**UKURASA WA 2**

**MAAGIZO YA MPINA YAMPONZA DED**

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo, amemwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo...

**UKURASA WA 5**

**KINA PAPA MSOFE WAUNGANISHWA KESI YA UHUJUMU**

WAFANYABIASHARA Marijani Msofe, maarufu Papa Msofe (53), na Fadhil Ibrahim (61), wameunganishwa na Wakili wa Kujitegemea, Abdul...

**UKURASA WA 25**

**MKAPA ASOMA HOTUBA YA JPM MAZIKO YA MOI**

MARAIS wastaafu wa Tanzania, Benjamin Mkapa na Jakaya Kikwete, jana walimwakilisha Rais John Magufuli kwenye...


## TCRA SASA YATANGAZA KUZIMA LAINI ZILIZOFUNGIWA

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



MICHEZO NDAYIRAGIJE ATETEA RATIBA LIGI KUU UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# Magufuli atikisa mawaziri vigogo

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS John Magufuli ametoa maagizo manane kwa mawaziri watano, wakiwamo watatu ambao walikuwa hawajawahi kutikiswa tangu atangaze Baraza lake la Mawaziri Desemba 10, 2015, mengi akitaka yatekelezwe ndani ya siku saba kuanzia jana.

Kwa kipindi chote cha takriban miaka minne uongozi wake, Rais Magufuli amefanya mabadiliko kadhaa katika baraza lake hilo, mawaziri sita pekee ndiyo hawakukumbwa na baa la kuteuliwa kwa uteuzi wao.

Mawaziri hao vigogo ni Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Hussein Mwinyi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Vijana, Kazi, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu.

Wengine ambao hawajawahi kuonja uchungu wa kutumbuliwa katika uongozi wa Rais Magufuli ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango.

Jana, Rais Magufuli wakati wa halfa ya uzinduzi wa Wilaya ya Kigamboni na majengo ya kutolea huduma katika wilaya hiyo mpya ya mkoani wa Dar es Salaam, alitoa maagizo manane ambayo yaliwagusa mawaziri watano, wakiwamo watatu ambao hawajawahi kutikiswa katika miaka minne ya uongozi wake. Watatu hao ni Ummy, Lukuvi na Mhagama.

Hafla hiyo mbali na uzinduzi wa wilaya, Rais alizindua jengo la utawala lililojengwa kwa Sh. bilioni 1.6 na jengo la halmashauri lililojengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 5.2.

WIZARA YA AFYA

Rais Magufuli aliiagiza Wizara ya Afya kuhakikisha inapeleka haraka vifaa tiba na dawa katika Hospitali mpya ya Wilaya ya Kigamboni.

Alisema kukamilika kwa ujenzi wa hospitali hiyo inayojengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 1.5 kunapaswa kwenda sambamba na upatikanaji wa dawa, madaktari na vifaa tiba.

"Nataka siku nikivamia katika hospitali hiyo nikute sindano, dawa zote, madaktari, nataka wananchi wakifika hapo wapate huduma zote," aliagiza.

Rais Magufuli aliongeza: "Wakati nafika hapa, nilipata harufu ambayo siyo nzuri,

INAENDELEA UK 8



Jaji Mkuu wa Zanzibar, Omar Othman Makungu, akisalimiana na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, baada ya kuwasili kuhitimisha kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Sheria jana.. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Rais JPM atumbua mtumishi anayedaiwa kuchana Qur'an

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS John Magufuli ametangaza kumfukuza kazi mtumishi wa Halmashauri ya Kilosa, mkoani Morogoro, Daniel Maleki, ambaye anatuhumiwa kuchana kitabu kitakatifu cha Qur'an.

Rais Magufuli alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati akiwa kwenye halfa ya uzinduzi wa Wilaya ya Kigamboni, jengo la utawala na jengo la halmashauri hiyo.

Wakati Rais Magufuli akichukua hatua hiyo, Jeshi la Polisi mkoani humo linamshikilia Maleki na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-Tamisemi), Selemani Jafo, ameshamsimamisha kazi.

"Shughulikieni watendaji ambao wanawacheleweshа... juzi nilikuwa namsikia Jafo kule Kilosa, mtu mmoja alichana kitabu kitakatifu ninashukuru umechukua hatua ya kumsimamisha kazi, lakini mimi ninamfukuza kabisa," alisema Rais Magufuli na kuongeza:

"Mwandike barua ya kumwondoa moja kwa moja, ashinde kesi asishinde huyo sio mfanyakazi wa serikali, hatuwezi tukakaa na wafanyakazi 'wapumbavu' katika serikali hii."

Jafo alimsimamisha kazi mtumishi huyo baada ya kusambaa kwa picha katika mitandao mbalimbali ya kijamii zikimwonyesha Daniel kutoka katika Halmashauri ya Kilosa Kitengo cha Biashara Idara ya Fedha akichana na kutupa kitabu cha Qur'an.

Mbali na kumsimamisha kazi, Jafo aliagiza mamlaka ya nidhamu kufanyia uchunguzi suala hilo na baada ya kujiridhisha hatua kali zichukuliwe dhidi ya mtumishi huyo.

Wakati huo huo, Rais Magufuli alimwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri Manispaa ya Kigamboni kumchukulia hatua Ofisa Ardhi wa wilaya hiyo ambaye ni mtoro.

Rais Magufuli alisema ofisa huyo hajaripoti kazini kwa muda wa miezi mitatu, lakini hajachukuliwa hatua zozote.

"Ninafahamu mlikuwa na matatizo na ofisa ardhi wa Kigamboni ni mtoro, hajafanya kazi karibu miezi mitatu na alishaandikiwa barua kusudi ashughulikiwe, lakini Wizara ya Ardhi bado wanaleta mshahara wake... ninajua hii meseji itafika kwao na huyo kama ni mtoro akatoroke moja kwa moja," alisema Rais Magufuli.

Aidha, Rais Magufuli aliuagiza uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni kushughulikia watumishi ambao ni watoro.

# Maagizo ya Mpina yamponza DED

**Na Mwandishi Wetu, KALAMBO**

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo, amemwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo na kamati aliyoundwa kutathmini miundombinu ya Soko la Samaki Kasanga, kufika mbele ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa kueleza sababu za kushindwa kutekeleza maagizo saba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, juu ya uboreshaji wa soko hilo.

Oktoba 30 mwaka jana, Waziri Mpina alitoa maagizo hayo alipozuru kikazi mkoani Rukwa na kujionea miundombinu chakavu iliyoko katika soko hilo na kusikiliza kilio cha wavuvi na wananchi wanaoishi karibu na soko hilo.

Soko hilo lilizinduliwa mwaka 2013 na aliyekuwa Makamu wa Rais wakati huo, Dk. Mohamed Gharib Bilal, na halijawahi kutumika tangu kuzinduliwa kwake.

Wangabo alisema juzi kuwa miongoni mwa maagizo yaliyotolewa kwao na Waziri Mpina ni soko kuanza kutumika kuanzia Desemba 31 mwaka jana, lakini amebaini halmashauri haijatekeleza.

Alisema soko hilo ni chanzo cha mapato cha halmashauri kwa kuwa kukamilika kwake kutaipatia ushuru na kuongeza mapato katika halmashauri hiyo ambayo ipo hoi katika makusanyo na hivyo kuwataka watumie pesa kupata pesa.

"Wala msitegemee wizara ndiyo itafanya kila kitu hapa ili soko liweze kufanya kazi, lazima ninyi mtumie pesa ili mpate pesa, sasa kama hamtumii pesa kuuvuta umeme kutoka pale, ilikuwa ni kikwazo kikubwa mkasema hakuna transfoma, tukamwambia Meneja wa Tanesco 'leta transfoma', akaleta ile pale mwaka jana.

"Kutoa pale ule umeme kuja hapa imekuwa shughuli, mnataka mwaka mwingine uishe, viongozi waendelee kutoka Dodoma, Dar es Salaam wanakuja hapa kwa ajili ya mambo madogo madogo? Haiwezekani, amkeni!" alisisitiza.

Akisoma taarifa ya mkoa juu ya utekelezaji wa maagizo hayo ya waziri, Kaimu Katibu Tawala Msaidizi (Uchumi na Uzalishaji), Respich Mayengo, alisema Waziri Mpina aliagiza kufanyika kwa maandalizi kuhakikisha soko linafanya kazi kuanzia Januari Mosi mwaka huu na hivyo masuala yote yakamilike ndani ya miezi miwili kuanzia siku hiyo.

"Soko halijaanza kufanya kazi kwa kuwa mfumo wa umeme ndani ya soko haujakamilika licha ya kuwekewa transfoma, elimu na hamasa kwa wavuvi wa Kata ya Kasanga haijatolewa," alisema.

**HABARI KITAIFA**

# Maalim Seif adai 50,000 Pemba hawana vitambulisho vya ukaazi

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais mstaafu wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, amedai zaidi ya wananchi 50,000 Kisiwani Pemba hawajapata Kitambulisho cha Mzazibari Mkaazi.

Mwananchi wa visiwani humo, bila kuwa na kitambulisho hicho, hawezi kuandikishwa katika daftari la kupiga kura.

Aliyasema hayo jana baada ya kukabidhiwa kitambulisho chake kipya cha Mzazibari Mkaazi na taasisi inayohusika na vitambulisho hivyo, akiwa nyumbani kwake, Chukwani, Zanzibar.

Maalim Seif alisema kuwakosesha wananchi kupata kitambulisho hicho, maana yake ni kuwakosesha haki yao ya kupiga kura katika uchaguzi mkuu.

Alisema utaratibu huo ni sawa na hujuma za makusudi na umelenga zaidi Kisiwani Pemba kwa sababu kuna wafuasi wengi wa upinzani.

Kwa mujibu wa Maalim Seif, taasisi ya vitambulisho ina wajibu wa kutekeleza sheria na katiba ya nchi, hivyo haipaswi kuongozwa na matakwa ya wanasiasa.

"Waachie CCM wavuruge sheria na katiba, lakini wao ni taasisi ya umma hawapaswi kuongozwa na matakwa ya wanasiasa. Lakini inavyoonekana wanaongozwa na matakwa ya wanasiasa," alisema Maalim Seif ambaye ni Mashauri wa Chama cha ACT - Wazalendo.

Maalim Seif alihoji kwa nini kitambulisho hicho kipya cha Mzanzibari Mkaazi kitumike kwa uchaguzi tu na kusema kuwa hiyo ni hujuma dhidi ya demokrasia katika nchi katika kutoa haki.

Alisema kuwakosesha baadhi ya wananchi kupata vitambulisho hivyo ni mkakati wa makusudi na umeanza kufanyika Pemba ambako wanaamini kwa kuna wafuasi wengi wa upinzani.

"Tumeshuhudia hapa Unguja katika maeneo ambayo wanasadiki kuna wafuasi wengi wa CCM hakuna matatizo katika kupata vitambulisho, lakini katika maeneo ambayo yanasadikiwa kuwa yanaungwa mkono na wapinzani huwa kuna figisufigisu," alisema.

Kutokana na madai hayo, Maalim Seif alimtaka Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, kusimamia suala hilo ili haki itendeke kila mmoja kupata kitambulisho.

Akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Sheria Kisiwani Pemba, Jaji wa Mahkama Kuu Zanzibar, Khamis Ramadhan Abdallah, aliwatoa hofu wananchi ambao hawakubahatika kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura kwa sababu mbalimbali ikiwamo kukosa vitambulisho vya Mzanzibar Mkaazi kutokuwa na wasiwasi wowote.

Jaji Mkuu alisema Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC ) iko mbioni kutafuta namna ya kuwasajili kwenye daftari hilo ili kupata haki yao ya kupiga kura katika uchaguzi mkuu.

Alisema ZEC haina uwezo wa kutoa mpiga kura yeyote kwenye daftari hilo ambaye ana sifa kama watu wengine wanavyodhani.



Wafanyakazi wa Shirika la Reli la Tazara (TRC), wakiweka magunia yenye udongo kuzuia mmomonyoko kwenye tuta la daraja la treni katika eneo la Mtoni Mtongani, Manispaa ya Temeke, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Laini za simu milioni sita zafungwa

**NA Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imesema imezifungia laini za simu milioni sita kutokana na kutosajiliwa kwa alama za vidole.

Hata hivyo, baada ya kuzifungia laini hizo, laini milioni mbili kati ya hizo zimefunguliwa baada ya kusajiliwa kwa alama za vidole.

Kadhalika, mamlaka hiyo imesema hadi sasa jumla ya laini za simu milioni 33 sawa na zaidi ya asilimia 74, zimeshasajiliwa kwa alama za vidole.

Hayo yalielezwa jana na Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, James Kilaba, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika maadhimisho ya Siku ya Usalama Mtandaoni, yaliyowakutanisha wanafunzi wa shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu.

Alisema wanaendelea na kazi ya kuzuia mawasiliano kwa laini za simu zote ambazo hazijasajiliwa kwa alama za vidole na baadaye watazifungia kama hawatazisajili.

Kilaba alisema wamejipa muda wa kuwasubiri waliokuwa wamiliki wa laini hizo, kuzisajili kwa alama za vidole na endapo watashindwa kufanya hivyo zitafungiwa kabisa.

Uzimaji wa laini za simu ambazo hazijasajiliwa kwa alama za vidole, ulianza Januari 20, mwaka huu na kazi hiyo inaendelea.

Kuhusu maadhimisho ya siku ya usalama mtandaoni, alisema ni mpango wa kitaifa ulioanzishwa mwaka 2004 kwa lengo la kukuza matumizi bora na salama ya mtandao wa intaneti.

Alisema lengo ni kuhamasisha jamii kutekeleza majukumu yake ili kuhakikisha uwapo wa usalama wa anga la mtandao dhidi ya matukio hatarishi ya kiusalama.

"TCRA imeingiza siku hii kuwa moja ya mikakati ya kukuza ufahamu kuhusu usalama mtandaoni. Mkakati huu unalenga kuwezesha watumiaji wa mtandao wa intaneti nchini kufahamu majanga yaliyopo na njia mbalimbali za kujilinda ili kujiepusha na vitendo vya uhalifu mitandaoni pamoja na matumizi yasiyofaa ya mtandao wa intaneti," alisema Kilaba.

Alisema kaulimbiu ya mwaka huu inasema 'Pamoja kwa Mtandao Bora', hivyo, Watanzania wote wana jukumu la kushirikiana kuhakikisha anga la mtandao linakuwa mahali salama kwa watu wa rika zote.

## Watafuta dawa ya ufaulu hafifu

**Na Woinde Shizza, KARATU**

BARAZA la Wafanyakazi wa Wilaya ya Karatu mkoani Arusha limeanza 'kujiuliza' na kutafuta dawa ya mwenendo wa matokeo mabaya ya ufaulu wa kidato cha nne wilayani humo, baada ya watahiniwa 986 kupata daraja sifuri mwaka jana.

Kutokana na mwenendo huo mbaya, baadhi ya wadau wa elimu wanahusisha matokeo hayo na walimu kuwa na uhusiano wa kimapenzi na wanafunzi.

Juzi, Mwenyekiti wa Baraza hilo, Waziri Mourice, alisema hawaridhishwi na baadhi ya walimu ambao utendaji wao wa kazi ni mbovu pamoja na wale ambao wanakuwa na mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi.

Morice aliyasema hayo, wakati wa kikao kazi cha kupitisha bajeti ya matumizi ya fedha ya mwaka ujao wa fedha wa 2020/21.

Alisema Wilaya ya Karatu ina wanafunzi wa kidato cha nne waliopata ufaulu wa daraja sifuri 986, huku wakilaumu kwamba hakuna sababu ya mwanafunzi kukaa miaka minne na kuishia kupata sifuri kwa sababu anayepata sifuri ina maana hana uwezo wa kupata alama D angalau mbili.

Alisema kama Karatu Sekondari wanafanya vizuri kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita, walimu wengine wanashindwaje kutumia mbinu hizo kwa wanafunzi wa kidato cha nne.

Karatu Sekondari wameongoza katika ufaulu wa kitaifa kwa somo la kilimo na mwalimu huyo, mwenyekiti amesema anapaswa kutambuliwa kama mwalimu hodari Mei Mosi.

Aidha, Mourice alisema amefanya ziara Kata ya Mbulumbulu na kutembelea shule mbalimbali na amebaini hata 'orientation course' kwa wanafunzi waliochaguliwa kuingia kidato cha kwanza hawakupata na kwamba walimu wameanza kufundisha moja kwa moja

Alibainisha kuwa maofisa elimu kata nao wameshindwa kusimamia ubora wa elimu katika maeneo yao huku akifafanua kuwa 'orientation course' ni muhimu ili kurahisishia wanafunzi wapate uwezo wa kuelewa na kupenda masomo.

"Si hivyo tu, kuna walimu wamekuwa wakijihusisha na mapenzi na wanafunzi wao, tuhuma hizo zimekithiri, lakini niwaambie tu kwamba hatafumbia macho suala hilo, isipokuwa tutakabiliana na walimu wa aina hiyo," alisisitiza.

Naye Katibu wa Chama cha Walimu (CWT) Mkoa wa Arusha, Felix Mnyanyi, akizungumzia madai hayo, alisema ualimu ni kazi ya kitume na hakuna mwalimu anayeweza kutembea na wanafunzi asifahamike kwa sababu kuna fununu na kwamba mahusiano ya mapenzi kati ya mwalimu na mwanafunzi huchangia kudidimiza ufaulu wa wanafunzi.

# Korti yakubali mazungumzo ya mwisho kesi Kabendera

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imekubali ombi la Jamhuri la kufanya mazungumzo ya mwisho katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili Mwandishi wa Habari za Uchunguzi, Erick Kabendera, kuhusu kukiri makosa na kuomba msamaha.

Kesi hiyo ilipangwa kutajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Janeth Mtega jijini Dar es Salaam.

Jopo la Upande wa Jamhuri likiongozwa na Mawakili wa Serikali Wakuu, Martenus Marandu, Faraja Nchimbi, Mawakili wa Serikali Waandamizi, Lenatus Mkude na Wankyo Simon, lilidai kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa.

Hata hivyo, Nchimbi alidai kuwa mazungumzo kati ya Jamhuri na upande wa utetezi yamefikia hatua ya mwisho na kwamba wanaomba kibali cha kuonana na mshtakiwa kumalizia sehemu iliyobaki.

Wakili wa Utetezi, Jebra Kambole, alidai kuwa upande wao hauna pingamizi dhidi ya ombi la Upande wa Jamhuri.

Hakimu alisema ombi la Jamhuri limekubaliwa na kesi hiyo itatajwa Februari 17 mwaka huu, mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa siku na mahali pasipofahamika, mshtakiwa alijihusisha na genge la uhalifu.

Inadaiwa kuwa katika tarehe tofauti tofauti kati ya Januari 2015 na Julai 2019, mshtakiwa alitenda kosa la kutoa msaada kwa genge la uhalifu kwa nia ya kujipatia maslahi.

Katika shtaka la pili, Kabendera anadaiwa kukwepa kulipa kodi ya zaidi ya Sh. 173,247,047.02.

Katika shtaka la tatu, Kabendera anadaiwa kati ya Januari 2015 na Julai 2019, katika maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam, alitakatisha Sh. 173,247,047.02.




Mkurugenzi Mtendaji Jukwaa la Wadau wa Kilimo nchini (ANSAF), Audax Rukonge (kushoto), akizungumza na wanahabari, jijini Dodoma jana, kuhusu mkutano wa sita wa wadau wa kilimo, unaotarajiwa kuanza leo, na ukushirikisha zaidi ya washiriki 270. Kulia ni Mchambuzi wa Sera wa Shirika la Aspires, Prof. Isaack Minde. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Vigogo Tanica kortini kesi uhujumu uchumi

**Na Restuta Damian, BUKOBA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Kagera, imewafikisha mahakamani watu wanne, akiwamo meneja wa kiwanda cha kusindika na kukoboa kahawa cha Tanica Manispaa ya Bukoba, Linus Leopord.

Wamo pia mhasibu wa kiwanda hicho, Didas Josiah, na wafanyabiashara wawili Athuman Kazinja na Abdul Kazinja, kwa mashtaka 15, yakiwamo uhujumu uchumi na kusababishia hasara kiwanda hicho zaidi ya Sh. bilioni 3.8.

Washtakiwa hao walifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Mkoa wa Kagera mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Neema Gasabila na kusomewa kesi ya uhujumu uchumi namba 1 ya mwaka 2020.

Upande wa Jamhuri uliwakilishwa na mawakili watatu wakiongozwa na Haruna Shomari. Wengine ni Juma Mahona na Naira Chamba, huku wa upande utetezi ni Mathias Byabato na Projestus Mulokozi.

Shomari anaeleza mahakama kuwa washtakiwa namba moja na mbili ambao ni watumishi wa kiwanda cha Tanica, kati ya Januari 2018 na Desemba 2019 kwa nyakati tofauti waliunga genge la uhalifu.

Alidai kuwa washtakiwa hao pia walitumia vibaya mamlaka ya ofisi kwa kupokea kahawa gafi tani 981.4 zisizo na ubora kwa bei ya juu, hivyo kukisababishia kiwanda hasara ya Sh. 3,888,000,000.

Alidai zaidi kwa nyakati tofauti kati ya Januari 2018 hadi Desemba 2019 kwa nyakati tofauti, walijipatia mali kinyume cha sheria ya uhujumu uchumi yakiwamo magari pamoja na matumizi mabaya ya ofisi.

Kadhalika, alidai kuwa Athuman Kazinja, alifanya biashara bila leseni, kukwepa kulipa kodi, hivyo kuisababishia serikali hasara ya Sh. 3,888,000,000.

Kwa mujibu wa Shomari, mfanyabiashara huyo pia alipeleka kahawa gafi kiwandani tani 981.4 isiyokuwa na ubora, na kuiuza kwa bei ya juu Sh. 3,888,000,000, na pia alijihusisha na utakatishaji fedha.

Kwa upande wa utetezi, Wakili Byabato, aliomba mahakama kama kesi haina ushahidi iondolewe mahakamai na kama ina ushahidi iharakishwe kusikilizwa ili wateja wake wapate haki zao mapema.

Naye Wakili Mulokozi alihoji sababu za Abdul Kazinja kuunganishwa katika kesi hiyo kosa la 15 la utakatishaji fedha, ambalo Jamhuri imeshindwa kufafanua anahusikaje.

Shomari alidai mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza hoja hizo, hivyo asubiri Mahakama Kuu.

Hata hivyo hajo hiyo ilipingwa na Mulokozi na kudai hati ya mashtaka inatakiwa kukidhi matakwa ya kisheria.

"Hatuwezi kuibuka ghafla kulalamika mahakama ya juu wakati kesi imeanzia chini na washtakiwa hao wanapelekwa magereza," alidai.

Hakimu Gasabila, alisema amerekodi maelezo hayo, lakini hana maelezo yoyote ya kusema kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo, hivyo itatajwa tena Februari 25, mwaka huu.

# Uvamizi machimbo madini waibua ulaji

**Na Mohab Dominick, KAHAMA**

SERIKALI mkoani Shinyanga imebaini uvamizi wa shughuli za uchimbaji wa dhahabu kwenye eneo la Shule ya Msingi Mwabomba, Halmashauri ya Ushetu, wilayani Kahama.

Akitoa taarifa hizo juzi kwa vyombo vya habari, Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Shinyanga, Injinia Joseph Kumburu, alisema kuwa uvamizi huo umebainika Februari 10, mwaka huu, baada ya Ofisi ya Madini Kahama kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama vya wilaya kutembelea eneo la Mwabomba lililovamiwa na wachimbaji wadogo kuanzia Februari 5, mwaka huu.

Alisema, eneo hilo lipo kwenye leseni ya utafiti wa Kampuni ya Carton Miyabi na maombi yake ni ya uchimbaji wa kati (ML).

Alifafanua kuwa eneo hilo lina mgogoro wa muda mrefu baina ya wachimbaji wadogo waliopo kwenye eneo hilo na ambao awali walikuwa na makubaliano maalum na kampuni hiyo kwamba wataruhusiwa kuchimba baada ya taratibu zote za fidia ama majadiliano ya kutatua mgogoro huo kupatiwa ufumbuzi.

Kumburu alisema yaliobainika wakati wa ukaguzi ni kuwa viongozi wa shule na kijiji kuingia makubaliano na baadhi ya wafanyabiashara, kukodi maeneo ya shule kwa ada ya Sh. 20,000 na kulipa Sh. 1,000 kwa siku kinyume cha taratibu na sheria za madini.

Alisema viongozi wa kijiji na shule wanakusanya kodi ya Sh. 1,000 kwa mfuko unaozalishwa kutoka kwenye mawe na hadi Februari 9, wamekusanya Sh. 617,000.

Kadhalika alisema uongozi wa shule unagawa mgao wa mawe na kuchukua Sh. 2,500,000 kama mapato ya mmiliki wa ardhi kati ya kijiji na shule na kuongeza kuwa kuna maduara ya mashimo kati ya 200 hadi 250 ambayo yanachimbwa na mengine yakiwa yamesitisha uchimbaji huo kutokana na wachimbaji hao kutopata dhahabu ya kutosha.

Alisema kuwa pia kamati hiyo ilibaini upatikanaji wa dhahabu kati ya gramu tano hadi sita kwa mfuko mmoja wa mawe baada ya kusagwa na kuchenjuliwa huku uchimbaji wa dhahabu na shughuli za biashara ukifanyika ndani ya eneo la shule hiyo.

Alisema kuwa eneo hilo lina-

ENDELEA UK 8

## HABARI KITAIFA

# Kina Papa Msofe waunganishwa kesi ya uhujumu

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYABIASHARA Marijani Msofe, maarufu Papa Msofe (53), na Fadhil Ibrahim (61), wameunganishwa na Wakili wa Kujitegemea, Abdul Lyana (37), katika kesi ya uhujumu uchumi.

Watatu hao wanakabiliwa na mashtaka ya kuratibu genge la uhalifu kwa nia ya kujipatia fedha na kutakatisha zaidi ya Dola za Marekani, 26,250 (Sh. milioni 60.375).

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Augustina Mmbando wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam.

Wakili wa Serikali, Gloria Mwenda, alidai upande wa Jamhuri unaomba kubadilisha hati ya mashtaka na kuwaunganisha washtakiwa wawili na mwenzao katika kesi hiyo.

Hakimu Mmbando alisema mahakama yake imekubali washtakiwa kusomewa hati mpya ya mashtaka.

Mwenda alidai kuwa kati ya Januari Mosi na Desemba 30, 2019, jijini Dar es Salaam, washtakiwa wote watatu waliongoza genge la uhalifu kinyume cha sheria kwa lengo la kujipatia fedha.

Katika shtaka la pili na la tatu, ilidaiwa kuwa siku ya tukio la kwanza, washtakiwa wote watatu, walitakatisha fedha baada ya kujipatia kwa njia ya udanganyifu zaidi ya Sh. milioni 60 kutoka kwa Yasser Abdelhamad kwa kijifanya kuwa wangemuuzia tani 25 za madini ya shaba huku wakijua si kweli.

Hata hivyo, washtakiwa hao hakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi.

Upande wa utetezi ulidai kuwa unaomba muda wa kuwasiliana na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kwa ajili ya kujadiliana kuhusu washtakiwa kukiri mashtaka yao.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa hauna pingamizi na ombi la utetezi.

Hakimu alisema kesi hiyo itatajwa Februari 17 mwaka huu na washtakiwa wataendelea kukaa mahabusu.








MFUKO WA MAENDELEO YA

KIPINDI CHA PILI CHA AWAMU YA TATU

**UTANGULIZI**

Kipindi cha Kwanza cha Awamu ya Tatu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF kilitekelezwa kuanzia 2012 na kukamilika Desemba 2019. Utekelezaji ulifanyika katika halmashauri 159 za Tanzania bara, Unguja na Pemba na kufikia kaya milioni1.1 zenye zaidi ya watu milioni 5.

Tathmini ya utekelezaji wa sehemu ya kwanza inaonyesha kuwa kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa Mpango huu umefanikisha azma ya serikali ya kupunguza umaskini nchini. Takwimu zinaonesha kwamba umaskini wa mahitaji ya msingi umepungua kwa asilimia 10 na umaskini uliokithiri umepungua kwa asilimia 12 kwa kaya maskini.

Utekelezaji umewezesha walengwa kujikita kwenye ufugaji, uvuvi, kilimo na biashara na kujiimarisha kiuchumi. Vile vile Mpango umeongeza idadi ya watoto kutoka katika kaya maskini kuandikishwa shule kwa kiwango cha asilimia 7.2. katika sekta ya afya, Mpango umeongeza mahudhurio ya kliniki kwa watoto walio na umri chini ya miaka 5 kwa kiwango cha asilimia 1.5

**Kipindi cha Pili cha Awamu ya Tatu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)**

Kipindi cha Pili kinatekelezwa katika halmashauri 185 za Tanzania bara, Unguja na Pemba katika vijiji/mitaa/shehia zote ikiwa ni pamoja na Vijiji/Mitaa/Shehia zaidi ya 5,000 ambavyo hazikufikiwa katika utekelezaji wa kipindi cha Kwanza. Kipindi cha Pili cha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kitafikia kaya milioni 1.4 zenye watu wapatao milioni 6 kote nchini.

Madhumuni ya Kipindi cha Pili cha TASAF ni kuwezesha kaya zilizoandikishwa kutumia fursa za kuongeza kipato, huduma za kiuchumi na kijamii na kuendeleza rasilimali watu husussan watoto.

Taarifa ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya wa mwaka 2011/2012 inaonesha asilimia 28.2 ya watanzania wanaishi katika umaskini huku asilimia 9.7 wanaishi katika umaskini uliokithiri hivyo utekelezaji wa Kipindi cha Pili utawezesha kaya maskini kujikwamua kutoka kwenye umaskini na kufanya kazi na kujiimarisha kiuchumi na kuiwezesha nchi kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025

Utekelezaji wa Kipindi cha Pili cha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

Shughuli kuu zitakazofanyika ni kutoa fursa ya ajira za muda kwa kaya maskini zenye watu wenye uwezo wa kufanya kazi kushiriki katika shughuli za uzalishaji na kuboresha miundombinu ya barabara za vijijini, elimu, afya, maji na hifadhi ya mazingira. Kuhamasisha walengwa kujiunga katika vikundi vya kuweka akiba na kuwekeza katika shughuli za uzalishaji mali na kutoa ruzuku kwa masharti ya elimu na afya kama kichocheo cha mahudhurio ya watoto shuleni na kliniki ili kupata elimu na huduma za afya na hivyo kuwajengea maisha bora. Aidha wadau katika ngazi mbali mbali watajengewa uwezo kwa njia ya mafunzo ambayo yatawawezesha kutekeleza na kutimiza majukumu yao kwa ufanisi.

**Matarajio**

Matarajio ya Serikali kupitia utekelezaji wa TASAF ni kupunguza kiwango cha umaskini kwa kutoa fursa kwa walengwa kushiriki kwenye kazi za kilimo na uzalishaji na hivyo kuchochea ukuaji wa viwanda, kuboresha miundombinu ya elimu afya hivyo kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto na kuongeza kiwango cha wanafunzi wanaomaliza darasa la saba na kupitia miradi ya kuongeza kipato kaya maskini ziweze kuboresha lishe kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano, na kupunguza udumavu na utapiamlo kwa watoto.

***Kipindi cha Pili cha Awamu ya III ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kitazinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.***

***Kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere Dar es Salaam, tarehe 15/02/2020***

215625502


# Watoto 125 watelekezwa mwaka mmoja Pemba

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

WATOTO 125 wametelekezwa Wilaya ya Wete kuanzia Januari hadi Novemba mwaka 2019.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi, Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Wete, Haroub Suleiman Hemed, alisema kati ya watoto hao waliotelekezwa, wanawake ni 63 na wanaume 62.

Alisema kuwa katika Ofisi ya Ustawi wa Jamii Wilaya ya Wete, jumla ya kesi 51 za utelekezwaji zimeripotiwa mwaka 2019, ambapo watoto 125 wametelekezwa.

"Kati ya kesi hizo za utelekezwaji wa watoto, kesi 40 zilipata ufumbuzi, kesi sita tulizipeleka Mahakama ya Kadhi kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi na tano zinaendelea kushughulikiwa," alisema ofisa huyo.

Aidha, alisema katika kuhakikisha wanapambana na hali ya udhalilishaji katika wilaya hiyo, Ofisi ya Ustawi wa Jamii ilifanya mikutano 31 ya wanajamii mwaka jana, ambapo waliwafikia watu 1,025, wanawake 600 na wanaume 425.

Alieleza kuwa wameamua kufanya mikutano hiyo katika jamii ili kuielewesha dhana nzima ya udhalilishaji na madhara yanayoweza kujitokeza.

"Kesi za udhalilishaji zimekuwa zikiripotiwa siku hadi siku zikiwamo za utelekezwaji wa watoto, na unapowatelekeza watoto ndio chanzo cha udhalilishaji mwingine kama kubaka, kutorosha na kulawiti," alisema.

Alisema changamoto zinazowakabili katika kukabiliana na kesi hizo ni rushwa muhali iliyotawala katika jamii, ambapo wanashindwa kufika katika vyombo vya sheria kuripoti ama kutoa ushahidi pale wanapohitajika.

"Kwa kweli rushwa muhali bado ni donda ndugu linalokwamisha kesi hizi zisimalize kwani jamii haiko tayari kutoa ushahidi na hii nahisi ndio inayosababisha pia upelelezi kukwama," alisema.

Akitaja mafanikio yaliyopatikana ni baadhi ya shehia kuunda kamati za maadili kwa ajili ya kusimamia tatizo la mporomoko wa maadili ili kupunguza ama kuondosha kabisa udhalilishaji katika jamii iliyowazunguka pamoja na jamii kuwa na mwamko wa kuripoti kesi hizo kwenye vyombo vya sheria.

"Kuwapo kwa ushirikiano kwa taasisi za Serikali na binafsi katika kusimamia na kufuatilia kesi za udhalilishaji, hii inasaidia sana kupambana," alieleza.

Ofisa Ustawi Hifadhi ya Mtoto, Nafhat Salim Yahya, alisema ili kuondosha udhalilishaji kwa wanawake na watoto, ni vyema jamii irejeshe malezi ya pamoja, kuchukuliwa hatua za haraka kwa mashauri yanayofikishwa mahakamani sambamba na kinababa waache kuzitelekeza familia, ili kuwakinga watoto kujiingiza katika vitendo viovu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha lengo lake ni zuri

**SERIKALI** imeweka muda wa mwisho kwa watoa huduma ndogo za kifedha nchini kukata leseni au kusajiliwa, lengo likiwa ni kufanya biashara hiyo kwa mujibu wa sheria.

Katika kutekeleza Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018 na kanuni zake zilizopitishwa mwaka 2019, watia huduma hizo ndogo wanapaswa kuwa wamejisajili au kukata leseni ifikampo Oktoba 31, mwaka huu.

Kwa maana hiyo, mtoa huduma ambaye hatakuwa amejisajili wala kukata leseni, atabanwa na sheria hiyo, ambayo kanuni zale zinaainisha adhabu mbalimbali zikiwamo faini na kifungo.

Ni jambo la kufurahisha kutokana na kutungwa kwa sheria hiyo pamoja na utekelezaji wake kuanza, kwa sababu huduma katika sekta ndogo ya huduma za fedha zimekuwa zikitolewa kiholela bila utaratibu.

Ni wakati ambao watumiaji wengi wa huduma hiyo wameathirika kwa njia mbalimbali, ikiwamo riba kubwa, mikataba ya ulaghai na wakati mwingine kupoteza fedha zao kutokana na ujanja ujanja uliokuwa unafanywa na baadhi ya watoa huduma hizo.

Kwa mfano, kuna matukio kadhaa ambayo wanachama wa vikoba wamejikuta wakipoteza fedha zao kwa kuambia na waweka hazina wao kuwa fedha zimepotea kwa njia za ajabu. Pia Saccos nyingi zimekufa na wanachama wake kupoteza fedha. Hayo yote yalisababishwa na kukosekana kwa sheria na kanuni za kuzisimamia.

Kwa upande mwingine, baadhi ya watumiaji wa huduma ndogo za fedha, wamekuwa tatizo kutokana na kushindwa kuwajibika ikiwamo kukiuka mikataba waliyosainiana na watoa huduma.

Kutokana na changamoto hizo na nyinginezo, ndio maana serikali ilianzisha mchakato wa kutunga sheria hiyo kuanzia mwaka 2007 na kufuatiwa na utafiti uliofanyika mwaka 2012, kwa lengo la kuzitafutia ufumbuzi.

Hata hivyo, pengine kukokana na jamii yetu kukosa uelewa wa kutosha kuhusiana na kuja kwa sheria hiyo, baadhi ya watu wanadai kuwa lengo la serikali ni kutaka kukusanya kodi kutoka katika madaraja mbalimbali yanayotoa huduma ndogo za fedha hususan vikoba na saccos.

Madai hayo hayana ukweli, bali ukweli ni kuwa lengo la serikali la kutunga sheria hiyo ni kutaka kuitambua sekta ndogo ya fedha, kuiratibu, kuiendeleza na kuiwezesha uku uwe endelevu, hivyo kusaidia wananchi wengi, ambao ndio watumiaji huduma hizo pamoja na kuwaondolea umaskini.

Kuja kwa sheria hii na kuanza kutumia mwishoni mwa mwaka huu, kunahitaji elimu ya kutosha kwa umma ili kuondoa upotoshaji wa aina mbalimbali yakiwamo madai kuwa lengo la serikali ni kutaka kodi.

Hata hivyo, jambo la kutia moyo ni kuwa kimeundwa kikosi kazi kwa lengo la kutoa elimu ambao wanatoka Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Tamisemi, Wizara ya Kilimo, Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na Kitengo cha Kilimo na Huduma za Fedha Vijijini (FSDT) pamoja na vyombo vya habari.


Kikosi hicho kwa kutumia njia mbalimbali za kuelimisha umma na kufika maeneo yote nchini kuhusu lengo na faida ya sheria hii, bila shaka mkakati huo utawawezesha watoa huduma kujisajili au kukata leseni kabla ya muda wa mwisho uliowekwa na serikali.

Pia tunaamini kuwa mamlaka zilizokamisiwa usimamizi na BoT, Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa upande wa Saccos na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa upande wa Vikoba, zitatimiza wajibu wake kwa kuwajibika katika kusimamia.

Tunasisitiza kuwa sheria hiyo umekuja wakati mwafaka ili kuiweka sekta ndogo ya huduma za fedha katika mstari.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com



Muungwana Lazima Nilonge

# Serikali iwamulike kwa kina wanaokuja kuwekeza bangi

Na Beatrice Moses

MAMLAKA za kiusalama nchini hivi karibuni, zimemkamata mwekezaji raia ya Poland, akiwa amelima bangi kwenye eneo lake alilokabidhiwa kwa uwekezaji wa hoteli na kituo cha yatima.

Taarifa kutoka kwa wananchi ndizo zinatajwa kuwa chanzo kilichowezesha kukamatwa kwa mwekezaji huyo, ambaye kwa hakika kama serikali isingechukua hatua za haraka, ni wazi angesababisha uharibifu mkubwa, ikiwamo kuchochea uhalifu katika eneo la utalii mkoa wa Kilimanjaro.

Serikali imekuwa ikihamasisha na kufanya jitihada za kuboresha mazingira ya uwekezaji na katika juhudi zake za mwka jana, ilitangaza kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya Mwaka 1996.

Ni sera iliyotungwa, ikiwa sehemu mojawapo ya jitihada za serikali kutatua changamoto zinazoikabili nchi katika kufikia matumizi bora ya rasilimali zake, ili kuwezesha kunufaika na kufikia malengo ya kiuchumi pia kijamii.

Ilibainisha wazi kwamba, mapitio hayo yanafanyika kutokana na mabadiliko mbalimbali ya mazingira ya biashara na uwekezaji katika ngazi za kitaifa, kikanda na dunia tangu kutungwa sera hiyo mwaka 1996.

Aidha, mapitio hayo yanadaiwa yatawezesha kutungwa sera mpya ya uwekezaji na kuandaa mkakati wa utekelezaji utakaowezesha nchi kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 kwa haraka.

Pia, itakuwa ni kutumia ipasavyo fursa zitakazotokana na uchumi wa kati na ilibainishwa kwamba, kazi hiyo inazingatia dhana ya uwazi na ushirikishwaji wa wadau wote muhimu.

Kitendo cha mwekezaji huyo ni kuhujumu juhudi zinazofanywa na serikali, kwa taarifa za awali alijitambulisha kuwekeza kwenye kituo cha yatima na hoteli tajwa.

Vyombo vya habari nchini viliripoti tukio la kukamatwa kwa mwekezaji huyo, ikibainishwa kuwa alianza kazi hiyo ya kuzalisha bangi na kuuza katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Inadaiwa baada ya kukamatwa, mwekezaji huyo alijaribu kuwashawishi maofisa waliokuwa katika kikosi kazi hicho kupokea rushwa ya Sh. milioni 10, ili 'mambo yaishe' na aliahidi kuwalipa kila baada ya mwezi mmoja, fedha Sh. milioni 40.

Kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa, ni kwamba aliingia nchini kwa ajili ya kuwekeza katika ujenzi wa hoteli za kitalii, karibu na uso wa Mlima Kilimanjaro, eneo la Njiapanda Himo katika Wilaya ya Moshi.

Kaimu Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kupambana na Kuzuia Dawa za Kulevya nchini, James Kaji, alithibitisha kukamatwa kwa mwekezaji huyo na wenzake watatu, akiwamo mkewe.

Mwekezaji huyo anadaiwa kuingiza nchini aina mpya ya mbegu ya bangi kutoka Hispania na alileta mkoani Kilimanjaro, ambako amekuwa akiivuna katika eneo maalum lililozungushwa uzio mrefu wa tofali. Hapo anadiwa aliichakata kwa kutengeneza malighafi mfano wa 'asali na jam' inayouzwa zaidi katika masoko ya nje, kupitia mipaka ya Pangani, Tanga na Zanzibar.

Ni mwekezaji anayetajwa kuendesha kilimo hicho haramu tofauti na maelezo yake ya uwekezaji na kwa mujibu taarifa ya awali ya Kamishna Jenerali Kaji, kuna baadhi ya wateja wa bangi inayozalishwa na mwekezaji huyo, wanaokuja kutoka Ulaya.

Waziri Mkuu wa Tanzania Kassim Majaliwa, alibainisha kuwa sema, Tanzania inaongoza kwa uwekezaji Afrika Mashariki na imemudu kuvutia uwekezaji wenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 1.18.

Majaliwa katika uwasilisho wake, kupitia Taarifa ya Mapitio na Mwelekeo wa Kazi za Serikali na makadirio ya mapato na Matumizi ya Fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2019/2020, kwenye mkutano wa 15 wa Bunge.

Uganda inatajwa kufuata kwa Dola za Marekani milioni 700, na Kenya dola za Marekani milioni 670. Ripoti mbalimbali za uwekezaji duniani zinaonyesha Tanzania imeongoza kwa kuvutia uwekezaji miongoni mwa nchi za Afrika Mashariki.

Taarifa ya Uwekezaji ya Dunia (World Investment Report) ya mwaka 2018 kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo (UNCTAD) inabainisha kiasi hicho cha uwekezaji.

"Taarifa nyingine ya 'The Africa Investment Index (AII) 2018' inaonyesha kuwa Tanzania imeshika nafasi ya 13 kati ya nchi 54 za Afrika katika kutoa fursa za masoko na vivutio vya uwekezaji."

Vilevile, Waziri Mkuu anasema kuwa taarifa iitwayo 'Where to Invest in Africa' (wapi kla kuwekeza Afrika) ya mwaka 2018, nayo imeonyesha Tanzania imeshika nafasi ya saba kati ya nchi 52 zinazovutia zaidi kwa uwekezaji barani Afrika.

Waziri Mkuu aliahidi kuwa serikali itaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara ikiwamo kutekeleza mapendekezo ya Mpango Kazi Jumuishi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji nchini.

Naamini kuwa serikali itaendelea kutoa elimu kwa wananchi jinsi ya kutoa taarifa kwa vyombo husika mara wanapobaini kuwa kuna matukio yasiyo ya kawaida yanatendeka katika maeneo yao ya kazi au makazi.

TANGAZO

# Absa Bank Tanzania kuleta mafanikio na kuwezesha ukuaji wa kiuchumi Tanzania

- Barclays Bank Tanzania yabadili jina lake, sasa kuitwa Absa Bank Tanzania Limited
- Yadhamiria kuleta ukuaji wa kiuchumi nchini

**Moja ya benki kubwa inayoongoza nchini imedhamiria kuendelea kukuza na kuleta maendeleo ya kiuchumi Tanzania baada ya kubadili jina lake kutoka Barclays Bank Tanzania Limited na sasa kuitwa Absa Bank Tanzania Limited.**

Absa Bank Tanzania Limited imeweka nadhiri hiyo ili kuweza kuimarisha historia yake ndefu ya kuihudumia Tanzania na kuendelea kufungua fursa mbali mbali zilizopo nchini. *"Leo tunaanza ukurasa mpya kama Absa Bank Tanzania Limited, ambalo ni jina la kampuni yetu mama. Kama taasisi, tunaamini katika utoaji wa fursa za mafanikio katika maisha, hivyo kuleta mchango chanya kwa wateja wetu, jamii na nchini kote tunapotoa huduma zetu,"* alisema Abdi Mohamed, Mkurugenzi Mkuu wa Absa Bank Tanzania Limited.

Kama kampuni tanzu ya Absa Group Limited, na moja ya kampuni 40 zilizojiandikisha katika Soko la Hisa la Johannesburg (moja ya soko kubwa la hisa barani Afrika), Absa Bank Tanzania Limited ina uhakika wa kutoa utaalamu wa hali ya juu utakaowawezesha watu na biashara kufanikiwa.

Kampuni hii imejisuka katika uchumi wa Tanzania kwa zaidi ya miaka saba na ina historia ndefu katika kuwekeza katika maendeleo ya nchi hii kwenye nyanja mbali mbali zikiwemo: biashara, viwanda, kilimo, nishati, biashara ndogo na kati, pamoja na miundombinu.

***Kifedha tumechangia jumla ya shilingi za Kitanzania bilioni 530 katika kipindi cha miaka miwili hadi mitatu iliyopita katika sekta mbali mbali za kiuchumi zikiwemo: Sekta ya Umma, Viwanda, Kilimo, Ujenzi, Biashara ya Mafuta na Gesi, Mawasiliano, na Biashara Ndogo na Kati, kwa kutaja chache. Tutaendelea kuwa mdau mkubwa kwa kuwekeza katika sekta hizi na kumsaidia mwananchi wa kawaida mwenye hitaji la kupata huduma za kifedha bora na uwekezaji salama ili aweze kulinda pesa anazozitafuta kwa jasho."*** alisema Mohamed.

Benki hii sasa inaadhimisha kuanza kwa zama mpya kama Absa Bank Tanzania Limited, benki halisi ya Kiafrika, yenye mfumo na mtandao mpana duniani kote. Kwa kutumia mkakati wake mpya wa kibiashara, benki imedhamiria kufungua fursa nyingi zaidi Tanzania na kuisaidia katika ukuaji wake wa kasi wa kiuchumi.



Katika dunia ambayo inakua kiushindani, moja ya rasilimali kuu ya nchi ni vijana wake, ambao ni nguvu kazi inayokua. Hivyo, Absa imekuwa ikikuza talanta za vijana wa Kitanzania kwa kutoa mchango wake kupitia mfumo wa elimu kwa miaka mingi sasa. ***"Tumetengeneza majukwaa ya kukuza maarifa kwa vijana, kutoa fursa za kuongeza uwezo wa vijana kuajiriwa, na kutoa msaada wa kitaalamu kuwezesha taasisi na wasimamizi husika kuboresha utoaji wa elimu bora kwa Tanzania. Dhamira yetu katika juhudi hizi itaendelea bila kuyumba,"*** alisema Mohamed.

Dhamira ya benki katika elimu inafuata rekodi ya kampuni yetu mama. Katika miaka michache iliyopita wamewekeza zaidi ya dola za Kimarekani milioni 24 katika elimu na kukuza ujuzi kwa kutoa: udhamini wa masomo kwa wanafunzi 3,600, fursa za elimu kwa matendo kwa wanafunzi zaidi ya 1,200, na kuwasajili zaidi ya watumiaji wapya 215,000 katika jukwaa la 'ReadyToWork' barani kote Afrika.

Kwa kutambua mchango wa wajasiriamali katika kuchochea ukuaji wa uchumi wa nchi, Absa Group Limited ilichangia zaidi ya dola za Kimarekani milioni 29 kwa ajili ya msaada wa kifedha kwa biashara ndogo na kati mwaka 2017, na kuzifikia zaidi ya biashara ndogo na kati 64,000 kupitia mpango wake wa kusaidia maendeleo ya biashara. Wakati huo huo, ilitoa mafunzo ya kibiashara na elimu ya kifedha kwa watumiaji 76,000.

Sambamba na kampuni yetu mama ya Absa Group Limited kuwa chachu ya maendeleo mazuri kwa jamii, Absa Bank Tanzania Limited imedhamiria kuwapa urahisi wajasiriamali nchini Tanzania kuweza kuanzisha na kukuza biashara zao. Afrika ni bara la watendaji, wanaojituma na kujitoa zaidi kila siku ili kuweza kukamilisha mambo yao. Tumehamasika na moyo huu ambao hausiti kugeuza kila changamoto kuwa fursa. Kama taasisi, tunaamini katika utekelezaji, na kuwasaidia watu kupata maarifa ya kufanikisha mipango yao. ***Ndani ya Absa, huu tunauita "Uafricanacity,"*** alisema Mohamed.



Wakati huo huo, Absa Bank Tanzania Limited imezindua kampeni mpya inayojumuisha dhana nzima ya 'Africanacity' katika kuunga mkono uzinduzi wa chapa yake hiyo mpya. Chapya mpya ya Absa pia imetekelezwa katika benki zingine za Barclays zilizo chini ya Absa Group Limited katika nchi kama Botswana, Ghana, Kenya, Mauritius, Seychelles na Zambia. Chapa hii mpya pia ilizunduliwa nchini Uganda na Mozambique mwezi Novemba 2019.

Absa Group Limited ni benki halisi ya Kiafrika yenye uwepo katika nchi 12 barani Afrika, na ofisi za kimataifa jijini London, huku ikitegemea kufungua ofisi nyingine jijini New York hivi karibuni. Mchakato wa kubadilisha chapa katika matawi, ATM, fomu, anuani, vifaa vya kazi maofisini, majukwaa na mengineyo katika zaidi ya nchi 12 ni mchakato mkubwa wa mabadiliko ya chapa kuwahi kutokea barani Afrika. Zoezi hili linatarajia kukamilika katikati ya mwaka 2020, bila kuathiri utoaji huduma wa benki hii.




**Benki ya Barclays Tanzania** imebadilisha jina lake rasmi kuwa **Benki ya Absa Tanzania**, na tarehe 10 Februari 2020 ndipo rangi za bluu tulizozizoea zilibadilika kuwa nyekundu. Pichani tunaona sherehe ya ufunguzi ambapo kutoka kushoto kwenda kulia ni; **Irene Singati-Giattas** ambaye ni Mkuu wa Utekelezaji na Sheria katika Benki ya Absa Tanzania Limited, **Godfrey Nyaisa** ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa BRELA, **Dk. Benard Kibese** ambaye ni Naibu Gavana wa Benki ya Tanzania, **Abdi Mohamed** ambaye ni MD katika Benki ya Absa Tanzania Limited, **Tuse Joune** ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Mabenki Tanzania na **Simon Mponji** ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi katika Benki ya Absa Bank Tanzania Limited.

***"Benki ya Absa inaendelea kuwa na matumaini juu ya uchumi wa Tanzania na imejikita katika hali nzuri ya uchumi na sera zinazowezeshwa na Benki ya Tanzania. Kwa hivyo, benki imewekeza TZS Bn15 tulivyokuwa tunabadilika kuwa Absa, hususan katika uboreshaji wa teknolojia, uboreshaji wa majengo na mafunzo.***

***Ujumuishaji wa kifedha ni eneo lingine muhimu kwa Absa, na tutafanya kazi na wadau wote katika eneo hili kuhakikisha kuwa Absa inasaidia kufanikiwa kwa ujumuishaji mkubwa wa kifedha nchini."***

**Abdi Mohamed**, Mkurugenzi Mtendaji.

# Waziri Mkuu awapa hadi Mei wadaiwa NHC kulipa madeni

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameuagiza uongozi wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) uwaandikie barua wapangaji wote wanaodaiwa kodi na shirika hilo na wahakikishe zimelipwa ifikapo Mei 30, mwaka huu.

"Orodha ya wadaiwa niliyonayo hapa ni kubwa na wengine inaonyesha wamehama na wameondoka bila kumalizia kodi zao. Hawa wote ni lazima tuwafuatilie na walipe madeni yao," alisema.

Alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na viongozi na wajumbe wa Bodi ya Shirika hilo kwenye kikao kilichofanyika ofisini kwake, jijini Dar es Salaam.

"Taasisi zote za serikali ambazo zimepanga kwenye nyumba za shirika ni lazima zilipe madeni. Chombo chochote cha serikali kinaishi na bajeti, kwa hiyo hata kama wamejenga ya kwao, walipaswa walipe kabla hajahama."

"Waandikieni barua wadaiwa wote ili walipe. Tunaelekea mwishoni mwa bajeti ya mwaka huu, na hawa wote wawe wamelipa ifikapo tarehe 30 Mei, 2020. Nami nipate orodha ya taasisi za serikali zinazodaiwa ili niwafuatilie; nitawaita Makatibu Wakuu wao mmoja mmoja. Hao wadaiwa binafsi wachukulieni hatua stahiki," alisisitiza.

Waziri Mkuu alisema madeni ambayo taasisi za serikali zinadaiwa yanafikia Sh. bilioni 4.3 na kama zitalipwa zote hizo, zitalisaidia shirika kuendelea na mpango wake wa ujenzi wa nyumba nafuu kwenye maeneo mbalimbali.

Wakati huo huo, Waziri Mkuu amelitaka shirika hilo lijielekeze kwenye ujenzi wa nyumba bora na za bei nafuu kwa sababu mahitaji ya nyumba nchini bado ni makubwa. "Simamieni suala hili, ili tupate nyumba nzuri na za bei nafuu. Simamieni wataalamu wenu ili wasikadirie miradi ambayo bei zake zitakuwa juu sana na kisha wananchi wetu washindwe kumudu. Ni lazima mhakikishe kuwa wananchi wa kipato cha chini wananufaika na uwepo wa shirika," alisema.

Alisema wataalamu hao wanahitaji kudhibitiwa kwa sababu sehemu kubwa ya malighafi inapatikana hapa nchini. "Hivi sasa kokoto, nondo, mabati na vifaa vingi vya ujenzi vinazalishwa hapa nchini, siyo kama zamani. Iweje bei ya kuuza nyumba inakuwa ya kutisha?" Alihoji.

Pia, Waziri Mkuu aliwataka viongozi hao waimarishe ukusanyaji wa mapato ya shirika hilo kwa kuhakikisha kodi zinakusanywa kwa njia ya kielektroniki. "Tuache tabia ya kuruhusu maofisa kwenda nyumba kwa nyumba na kudai Sh. 500,000 kwa risiti za kuandika. Tumieni control number, ili mwananchi aweze kulipia kwa simu au benki na hela inaingia moja kwa moja katika shirika," alisema.

Akitoa taarifa ya shirika hilo mbele ya Waziri Mkuu, Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Dk. Sophia Kongele, alisema shirika hilo linawadai wapangaji waliohama na waliopo ambao wengi wao ni wizara na taasisi za Serikali na akaomba wahimizwe kulipa ili wao waweze kuendesha shirika kwa ufanisi.




Meneja wa NMB Kanda ya Magharibi, Sospeter Magesse (kushoto), akimkabidhi Mkuu wa Wilaya ya Kaliua, Abel Busalama mashuka. Katikati ni Mkurugenzi wa Wilaya hiyo, Dk. John Pima akishuhudia. Benki hiyo imetoa vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni 35 kwa zahanati mbili za Shinyanga na Hospitali ya Kaliua. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Magufuli atikisa mawaziri vigogo

INATOKA UK 2

nimeambiwa kuna Sh. milioni 500 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa mochwari, kama ni kweli au ndoto, basi mfute, kiasi hicho cha fedha kinajenga kituo cha afya na si jengo moja."

WIZARA YA ARDHI

Rais Magufuli alimtaka Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Lukuvi, kuhakikisha ndani ya wiki moja, anarejesha umiliki wa ardhi wa ekari 750 kutoka wizarani kwenda kwa Halmashauri ya Kigamboni.

"Mawaziri mliopo hapa mfikishieni salamu mwenzenu, ndani ya wiki moja umiliki uwe umerudi kwa halmashauri, utoke kwa wizara," aliagiza.

Rais Magufuli pia aliuonya uongozi wa Halmashauri ya Kigamboni kuhusu matumizi ya ardhi hiyo, akieleza kuwa wakipewa umiliki wake, wahakikishe wanaitunza kwa maendeleo yao.

"Mkishapewa ardhi, pangeni wenyewe, jengeni kama ni kiwanda au ofisi ya CCM, sasa isije mkarudishiwa halafu iwe fujo," aliagiza.

**NYUMBA ZA WATUMISHI**

Kiongozi huyo wa nchi pia aliagiza watumishi wa wilaya hiyo kuishi wilayani humo, kujengwa kwa nyumba za watumishi ndani ya kipindi cha miezi sita.

Alitoa muda wa wiki moja kwa watumishi wa wilaya hiyo kuhakikisha wanahamishia makazi yao katika wilaya hiyo ili kuwarahisishia huduma wananchi.

"Ndani ya wiki hii, nataka mhamie Kigamboni, zile nyumba za NSSF mkakae mwaka mmoja bure, mlale Kigamboni muamke Kigamboni," aliagiza.

Rais Magufuli alimwagiza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, kutafuta Sh. bilioni mbili kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi wa wilaya hiyo na ujenzi wake ukamilike ndani ya kipindi cha miezi sita.

**BILIONI 36/-**

Rais pia aliagiza wizara husika kusimamia kukamilika kwa ujenzi wa kipande cha barabara yenye urefu wa kilometa mbili.

"Ninafahamu hapa Kigamboni kuna kipande cha barabara kina urefu wa kilometa mbili, mkandarasi amesaini mkataba kwa Sh. bilioni 2.1 na NSSF, hakuna barabara Tanzania ilishawahi kujengwa kwa bei hiyo.

"Na hivi sasa nimeambiwa mkandarasi anadai fedha zingine Sh. bilioni 36, waziri upo, mkurugenzi upo, nataka ndani ya siku saba mlimalize suala la mkandarasi, serikali haiwezi kulipa hizo Sh. bilioni 36, ajenge kwa makubaliano ya awali na kama hataki mfukuzeni, halafu tukutane mahakamani," aliagiza.

Rais Mgufuli pia aligiza fedha za mfuko wa barabara zitakazotengwa kwa ajili ya Jiji la Dar es Salaam mwaka ujao wa fedha, zote zipelekwe wilaya mpya za Kigamboni na Ubungo kwa ajili ya ujenzi wa barabara.

Alisema Sh. bilioni 600 zilizotengwa awali kwa ajili ya ujenzi wa barabara katika jiji hilo hazikupelekwa katika Wilaya ya Kigamboni.

"Kigamboni haikunufaika hata kidogo na fedha hizo, hata barabara zilizostahili kujengwa hazikujengwa, Km 78 za barabara za mzunguko zingeweza kujenga kutoka Mjimwema hadi Kimbiji, na ni barabara iliyopo katika ilani ya CCM," alisema.

**UJENZI MABONDENI**

Mbali na wizara tajwa hapo juu, Rais Magufuli pia aliigusa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), akitoa agizo kwa wakazi wanaoishi mabondeni kuhakikisha wanahama kwa kuwa serikali haitakuwa na msaada wowote kwao pindi watakapokumbwa na mafuriko.

Alisema wananchi wanapaswa kuyatumia mabonde kwa ajili ya kilimo na siyo makazi, akiwataka Watanzania kuutumia msimu huu wa mvua kama fursa ya kilimo.

# Uvamizi machimbo madini waibua ulaji

INATOKA UK 4

hatarisha usalama wa wananchi kutokana na mashimo mengi kukaribiana na uchimbaji bila kuzingatia utaratibu na kutokuwa na msimamizi.

Pia imedaiwa kuwa ipo mivutano ya mgawanyo wa mapato yanayotokana na mgao wa mawe baina ya wachimbaji, viongozi wa kijiji, kitongoji na shule kutokana na kutojua utaratibu wa uchimbaji.

Alisema kuwa walibaini kuwapo wizi wa mawe nyakati za usiku unaofanywa na walinzi na baadhi ya viongozi wa kijiji na walimu.

Ofisa madini huyo alisema kuwa licha ya mkutano wa wanakijiji na wadau, waliketi kikao kingine cha ndani ambacho kilibaini kuwapo na mgogoro baina ya viongozi, wananchi na wachimbaji huku chanzo kikiwa makundi mawili yaliogawanyika ya upande unaomtaka mwekezaji kuendelea na shughuli za uchimbaji na wanaotaka mwekezaji huyo kuachia baadhi ya maeneo yamilikiwe na wachimbaji wadogo.

**MAELEKEZO YALIOTOLEWA**

Kamati hiyo ilielekeza wafanyabiashara wote waliopo kwenye eneo la shule kuondoka kwenye eneo hilo kuanzia Februari 10 na wote waliokuwa wamechangishwa hela kwa ajili ya kupewa maeneo warejeshewe fedha zao.

Kamati iliyoundwa kusimamia mgao wa mawe yaliyopo katika eneo hilo ilielekeza yagawiwe kwa kuzingatia utaratibu wa asilimia za migao pamoja na mwongozo wa Tume ya Madini huku viongozi wa kijiji na shule wakipewa jukumu la kusimamia wachimbaji kusitisha kupita kwenye maeneo ya shule ili kuepusha uchafuzi na uharibifu wa mazingira.

Alisema, wachimbaji wanapaswa kutambua kuwa eneo wanalochimba ni la shule na hawaruhusiwi kuendelea na uchimbaji katika maeneo hayo, hivyo watambue kuwa watatakiwa kuondoka kwenye eneo, huku akiahidi kutoa taarifa kwa Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha ili naye afike kujionea.

## Chato yapata ofisi ya mwendesha mashtaka

**Na Daniel Limbe, CHATO**

SERIKALI imeanzisha rasmi ofisi ya taifa ya mwendesha mashtaka wilayani Chato mkoani Geita ili kuhakikisha inapunguza wingi wa kesi za makosa mbalimbali kwa lengo la kuongeza muda wa uzalishaji mali kwa jamii badala ya kutumia muda huo kuhudhuria mahakamani.

Hatua hii inatazamiwa kwenda sambamba na kaulimbiu ya maadhimisho ya Wiki ya Sheria Mwaka 2020 ambayo ni " Uwekezaji na Biashara Wajibu wa Mahakama na wadau kuwekeza mazingira wezeshi" ili kuhakikisha Tanzania inafikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Hayo yamebainishwa na Mwendesha Mashtaka wa Serikali Wilaya ya Chato, Anosisye Erasto, wakati akitoa hutuba yake kwenye maadhimisho ya kilele cha wiki ya sheria nchini, akisema ofisi yake inalo jukumu kubwa la kuendesha kesi au kufuta kesi ambazo zitaonekana hazina mashiko mbele ya jamii.

Aidha, alitoa wito kwa jamii kuheshimu sheria za nchi ili kuepuka kupoteza muda mwingi wa uzalishaji mali kutokana na kuhudhuria mahakamani mara kwa mara.

Kwa upande wake Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Chato, Odira Amworo, amedai kuwa ofisi yake imejipanga kuhakikisha mashauri yote yanamalizika kwa wakati kwa mahakama zote zilizopo wilayani humo ili kuongeza imani kwa jamii.

Aidha, alisema miundombinu ya mahakama zilizopo wilayani humo ni mibovu sana huku akiiomba serikali kusaidia kutatua changamoto hiyo ili kuongeza ari ya mahakimu kutimiza wajibu wao haraka.

Alisema licha ya changamoto zilizopo kwenye mahakama hizo, wanaendelea kuwahudumia wananchi kadri iwezekanavyo kwa lengo la kutoa haki.

Aliipongeza serikali kujenga jengo jipya la mahakama ya wilaya hiyo, ambalo limeongezewa nguvu kazi ya utendaji kwa kupewa mahakimu wanne, ambapo kwa mwaka 2020 mahakama imeanza na kesi 80 pekee ukilinganisha na mwaka jana ambapo kulikuwa na kesi 187.

Mwakikishi wa Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS) Kanda ya Geita, Wakili Traiford Bashaya, aliwaomba waendesha mashtaka wa serikali kuondokana na imani potofu ya kwamba mawakili wa kujitegemea kazi yao ni kuwatetea wahalifu.

"Jukumu moja wapo la mawakili ni kuhakikisha wanaisaidia mahakama kufikia maamuzi ya haki na kwa wakati mwafaka wala siyo kutetea uhalifu," alisema Bashaya.

# Madaktari 106 wapewa mafunzo

**Neema Emmanuel na Rose Jacob, MWANZA**

MADAKTARI nchini wametakiwa kutoa tathmini zilizo sahihi wanapopokea wafanyakazi wagonjwa waliopatwa na ajali wawapo kazini ili kuwasaidia kupata fidia sahihi.

Rai hiyo ilitolewa kwenye mafunzo yaliyotolewa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) kwa madaktari 105 wa Kanda ya Ziwa ya kufanya tathmini ya ulemavu unaotokana na ajali na magonjwa ya saratani, jijini Mwanza.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, alisema wafanyakazi ni kundi nyeti lenye umuhimu katika kuleta maendeleo ya jamii hivyo mafunzo hayo yatakuwa chachu ya watu kutendewa haki na kupata fidia zinazostahili.

Alisema upungufu unatokea kutokana na watu wengi kutokuwa na uelewa wa taratibu zinazotolewa na taasisi zao hivyo elimu hiyo itachangia watu wote kuwa na uelewa wa aina moja huku sheria ikisimamia kwa namna bora zaidi fidia ya wafanyakazi.

"Siyo ukipigana na mkeo unadai fidia, lakini ukiwa sehemu ya kazi au ikathibitika madhara uliyoyapata yanatokana na kazi yako utapata fidia kwa sababu fidia ni haki yako na wafanyakazi rasilimali kubwa katika kuchochea maendeleo ya taifa," alisema Mongella.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa WCF, Anselim Peter, alisema wanatoa elimu hiyo ya siku tano kwa madaktari kwa kuwa ni mtu wa kwanza kumuona mgonjwa ambaye ndiye anatakaye tambua kiwango cha ulemavu alioupata ili aweze kulipwa fidia.

Pia alito rai kwa waajiri kutambua wafanyakazi wao ndio viini vya maendeleo hivyo wanapopata ajali watoe taarifa ili mfanyakazi huyo aweze kupatiwa matibabu bure na fidia endapo akifariki wategemezi wake walipwe na kuwataka washiriki kuzingatia elimu inayotolewa ili waweze kutekeleza majukumu kwa weledi wa hali ya juu.

Mwanasheria wa WCF, Abraham Siyovelwa alisema changamoto kubwa wanayokabiliana nayo ni baadhi ya wafanyakazi wasio waaminifu kujipandikizia ugonjwa ili waweze kulipwa fidia.

"Tulianza kupokea madai ya udanganyifu watu akiamini wanaweza kupata hela kirahisi wengine wakigushi document za ugonjwa wakiongeza viwango vya ulemavu tunatoa mafunzo haya ili kuwapa uelewa madaktari pia tunazo kesi chache ambazo tunazishughulikia," alisema Siyovelwa.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongela, akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Sizu, Kata ya Kagunguli, wilayani Ukerewe juzi, kuhusu masuala ya maendeleo na changamoto za afya. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

## Bil. 90/- kutoa mafunzo wataalamu elimu

**Na Allan Isack, ARUSHA**

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetumia Sh. bilioni 90, kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wataalamu wa elimu, walimu wa vyuo vya ualimu na kununua vifaa vya kufundishia kwenye vyuo hivyo.

Hayo yalisemwa jana jijini Arusha na Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard Akwilapo, wakati wa ufunguzi wa mkutano wa wadau wa kitengo cha kuendeleza elimu ya ualimu (TSP).

Akwilapo alisema wametumia Sh. bilioni 90, kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika vyuo vya ualimu vya serikali, shule za msingi na sekondari za mfano za serikali na kutoa mafunzo kwa walimu wa vyuo na shule hizo.

Alisema fedha hizo, zimetolewa na Serikali ya Canada kwa ajili ya kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo walimu wa vyuo hivyo wanapokuwa katika majukumu yao ya kikazi.

"Lengo la mkutano huu, ni kujadili na kuangalia matokeo ya mradi huu ulioanza mwaka 2018, ukiwa na lengo la kuimarisha vyuo vya ualimu nchini kutoa mafunzo bora," alisema Akwilapo.

Alisema licha ya mradi huo, kutoa mafunzo na ukarabati kwa vyuo vya ualimu, pia wameanza ujenzi wa chuo kipya cha ualimu cha Kabanga, unaotarajiwa kukamilika mwezi Juni, mwaka huu.

Pia alisema kupitia mradi wa TESP, wametoa vifaa vya kufundishia katika vyuo, shule za msingi na sekondari za mfano ili kuongeza ufaulu na kuboresha sekta ya elimu.

"Tunaishukuru Serikali ya Canada kwa kutupatia fedha hizi kwa kuwa zimeleta mchango mkubwa katika sekta ya elimu," aliongeza.

Mratibu wa Mradi wa TESP, Ignas Chonya, kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Idara ya Sera na Mipango, alisema mradi huo, umejikita zaidi kwenye maeneo ya miundombinu, ikiwamo kufanya ukarabati wa majengo, kununua vifaa vya kufundishia, kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wataalamu na walimu wa vyuo hivyo na shule za mfano za msingi na sekondari.

Kansela Mkuu wa Ushirikiano na Maendeleo wa Ubalozi wa Canada hapa nchini, Gwen Walmsley, alisema mradi huo, unafahamu umuhimu wa Sera ya Serikali ya Tanzania ya Mwaka 2015, ya kutoa elimu bure kwa wanafunzi wa shule ya msingi na sekondari.

Alisema tangu mwaka 2015, sera ya elimu bila malipo imesaidia wanafunzi milioni 10.6 wa shule za msingi na sekondari kupata elimu bure.

Alisema Serikali ya Canada kati ya mwaka 2018/21 imejitolea Dola za Kimarekani milioni 180 kwa ajili ya vijana.

Alisema pia wamechangia Sh. bilioni nane kwenye suala la usaidizi wa kiufundi ili kuboresha utekelezaji wa kati kwa wataalamu.

# Waziri awatoa hofu wakulima ujio nzige

**Na Mathias Canal, ROME**

SERIKALI imewahakikishia wakulima na Watanzania kwa ujumla kuwa Tanzania haijavamiwa na nzige wa jangwani kama inavyoripotiwa na mitandao mbalimbali ya kijamii.

Kauli hiyo ya serikali ilitolewa jana na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alipozungumza na Balozi wa Tanzania Italia, George Madafa.

Mara tu baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Flumicino jijini Rome, Italia, Hasunga alisema kumekuwa na maneno yakienezwa, lakini hakuna nzige wa jangwani Tanzania.

"Mimi nawahakikishia wakulima na wananchi wenzangu wa Tanzania kuwa kumekuwa na taarifa zinazoenea kwenye baadhi ya vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kuhusu uwapo wa nzige wa jangwani nchini hususani mkoa wa Kilimanjaro, siyo za kweli, sisi tupo salama," alisema.

Aliongeza kuwa hakuna taarifa za kitaalamu zilizothibitisha uwapo wa nzige kwenye mikoa ya Kilimanjaro na Arusha, lakini akakiri kuwa kuna nzige wameonekana Kaunti ya Kajiado, Kenya takribani kilomita 50 toka mpakani na Tanzania.

Hasunga alisema wataalamu wa Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO), wanaendelea na ufuatiliaji wa viashiria vya uwapo wa nzige na tayari hatua za awali za kuwadhibiti endapo wataingia nchini zimechukuliwa.

Alisema kuwa hatua hizo ni pamoja na mashirika ya kimataifa ambayo Tanzania ni wanachama, kuiahidi Serikali ya Tanzania ndege tatu maalum za kunyunyizia dawa na uwapo wa dawa za tahadhali kwenye mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro.

Waziri Hasunga alitoa wito kwa wakulima, maofisa ugani na kilimo na wadau wote wa kilimo kuendelea kutoa ushirikiano wa taarifa sahihi kwa serikali endapo kutajitokeza viashiria vya nzige kwenye maeneo ya mashamba.

# Waitara amvaa Zitto Kabwe

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(Tamisemi), Mwita Waitara, amedai Mbunge wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe, anastahili kuhukumiwa na wananchi wake katika uchaguzi mwaka huu kutokana na kile alichokiita kukosa uzalendo kwa nchi.

Waitara alitoa kauli hiyo jijini Dar es Salaam wakati akifungua kozi fupi ya nane ya uongozi ya mwaka 2020 kwa viongozi kutoka Tanzania Bara na Zanzibar inayotolewa na Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC).

Alidai kiongozi yeyote anapaswa kuwa mstari wa mbele kuitetea nchi yake badala ya kuibomoa na anapaswa kutanguliza uzalendo mbele.

"Kwa mfano, kiongozi wa chama cha siasa unapotoka hapa ukaenda nje ya nchi unazungumza vibaya mambo ya nchi yako wakati kwenda huko umechukua kodi ya Watanzania, iwe ni posho, nauli au tiketi ya ndege mpaka mavazi unayovaa, vina jasho ya Watanzania humo, halafu unaenda unazungumza mabaya ya nchi yako.

"Lakini ukishamaliza kuitukana nchi yako na kuikashfu kule kwamba wazuie misaada, halafu ukimaliza unarudi tena pale ulipokuwa unapatukana," alilalamika.

Waitara alisema, mbali na viongozi wa serikali na taasisi zake kupatiwa kozi na NDC ya namna bora ya uongozi na kusimamia misingi ya kiutawala, pia kuna haja ya kutoa kozi hiyo kwa viongozi wa juu katika nyanja nyingine hususani wanaosimama kwenye majukwaa na kutoa kauli, hasa wanasiasa.

"Ndiyo maana nasema ni muhimu kwa 'level' (kiwango) fulani ya uongozi, hata kwenye vyama vyetu vya siasa, wakawa na uelewa wa umuhimu wa uzalendo.

"Mataifa mengine, huwezi kukuta mtu anarudi ulikotukana, hata kama kwao kuna mambo mabaya, akawa anaponda nchi yake, sijawahi kusikia mtu wa namna hiyo na akigundua kwamba unamhoji vitu ambavyo ni vya kuikosesha heshima nchi yake, atakukataza na huo mjadala atausitisha.

"Sasa, inashangaza Mtanzania, amesomeshwa na Watanzania, amekuzwa na Watanzania, amekula kodi za Watanzania masikini, anapata nguvu, utashi na uelewa kiakili, halafu anaenda kuiponda nchi yake nje ya nchi nyingine.

"Ndiyo maana nasema ni muhimu hawa watu nao ambao hawana uzalendo waelewe kwamba mwisho wa siku hata kama kuna tofauti za kisiasa, hata kama tutakinzana hoja kwa namna gani, ni lazima tutangulize uzalendo mbele na maslahi ya nchi yetu," alisema.

Mkuu wa Chuo hicho, Luteni Jenerali Peter Massao, alisema mafunzo hayo yameshirikisha viongozi wa ngazi za juu serikalini na taasisi zake kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wa namna misingi bora ya kiutendaji, namna ya kukabiliana na vikwazo vya uongozi, kufanya uamuzi kwa usahihi na weledi kwa mambo yanayohusu serikali na usalama wa taifa na kusimamia maadili na uzalendo katika taifa.

Alisema mafunzo hayo yamekuwa yakifanyika kwa viongozi mbalimbali na yamesaidia kwa kiwango kikubwa kuleta ufanisi kwa viongozi hao.



Mkuu wa Wilaya ya Kilolo, mkoani Iringa, Asia Abdallah (katikati), akikata utepe kuzindua jengo la ofisi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), wilayani humo, juzi. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Majaliwa kuongoza kongamano la uwekezaji mkoani Songwe

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, anatarajiwa kuongoza kongamano kubwa la siku tatu la uwekezaji katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe mwezi huu.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali mstaafu Nicodemus Mwangela, alisema jana jijini Dar es Salaam katika mkutano wa pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), Godfrey Simbeye, kuwa kongomano hilo ni muhimu kwa mustakabali wa kuvitangaza vivutio mbalimbali vya uwekezaji katika mkoa wake.

"Mkoa wa Songwe una kila fursa ya kujivunia katika sekta zote za kiuchumi na kongamano hili litatoa fursa kwa wawekezaji wa ndani na nje kujionea wenyewe," alisema Mwangela, na kuongeza kuwa maandalizi yamekamilika ambapo ofisi yake kwa kushirikiana na Taasisi ya Home of Events wamefanya kazi hiyo.

Alizitaja fursa za uwekezaji zilizopo kwenye mkoa wake ni kilimo, ufugaji, utalii, usafirishaji, madini na viwanda.

"Mkoa wa Songwe una miundombinu muhimu kwa uwekezaji kutokana na uwapo wa barabara ya kimataifa ya Tanzam, reli ya Tazara, uwanja wa ndege wa kimataifa na vingine vingi.

Alisema hivyo ni nafasi ya kipekee kwa wale wote wenye nia ya kuwa wafanyabiashara wakubwa kwenda kuwekeza Songwe.

Mwangela alisema viongozi mbalimbali, wafanyabiashara, wawekezaji wa kitaifa na kimataifa pamoja na wananchi watakaohudhuria kongamano hilo watapata fursa ya kufahamu kwa undani mazingira rafiki yaliyopo kwa ajili ya uwekezaji hususan katika sekta za kilimo na mifugo, maliasili na utalii, viwanda na biashara pamoja na sekta ya madini.

"Napenda kuwakaribisha wawekezaji, wafanyabishara na wananchi wote kushiriki kwa wingi na kujionea fursa mbalimbali zilizopo mkoani Songwe. Songwe ni lango la biashara kwa nchi za SADC, asilimia 70 ya mizigo hupita katika mpaka wa Tunduma kuingia nchini, hivyo soko la bidhaa zitakazozalishwa litakuwa pana," alisema.

Naye Simbeye alisema TPSF ni mwenyekiti katika baraza la biashara nla SADC, hivyo hawanabudi kuhakikisha wanachochea maendeleo hasa katika sekta ya biashara na uwekezaji.

Alisema Songwe ni moja ya mikoa yenye fursa nyingi na kutoa wito kwa vijana wanaotamani kukua kiuchumi kuchangamkia fursa hizo.

"Songwe ni mkoa wa kipekee sana, wito wangu kwa vijana pamoja na wanawake kuhudhuria kongamano hili kujionea fursa zilizopo na kuzitumia katika kujikwamua kiuchumi."





## Madiwani wakataa taarifa madai ya kudharauliwa

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUMERU**

MADIWANI wa Halmashauri ya Meru, wamekataa kusomwa kwa taarifa ya Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (Tarura) baada ya kudai kudharauliwa na mamlaka husika.

Wakiomba taarifa ya mwaka wa fedha wa 2018/19 kutosomwa na kuwasilishwa katika baraza hilo jana, madiwani hao walisema hawana shida na Tarura bali shida ni kwa Meneja wa Tarura wilayani hapo ambaye alimtuma Mwakilishi wake Mhandisi Baraka Sunga.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Nelson Mafie, alidai Tarura katika halmashauri hiyo wana dharau kwa Baraza la Madiwani kwa kuwa badala ya viongozi waliopewa mamlaka kusimamia barabara kuongea na madiwani hao, ili kujua changamoto za barabara na miundombinu kwa ujumla, wao wanaleta taarifa zao asubuhi kabla ya kikao ili zipitishwe au kujadiliwa.

"Hatunashida na Tarura bali tunashida na huyu Meneja wa Tarura katika halmashauri hii anatudharau sana na hata akileta taarifa zake tunambia azirekebishe hafanyi haya sasa na sisi leo hatutaki asome taarifa yao waliyoleta asubuhi hii," alisema.

Kabla ya taarifa hiyo kusomwa awali mwakilishi wa Meneja wa Tarura katika halmashauri hiyo Sunga aliomba kusoma taarifa hiyo ya mwaka wa fedha uliopita 2019/20.

"Nimekataliwa kuisoma ila kukataa taarifa ni kitu kingine tutaenda kufanyia marekebisho taarifa hii ili kesho tuje tena katika kikao hiki ili kuhakikisha maendeleo yanapatikana katika kutatua kero za barabara wilayani hapa," alisema.

Baadhi ya madiwani akiwamo Evelyne Kaaya, alisema ni vema mwasilishaji huyo angetoa taarifa kwa muda wa kutosha kwa madiwani wazipitie kabla ya kikao hicho ili jana asome taarifa yake japo hakuna matengenezo yoyote ya barabara wanayofanya na hali ya barabara mitaani ni mbaya.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, William Njau, alisema taarifa hiyo ina mambo mengi na inahusu miundombinu ya barabara, lakini tatizo Meneja wa Tarura anadharau madiwani hivyo taarifa hiyo isisomwe badala yake kikao cha bajeti kitaamua taarifa hiyo isomwe ili kurekebisha makosa katika taarifa zao kisha walete ili wajue pa kuanzia na barabara gani zimepewa kipaumbele kwa mwaka wa fedha 2020.

# Aeleza serikali inavyoibiwa katika 'dili' za ujenzi

**Na Mwandishi Wetu, ARUSHA**

OFISA Tarafa Kata ya Themi jijini Arusha, Felician Mtahengerwa, amempongeza Rais John Magufuli kwa kazi anayofanya ya kujenga nchi ili iachane na utegemezi wa misaada yenye masharti magumu.

Akizungumza jana na Nipashe ofisini kwake jijini hapa, Mtahengerwa alisema pamoja na mazuri anayofanya bado baadhi ya wasaidizi wake wanaiba fedha za serikali.

"Kwa mfano maeneo wanayoiba ni kwenye ujenzi wa stendi, kila mkoa sasa wapo wanajenga stendi za mabasi tena kwa mkopo, gharama za ujenzi stendi hizi sio halisia wanaweka cha juu na kama ukichunguza vizuri unaweza kukuta mkondo huu wa wizi unaanzia mbali hadi mkoani na kushuka kwenye halmashauri," alisema.

Alisema endapo wateule wote wa Rais wangefuata nyayo zake kupiga vita ufisadi kwa vitendo nchi ingepiga hatua haraka ya kimaendeleo.

Pia eneo lingine wanalotumia kula fedha za serikali ni la ujenzi wa masoko na dampo za kuhifadhia taka.

Mtahengerwa alisema hata kwenye ujenzi wa vituo vya afya, ukitumia force account gharama yake inapungua, lakini baadhi yao wanaomba Sh. milioni 500, huku wakijua gharama halisi Sh. milioni 300.

"Hili naomba Rais aliangalie sana na cha kushangaza unakuta gharama hiyo ya Sh. milioni 500 inakuwa kwa mikoa yote, wanasahau kuwa Dar es Salaam na Kigoma sio sawa, lakini kuna suala la umbali, upatikanaji wa vifaa, lakini wakitumia gari force account yote haya yakizingatiwa gharama zitapungua zaidi," alisema.

Alitaja eneo lingine la wapiga dili la ununuzi wa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa taasisi na huduma za serikali.

Akitoa mfano kwa Mkoa wa Arusha alisema bei ya maeneo mengi kwa ekari moja Sh. milioni 20, lakini serikali ikienda kununua wananunua kwa Sh. milioni 100 au zaidi.

Alisema viongozi wakubwa wanaweka msukumo mkubwa kuhakikisha maeneo hayo yananunuliwa kwa haraka ili maendelezo yafanyike.

"Lakini akitokea kiongozi mzalendo mteule wa rais akatilia shaka kwa kuhisi kuwa hilo ni dili atatengenezewa zengwe na kuchongewa kila mahali," alisema.

Aliomba Rais kuwa macho na baadhi ya wateule wake kwenye maeneo hayo ili serikali isiendelee kupata hasara.



Mama mchuuzi wa loshoro, akihudumia wateja wake katika viunga vya Jiji la Arusha jana. Loshoro ni chakula maarufu kwa makabila ya Wachaga, Wamaasai, Wameru na Waarusha hutengenezwa kwa mchanganyiko wa makande na maziwa ya mgando. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Nyumba 300 zazingirwa maji

**Na Jaliwason Jasson, MANYARA**

ZAIDI ya nyumba 300 za wakazi wa Wilaya ya Babati mkoani Manyara zimezingirwa na maji na zingine kubomoka kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Wilaya ya Babati, Elizabeth Kitundu, wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake kuhusu athari zilizotokana na mvua na namna serikali ilivyokabiliana nazo.

Kitundu alikiri mvua hizo kusababisha athari huku akisema watu wanne walipoteza maisha kwa kusombwa na maji, akiwamo mwanafunzi wa shule ya msingi (hakuitaja) ambaye alipoteza maisha wakati akitafuta kiatu chake kilichoangukia kwenye korongo.

Alisema nyumba zilizozingirwa na maji katika maeneo mbalimbali ni 342, zilizobomoka 54 na zilizoezuliwa na upepo ni 17.

Alisema athari kubwa walizozikuta kutokana na mvua ni kwa sababu ya wananchi kuharibu mazingira kwa kukata miti hasa magogo ambayo yanaenda kuziba karavati na mchanga kujaa kwenye madaraja.

Alisema serikali inawashukuru wananchi wa karibu na waathirika kwa hatua walizochukua za kuwasaidia kupata chakula na sehemu za kulala.

Kitundu alisema pamoja na misaada waliyopata, serikali kupitia kamati za maafa za vijiji, kata na wilaya nao walishirikiana kuokoa watu na kuwatafuta wadau ili kusaidia waliokumbwa na maafa hayo.

Alisema yanapotokea maafa wilaya haina fungu lolote la kutoa kwa waathirika badala yake wanawashirikisha wadau ili kukabiliana na madhara yanayotokea.

Pia alisema baada ya kuchukua hatua za dharura wanaiomba serikali kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu iwasaidie ili kukabiliana na maafa yaliyojitokeza.

Katika kuhakikisha mvua haiwaathiri watu tena, alisema Kijiji cha Minjingu kimetenga ekari 30 kuwapatia walioathirika, Kijiji cha Kakoi kimetenga ekari nane na Kijiji cha Vilima Vitatu kimeomba wapewe maeneo ya kujenga.

Mkazi wa Magugu Ignas Jacob, alisema madhara ya mvua mwaka huu ni makubwa kutokana na kusomba mazao shambani.

Mkazi mwingine Zabron Bahati aliishauri serikali kupitia kitengo cha maafa kuzunguka kutoa elimu wakati wote ili jamii ibadilike na kuacha kukaa maeneo ya mabondeni badala ya kusubiri maafa yatokee.





## Wachangishana kujenga zahanati ya kisasa

**Na Mary Mosha, SIHA**

WAKAZI wa Kijiji cha Roseline katika Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro wameanza kuchangishana fedha za kutekeleza mradi wa ujenzi wa zahanati ya kisasa, ili kukabiliana na matatizo ya kufuata huduma za afya zaidi ya kilomita 24 katika Mji Mdogo wa Sanya Juu.

Hadi kukamilika kwake, ujenzi wa zahanati hiyo unakisiwa kugharimu zaidi ya Sh. milioni 250.

Mkuu wa Wilaya ya Siha, Onesmo Biwelu, aliyasema hayo jana katika taarifa yake kwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Kilimanjaro, Yasini Lema, katika maadhimisho ya miaka 43 ya kuzaliwa kwa chama hicho.

Alisema wananchi wa Kijiji cha Roseline, wameamua kujenga kituo kipya cha afya ili waweze kuondokana na adha ya kutembea umbali mrefu kutafuta huduma za afya.

Alisema katika ujenzi huo ulianza mwaka 2017 kwa kuwekwa jiwe la msingi, lakini hadi sasa ujenzi huo haujakamilishwa na kwamba serikali imetoa Sh. milioni 150 kufikisha huduma ya umeme kwenye zahanati hiyo.

Alisema kwa sasa dawa na vifaa tiba vipo tayari na vinasubiri kukamilika kwa zahanati hiyo, ili ianze kutoa huduma kwa wananchi na kwamba huduma mbalimbali za afya zitaanza kutolewa katika zahanati hiyo.

Alisema anategemea ujenzi huo kukamilika baada ya miezi mitatu na kwamba huduma zitakazotolewa ni pamoja na zile za vipimo vya mabara, upasuaji, watoto na wazee na kwamba wananchi, taasisi, vikundi, mashirika mbalimbali ikiwamo CCM wamejitokeza kusaidia ujenzi wa zahanati hiyo.

Akizungumza na kushiriki ujenzi wa kituo hicho, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM, Mkoa wa Kilimanjaro, Yasini Lema, alitoa wito kwa wananchi kuendelea kujitokeza na kuchangia ujenzi wa zahanati hiyo ili iweze kukamilika na kuwa hudumia kwa wananchi.

Lema alitoa wito kwa Serikali ya Wilaya ya Siha, kuangalia namna ya kuunga mkono jitihada za wananchi kukamilisha ujenzi wa kituo hicho ili kiweze kukamilika na kutoa huduma za afya kwa wananchi.

Alitoa wito kwa serikali kuhakikisha miradi ya ujenzi unaofanywa na wananchi kamwe wasikubali nguvu zao kupotea bure kwa kutokamilisha miradi ya afya na elimu na kwamba miaka 43 ya kuzaliwa kwa CCM, kwa amani ni jambo kubwa la kumshukuru mwenyezi Mungu.

Alisema miaka 43 ni mingi na serikali iliyopo madarakani imefanya kazi kubwa ya kusimamia amani na kuleta maendeleo ya nchi katika nyanja mbalimbali ikiwamo sekta ya afya, elimu, maji, barabara.

# Same watafuta mwarobaini ongezeko ukatili watoto wa kike

**Na Godfrey Mushi, SAME**

SIKU chache baada ya Bunge kuelezwa kuwa Tanzania inatishiwa na ongezeko kubwa la vitendo vya ukatili wa kijinsia, maofisa wa serikali wilayani Same mkoani Kilimanjaro, wameanza kutafuta mwarobaini wa tatizo hilo kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Jana, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya ya Same, Charles Anatoly, alisema maofisa wa idara hiyo kwa kushirikiana na wenzao wa ustawi wa jamii, hivi sasa wanaendelea kufanyia kazi taarifa za madai ya kuwapo kwa vitendo vya ulawiti na ubakaji kwa wanafunzi ambavyo vinafanywa na baadhi ya walevi katika baa moja iliyopo katikati ya mji wa Same.

Maofisa hao wamelazimika kuanza kazi ya uchunguzi dhidi ya madai hayo kutokana na malalamiko ya baadhi ya wananchi hasa wanaharakati wanawake wanaounda Jukwaa la Vuguvugu la Mapinduzi ya Fikra kwa Mwanamke (Tapo) Wilaya ya Same.

Wiki iliyopita, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Peter Serukamba, wakati akiwasilisha bungeni taarifa ya utekelezaji wa majukumu na shughuli za kamati yake kwa mwaka 2019/2020, alisema matukio ya ukatili wa kijinsia yameongezeka nchini kutoka watu 31,996 kwa mwaka 2016 hadi kufikia 43,487 mwaka 2018 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 35.9.

Akizungumzia malalamiko hayo ya wanaharakati wanawake, Anatoly alikiri: "Zipo changamoto nyingi sana Wilaya ya Same na bahati nzuri wametoa mifano ya baadhi ya kata wanazotoka. Tatizo la ulawiti hasa kwa watoto wadogo linazidi kukua siku hadi siku. "Ukienda shule ya msingi (anaitaja) tatizo linazidi kuwa kubwa na mwaka jana tulienda pale kuna watoto walilawitiana na mmoja alikimbia na lile suala tulilipeleka Polisi na wanaendelea na uchunguzi. Lakini hata shule nyingine hilo tatizo limekuwa linaendelea."

Ofisa huyo alisema kwa sasa wananajaribu kuangalia tatizo ni nini na kwamba kuna mambo kadhaa yanajitokeza kwa sababu watoto hao wa shule kuna mambo wanayaiga na kujaribu.

Alisema wengine wanajiingiza katika matukio hayo kutokana na uangalizi mdogo wa wazazi.

Kutokana na ongezeko la matukio ya aina hiyo, Bunge limeshauri serikali kuweka utaratibu wa kuzishauri halmashauri za wilaya, manispaa, majiji na miji kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa uhamasishaji wa namna bora ya kupunguza ukatili huo na hata kujikinga na kutoa taarifa katika vyombo husika ikiwamo polisi.



Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira (katikati), akiwa na viongozi mbalimbali wa kisiasa, wahifadhi na wadau wa utalii, baada ya kuzindua sanamu ya Mlima Kilimanjaro kwenye makutano ya barabara ya Moshi/Arusha juzi. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Maofisa SADC wajadili sekta wanyamapori

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

MAOFISA waandamizi kutoka Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) wanaoshughulikia sekta ya wanyamapori na utalii, wameanza majadiliano ya siku nne na Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori nchini kwa ajili ya kuanzisha mafunzo maalum kwa mameneja na askari wa wanyamapori wa jumuiya hiyo.

Taarifa iliyopatikana jana na kuthibitishwa na Ofisa Uhusiano Mkuu wa Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori (Mweka), Ernest Emmanuel, inaeleza kuwa maofisa hao wa SADC wako katika ziara ya siku nne kuanzia Februari 11 hadi 14 katika Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Inaelezwa kuwa timu hiyo inaongozwa na Ofisa Mwandamizi wa Programu ya Maliasili wa SADC, Deborah Kahatano ambaye amefuatana na Tawanda Gotosa, Mshauri wa Ufundi wa maeneo yaliyohifadhiwa yanayovuka mipaka ya nchi.

"Ni kweli tunao wageni kutoka SADC ambao wamekuja kufanya majadiliano ya kuhusu majukumu ya chuo katika uanzishwaji wa mafunzo kwa mameneja wa uhifadhi na askari wa wanyamapori wa Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika.

"Lakini wamekuja kufanya ufuatiliaji wa kawaida wa chuo kama kituo mahiri (centre of excellence) cha utoaji wa mafunzo ya usimamizi wa wanyamapori na kujadili njia bora za kuimarisha hadhi hiyo."

Chuo hicho kimethibitisha kuwa wataalamu hao wa SADC pamoja na mambo mengine wanalenga kupata ufahamu wa jumla kuhusu shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na chuo hicho cha kimataifa.

Hivi karibuni, Wizara ya Maliasili na Utalii ilikipa jukumu Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka kutoa mafunzo maalum kwa waongoza watalii nchini.

Mafunzo hayo yanalenga kuwawezesha watoa huduma katika sekta ya utalii kupata sifa za kusajiliwa na kupewa leseni ya kuendelea kutoa huduma hiyo kwa mujibu ya Sheria ya Utalii Namba 11 ya Mwaka 2008 kifungu cha 48.



Ukurasa 14

**Uboreshaji daftari uchaguzi Kibaha waanza na msisitizo kwa vijana**

Miaka 30 Mandela kutoka gerezani na yaliyojificha



Ukurasa 17




Ukurasa 18

**Hashim Rungwe afunguka yake kisiasa ndani na nje**


# siasa

JUMATANO FEBRUARI 12, 2020

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe




Ukurasa 20

RAIS UHURU VS MAKAMU RUTO

## Kilichojificha katika historia kuu, hatima kuelekea uchaguzi 2022

UCHAGUZI MKUU 2020:

# Mbinu, uzoefu kukwepa rushwa ngono hizi hapa

• Wazoefu waonyesha njia

**Na Marco Maduhu,** Shinyanga

WANAWAKE waliokuwa wakijihusisha na siasa, wakigombea nafasi mbalimbali za uongozi kwenye uchaguzi mbalimbali, ukiwamo wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu, baadhi yao wanakumbana na changamoto ya ukosefu wa fedha za kuendeshea kampeni kujinadi kwa wapiga kura.

Chanzo kikuu ni ukosefu wa fedha za kuendeshea kampeni kuzunguka kwenye mitaa, kufanya mikutano ya hadhara na kumwaga sera kwa wananchi.

Baadhi yao wamekuwa wakirubunika na watu wenye fedha na kuombwa rushwa ya ngono, ili wapate ufadhili wa kuendeshea kampeni hizo.

Mtandao wa Kijinsia Tanzania (TGNP), ni miongoni mwa wanaharakati ambao wamekuwa


INAENDELEA UK.16




Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana na Ajira), Anthony Mavunde, akizungumza kwenye kongamano la wanawake wajasiriamali (hawapo pichani), mjini Shinyanga. **PICHA ZOTE: MARCO MADUHU**

**Mangula na onyo analolirudia kwa waendekeza rushwa CCM** Ukurasa 15

UBORESHAJI DAFTARI UCHAGUZI

# Kibaha waanza na msisitizo kwa vijana

- Kamishna, Mkurugenzi: Jamani msituangushe
- Mratibu Uchaguzi: Vifaa vina bei, tuvitunze



Wasaidizi wa uandikishaji wapigakura Mkoa wa Pwani, wakiwa katika mafunzo ya pamoja, Kibaha. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Khadija Kalili,** KIBAHA

WAKATI nchi ikiwa katika maandalizi ya kuelekea kwenye Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani nchini kote kunaelezwa kuna haja ya kuwatupia jicho vijana, ambao ndiyo kundi kubwa nchini na duniani kote.

Pia, hata katika mikakati ya kitaifa, hao ndiyo nguvukazi kubwa katika jamii, ambao kimsingi ni idadi kubwa katika jamii wanaopaswa kupewa elimu zaidi ya kuwa na ari ya kwenda kujiandikishwa kwenye daftari la kudumu la kupiga kura, katika mchakato unaoendelea nchini kote.

Wanaonuia kujitosa katika uchaguzi wa sasa, katika kipindi cha uchaguzi uliopita wa mwaka 2015, wengi walikuwa hawajatimiza umri rasmi wa miaka 18, wanaaswa kufanya jitihada za kupata fursa ya kujiandikisha kupiga kura, badaaye mwaka huu.

Kamishna wa Tume ya Uchaguzi, Jaji Mstaafu Mary Harieth Stella Longway, anasisitiza kwamba kundi hilo ni muhimu na jambo linalotakiwa kila mmoja mahali alipo, awasisitize vijana wanaowajua, wajiandikishe kwenye daftari la kudumu la mpiga kura, mahali wanakoishi.

Anasema vijana wajitokeze kujiandikisha, ili wawe miongoni mwa wapiga kura halali siku ya uchaguzi mkuu ujao na anasisitiza nguvu zaidi zielekezwe kutoa hamasa, kundi hilo la vijana lijitokeze kujiandikisha kwenye daftari hilo la mpiga kura mkoani Pwani ambako kazi hiyo inaendelea.

Akizungumza na Nipashe hivi karibuni, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kibaha, Jeniffer Omolo, anatoa hamasa kwa wananchi wa Kibaha na vijana kwa ujumla, wajitokeze kwa wingi kujiandikisha katika daftari la kudumu la mpiga kura kuelekea uchaguzi mkuu ujao.

> "Katika kiapo walichokula, ni pamoja na kujivua itikadi zao za vyama, huku wakitakiwa kuwahudumia wananchi wote kwa usawa.



Kamishna katika Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Mary Longway.

**MKURUGENZI KIBAHA**

Halmashauri ya Mji Kibaha ina kata 73 na vituo 122 vya uandikishaji na Jeniffer anasistiza kwamba, ni vyema wazazi na walezi wanapaswa wakajiandikishe kwenye daftari la kudumu la mpiga kura huku wakiwa na maelezo ya kutosha kuhusu vijana hao wanaojiandikisha kwa mara ya kwanza.

Jennifer ana wito kwa wakazi wote wa Halmashauri ya Mji Kibaha, wajitokeze kwenda kuhakiki taarifa zao, ili waweze kupata haki yao ya msingi ya kushiriki katika uchaguzi mkuu ujao.

"Wale ambao walikuwa hawajatimiza umri wa kupiga kura katika kipindi kilichopita, kuwa sasa ni wakati wao wajitokeze na kujiandikisha kwenye maeneo yao husika nawasihi wafuate maelekezo yote ambayo watapatiwa na wasimamizi wa vituo.

"Tunawahamasisha wananchi ambao walipoteza kadi zao za kupigia kura, nao wasisite kwenda kuhakiki taarifa zao, wakiwa na vithibitisho vyote vitakavyotakiwa na wasimamizi wa vituo, huku maelezo mengine watayapata wakiwa vituoni," anasema Jennifer.

**MRATIBU DAFTARI**

Mratibu Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Mpiga Kura Mkoa wa Pwani, Gerald Mbusoli, anasema wakati nchi ikielekea kwenye uchaguzi mkuu ujao, Mkoa wa Pwani kama ilivyo mingine inafunga milango ya uboreshaji wa daftari hilo la kudumu la mpiga kura.

"Mkoa wa Pwani una changamoto kubwa ya miundombinu, lakini tutahakikisha tunawafikia wananchi wote na wote watajiandikisha, ili kila Mtanzania aweze kushiriki katika kupiga kura kwenye uchaguzi mkuu ujao.

"Tumejipanga vyema kama ilivyokua katika uchaguzi wa serikali za mitaa, ili kuwafikia wananchi wote, licha kuwa mkoa wa Pwani, umegubikwa na changamoto nyingi... ikiwamo baadhi ya wilaya na maeneo ya delta (mkondo wa bahari) kama vile Mafia na Rufiji, lakini tunaahidi tunawafikia," anaeleza.

Mbusoli anaeleza kwamba, tayari mafunzo yameshatolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa maofisa mbalimbali kutoka kwenye halmashauri zote za mkoa wa Pwani, wakiwamo wataalamu wa teknolojia ya habari na mawasiliano.

"Hawa ni maofisa walioteuliwa kutokana na uzoefu wao, ambao tunashirikiana na halmashauri zote, kwani hii ni taasisi ambayo tume tuna utaratibu wa kuitumia miaka yote, huku washiriki hao wakila kiapo cha kutunza siri za taarifa mbalimbali za wananchi, ambao watafika kwenye vituo mbalimbali nchini kote," anasema Mbusoli.

Pia, anawatoa hofu wananchi kwa kuwahakikishia kwamba taarifa zao zote watakazozitoa, zitabaki kuwa siri, kwani maofisa hao wamekula kiapo na endapo wataenda kinyume na kiapo, basi kuna taratibu zitakazofuatwa kisheria.

"Katika kiapo walichokula, ni pamoja na kujivua itikadi zao za vyama, huku wakitakiwa kuwahudumia wananchi wote kwa usawa. Hilo (uboreshaji daftari) umepangwa kuanza Februari 14(keshokutwa) hadi 20 mwaka huu, "anasema Mbusoli.

Waliopatiwa mafunzo ni katika ngazi ya mkoa na watakuwa na wajibu wa kwenda kusambaza elimu hiyo, kwa waandikishaji wa ngazi za kata, kuthamini vifaa muhimu vya kazi, kama mashine za kompyuta na viti, vyote vikiwa ni vya thamani kubwa.

Maofisa waliohudhuria mafunzo ni kutoka katika Halmashauri za Mkuranga, Bagamoyo, Mji Kibaha, Kisarawe, Kibiti, Mafia, na Rufiji na maeneo mahsusi ya mafunzo yao yanagusa utumiaji wa mashine za kielektroniki za 'BVR Kits' na stadi za kukabili changamoto zinazojitokeza katika kazi zao.

Mbusoli anahitimisha kwa kutoa rai ya kuwataka watumie vifaa vya 'BVR Kits' kwa makini, kwani vimenunuliwa kwa gharama kubwa sanjari na kuzingatia maelekezo yote yatakayotolea na Tume, huku serikali ikiwahakikishia kuwa kazi hiyo itaendeshwa kwa weledi mikubwa.

# Mangula na onyo analolirudia kwa waendekeza rushwa CCM



Mwenyekiti wa CCM, Dk. John Magufuli, alipoagana na Makamu Mwenyekiti (Bara), Philip Mangula na kulia ni Katibu Mkuu, Dk. Bashiru Ally, baada ya kuongoza kikao katika Ofisi Ndogo za CCM, Mtaa Lumumba, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Sabato Kasika**

WIKi moja kamili iliyopita, Chama Cha Mapinduzi (CCM), kilitimiza miaka 43 tangu kilipozaliwa, baada ya kuungaishwa vyama vya TANU na Afro-Shirazi.

Kabla ya kilele hicho, kulifanyika kongamano katika maeneo mbalimbali nchini, yaliyoelezea historia yake kwa kina.

Mengine katika mjadala huo, Makamu wa Mwenyekiti (Bara), Philip Mangula, aliwaonya makada wao wenye nia ya kuwania uongozi katika uchaguzi mkuu ujao, kwamba wajiepushe na rushwa ya hadaa za aina yoyote, katika kipindi kilichopo kuelekea katika uchaguzi mkuu.

Anasema, wanaojiandaa kujitosa katika kampeni za kabla ya wakati ya nyendo za rushwa, watakapobainika wataondolewa majina yao haraka kabla hata ya kufikishwa katika kura za maoni ndani ndani ya chama.

Ni onyo ambalo Mangula, analitoa kwenye kongamano jijini Dodoma, ikiwa si mara ya kwanza kuitoa kauli hiyo na ufafanuzi wake, akinena kuna baadhi ya maeneo makada wametuma wakala wao kuwapigia debe kwa kificho.

Mangula anasema CCM inataka uchaguzi na siyo anachokiita 'uchafuzi,' hivyo haitakubali makada wake wafanye vilivyo nje ya kanuni, akiwaonya kwamba endapo wataendekeza nyendo hizo hata kimya kimya, hawataachiwa.

"Kuna maeneo mengine watu wametuma mawakala kwenye majimbo ya wenzao, wanatembelea matawi, kata, jimbo na wilaya au nchi nzima kushawishi wanachama kwa michango, tafrija na misaada ili wapigiwe kura," anadokeza Mangula.

**ONYO LAKE**

Mangula anaonya kwamba, wakibainika 'watafyekwa' na kufafanua mbali na kuwa hatua ya kukabili rushwa, wafahamu kuna kanuni za uongozi na maadili zinazoelekeza kwamba "uchaguzi kiongozi yeyote atakayethibitika, ameshinda kutokana na kitendo chochote cha rushwa, anatakanyang'anywa ushindi wake."

Mangula anaendelea: "CCM inataka uchaguzi siyo uchafuzi, hivi sasa nafasi bado zina wenyewe, rais bado ni rais, wabunge na madiwani bado wapo. Ukionekana unajipitisha pitisha huko, unanusanusa huko, jua hilo ni kosa la kimaadili."

> Viongozi wa kuchaguliwa wa ngazi zote wanaruhusiwa kutafuta na kutoa michango na misaada, isipokuwa tu kipindi cha uchaguzi.

**KATIBA CCM**

Kiongozi huyo anasema, katiba ya CCM inaweka wazi kuwa kada anayekiuka hayo aliyoelekeza, atazuiwa kugombea uchaguzi mwingine wowote kama itakavyoamriwa na Halmashauri Kuu ya Taifa ya chama hicho.

"Sasa mfumo umebadilishwa kwa kupitia kikao cha chama kilichokaa Mwanza na kukubaliana kuwa kila watu 10 wanaoingia jimboni, wanachukua fomu na kuzunguka kata mbalimbali, hao ndiyo wanaochochea rushwa na kugawanyika katika makundi au kupata kura kwa njia haramu, hivyo wataondolewa," anasema.

Makamu Mwenyekiti, anarudia kwa kutaja yanayozuiliwa kuwa ni kutoa michango, misaada na vingine vyenye lengo la kushawishi na kwamba mwanachama kama anataka kutoa msaada, basi ni hadi kamati ya siasa iridhie.

"Viongozi wa kuchaguliwa wa ngazi zote wanaruhusiwa kutafuta na kutoa michango na misaada, isipokuwa tu kipindi cha uchaguzi," Mangula anasema na kuongeza:

"Pia, wabunge na madiwani wanaruhusiwa kuendelea kuchangia miradi mbalimbali ya maendelea kwenye maeneo yao."

Mwanasiasa huyo mkongwe anaendelea: "Lakini mtu mwingine utoke na kiherehere uende kule! Bahati nzuri mwaka huu tunawakata kabla hamjaenda kuzunguka kwa wananchi."



Philip Mangula

**MANGULA HATANII**

Mangula amekuwa akirudia kauli yake, hali inaoonyesha umakini wake kupitia kauli hiyo aliyozitoa ziarani katika mikoa ya Simiyu na Njombe, katika vikao akisisitiza umuhimu wa kila kada wa CCM kufuata kanuni na kuzingatia maadili.

Mangula ameshatamka kwamba wapo baadhi ya makada wanaojisahau wakisimamia itikadi fedha wanazotanguliza kwa wapigakura, ndizo maarufu na siyo wao.

"Hivyo wasijidanganye, bali wafuate taratibu na kanuni na katiba ya chama ili kupata uongozi, kuliko kwenda kinyume na kujikuta wakikwama mapema," anasema.

"Hakuna mtoa rushwa atakayepona, katika hili kwa sababu tunaendelea kurudisha heshima ya chama chetu, ambayo miaka ya nyuma ilipotea kwa sababu ya wala rushwa wachache," anasema.

Aidha, anawataka wanachama wenzake kuacha kununuliwa kwa kupewa chochote na watu wanaotaka kuwania uongozi kwa vile rushwa ni aibu na kuwataka wafuate maadili ya chama hicho.

**UCHAGUZI MKUU**

Hadi sasa tayari vyama vya siasa vimeanza mchakato wa kupata wanachama, watakaopeperusha bendera zao, katika uchaguzi huo utakaofanyika mwishoni mwa Oktoba.

Miongoni mwake ni Chama cha Demoktasia na Maendeleo (Chadema), kinachowataka wanachama wake kuwania uongozi, kuandika barua za kuonyesha nia hiyo.

Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika, katika maelekezo yake, anasema kwamba kuteua wagombea ni sehemu ya uchaguzi na kwamba mchakato huo ni muhimu kwa ajili ya kupata wagombea bora wa kuwakilisha chama .

JUMATANO FEBRUARI 12, 2020



# Mbinu, uzoefu kukwepa rushwa ngono hizi hapa

INATOKA UK.13



Wanawake kutoka maeneo tofauti katika Mkoa wa Shinyanga, wakijadili changamoto za kupata nafasi za uongozi katika uchaguzi mkuu ujao. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

mstari wa mbele wakipinga kuwapo rushwa ya ngono kwa wanasiasa wanawake, jambo linalowashushia utu wao na kudiriki hata kufanya mikutano na kongamano ya kupinga vitendo hivyo.

Katika hilo wanaendesha mafunzo na elimu za njia tofauti kuwaimarisha kinamama walioko kote nchini.

**NAIBU WAZIRI**

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia Kazi, Vjana na Ajira, Anthony Mavunde, akiwa mkoani hapa anatoa wito kwa wanawake wajiunge kwenye vikundi ili wanufaike na mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ambayo yanasimamiwa na serikali.

Anasema kuna fursa nyingi sana na serikalini inawawezesha wanawake kuinuka kiuchumi, ukiwamo Mfuko wa Maendeleo ya Jamii kwenye fedha za mikopo bila riba.

Mavunde anasema, ni fedha zinazotolewa na halmashauri kupitia mapato ya ndani na anawataka wanawake wajiunge kwenye vikundi wazopate fedha hizo na kuanzisha biashara za kuingizia kipato.

Mtandao wa Kijinsia Tanzania (TGNP), ni miongoni mwa wanaharakati wanaopinga kuwapo rushwa ya ngono kwa wanasiasa wanawake, jambo linalowashushia utu wao na kudiriki hata kufanya mikutano na kongamano ya kupinga vitendo hivyo.

**WENYEWE WANENA**

Mwenyekiti wa chama cha Act Wazalendo mkoani Shinyanga, Siri Yasini, anawaambia kinamama wenzake kwamba, mwanasiasa yeyote mwanamke asiye na biashara ya kumuingizia kipato, ni lazima atakumbana na changamoto nyingi, ikiwamo kuombwa rushwa ya ngono.

"Huwa nafanya shughuli ya kuuza nguo pamoja na nafaka, biashara ambazo zinaniingizia kipato bila ya kutegemea ufadhili wa mtu yeyote na kufanikiwa kuepuka vishawishi vya rushwa ya ngono.

"Kwenye Uchaguzi Mkuu wa Mwaka huu (2020) tayari nimeshajipanga vyema kifedha, nagombea ubunge katika Jimbo la Shinyanga Mjini na sitategemea fedha ya mfadhili yeyote na mwanamume ili akupe fedha yake lazima kuwapo na 'element' (nyendo zake) kutaka kufanya naye ngono kwanza ndipo akupe hela yake," anaongeza.

Ni hoja inayodakwa na Zuhura Waziri, diwani wa vitimaalum katika Manispaa ya Shinyanga, anayesema ili mtu awe mwanasiasa mzuri, ni lazima awe na kazi itayomuingizia kipato, akifafanua hoja yake kwamba, inatokana na ukweli, siasa ni zao la utoaji huduma.

"Mwanasiasa ambaye ana shughuli yake pembeni ya kumuingiza kipato, huyo lazima atafanikiwa, kwa sababu ataweza kumudu kampeni zake na kuzifanya vizuri kwa kuzuguka maeneo yote kuomba ridhaa kwa wananchi, ili wamchague, lakini yule ambaye hana shughuli hawezi kufanikiwa lazima atumie mbinu mbadala," anasema Zuhura.

> Ni fedha zinazotolewa na halmashauri kupitia mapato ya ndani na anawataka wanawake wajiunge kwenye vikundi wazipate fedha hizo.

"Mimi nimeingia kwenye siasa mwaka 2015 na kufanikiwa kuwa diwani wa viti maalum na wakati napiga kampeni ndani ya chama changu kuomba ridhaa ya kuchaguliwa kuwa diwani, niliona kazi yake, kwa kweli bila ya kuwa na fedha huwezi kufanikiwa,

"Baada ya kushinda tu kuwa diwani wa viti maalum, ikanibidi nifungue duka la kuuza vitu mbalimbali, pamoja na kuwa wakala wa taasisi za kifedha na sasa ndio kazi ambayo inaniingizia kipato na ninatekeleza vizuri ilani yangu," anaeleza.

Wito wake kwa wanasiasa wanawake wasio na shughuli za kuwaingizia kipato, wabadilike kwa kujishughulisha na biashara mbalimbali za kuwaingiza kipato, wafanikiwe kwenye uongozi na kumudu harakati za kampeni, wakiwa huru

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kitangili, katika Manispaa ya Shinyanga, Habiba Ramadhani, anafafanua changamoto wanazokutana nazo kinamama wakati wa kampeni ni kujinadi kwa wananchi kupitia mikutano ya hadhara, wanakwazwa sana na kipato.

Anasema, hiyo humfanya mwanamke kuna hatua anajikuta kuingia katika mitego ya kuombwa rushwa ya ngono, ili afandhiliwe, akifafanua kwamba bila ya fedha ni vigumu kukubalika kwa wananchi. Anafafanua:

"Unapopitishwa na chama chako kuwa mgombea wa kiti fulani, lazima na wewe sasa ujipage kifedha, ili kuendesha kampeni za kuzungukia wananchi kupitia mikutano ya hadhara kuuza sera zako, ili wazikubali na kukuchagua na usipofanya hivyo, utaonekana umewadharau wananchi na hawataweza kukuchagua," anasema Habiba.

"Kuendesha kampeni kuna vitu ambavyo vinahitajika na lazima uingie gharama, mfano kukodi gari la matangazo, muziki kwenye eneo la mkutano, nauli za wajumbe kuja kukuunga mkono na kama huna shughuli ya kukuingia kipato fedha, hizo utazitoa wapi?" anahoji.

Habiba anaendelea kwa kutoa angalizo: "Ni lazima tu utaingia kwenye vishawishi vya rushwa ya ngono ili upate ufadhili."

Anarejea darasa la uzoefu ea nafsi yake, kwamba amekuwa akiepuka vishawishi vya rushwa ya ngono, akiegemea mbadala wa shughuli zake za ujasiriamali wa bidhaa ya nguo.

Kwa mujibu wa habiba, mtindo wake mkuu ni kwamba, amekuwa akitenga fedha za maandalizi ya kampeni, sasa akiwa katika awamu ya pili uongozi wa mtaa.




Diwani katika Manispaa ya Shinyanga, Zuhura Waziri, akiwa dukani mwake, kunakomuwezesha kiuchumi, kumudu hata nyendo za kisiasa.

**ILIVYO RUSHWA**

Sara Njabuyaga, ni mwanasiasa mwanamke wa Shinyanga anayedai kuwahi kukutana na madhila ya kuombwa rushwa ya ngono kwenye uchaguzi mkuu uliopita mwaka (2015), alipogombea nafasi ya udiwani.

Anakumbuka yeye na wifi yake (dada wa mumewe) walijitosa kuwania nafasi hiyo, wakimtegemea mfadhili mmoja ambaye ni mume wake na hali halisi ya kibajeti kuwa chini, akakwama njiani.

"Mwanasiasa mwanamke kwa kweli kama huna biashara ya kukuingizia kipato na kutegemea mtu mwingine akupatie fedha, ni sawa na kucheza bahati nasibu, akikunyima tu fedha za kuendesha kampeni, tayari unakwama na kupoteza nafasi ya uongozi kwa sababu hutaweza kujinadi kwa wapiga kura.

"Baada ya mimi kukosa fedha za kuendesha kampeni, kuna baadhi ya wanaume walinifuata na kuniomba rushwa ya ngono, wakinishawishi kuwa watanipatie fedha za kampeni pamoja na kuhakikisha nashinda udiwani wa vitimaalumu, lakini niligoma... hatimaye nikashindwa kuwa diwani," anasimulia mkasa.

**ULIKO MTAJI**

Theogonius Ligonja, Mkuu wa Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Shinyanga, anayetaja majhali kinamama hasa wa Shinyanga kuibuka, ni mkopo wa kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii wa kuwezesha wanawake, vijana na walemavu na katiajm mkoa Shinyanga, katika mwaka wa fedha uliipita (2018/19) ilitolewa Sh. milioni 166.1.

Ligonja anasema walizitoa katika vikundi 21; kikundi cha wanawake kilipata Sh. milioni 93; vijana vikundi vilipata Sh. milioni saba; walemavu vikundi viwili vilikopeshwa Sh. milioni 3.9.

> Ni lazima tu utaingia kwenye vishawishi vya rushwa ya ngono ili upate ufadhili.

Anasema katika mwaka wa fedha uliopo sasa, zimetolewa Sh. milioni 20 kwa vikundi saba, kati yake wanawake vikundi vinne vimepata Sh. milioni 13; vikundi vitatu vya walemavu walipata, sh. milioni saba na vijana safari hii hawakuomba.

Pia, Ofisa Ustawi Jamii huyo, anaongeza kuwa hivi karibuni wanatarajia kutoa tena fedha za mikopo Sh. milioni 136 kwa vikundi 20 vikiwamo vya vijana, walemavu na wanawake, ambao wanasubiri taratibu zikamilike, akitoa wito kwa wanasiasa wanawake wasiogope kujiunga kwenye vikundi, kwa ajili ya kunufaika na kuinuka kiuchumi.

## Miaka 30 Mandela kutoka gerezani na yaliyojificha



Marehemu Nelson Mandela. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Mwandishi Wetu**

JANA ilikuwa siku ya kumbukumbu ya miaka 30 tangu Rais wa Afrika Kusini, Nelson Mandela, alipoachiwa kutoka gerezani wakati wa ubaguzi wa rangi nchini kwake. Ni siku inayotumika kumuenzi na kutambua mafanikio yake.

Mandela, aliyefariki mwaka 2013 akiwa na umri wa miaka 95, alikuwa kiongozi wa kwanza mweusi nchini Afrika Kusini, baada ya kutumikia kifungo cha miaka 27 gerezani. Anakumbukwa kuwa mmoja wa viongozi bora aliyewahi kushuhudiwa duniani.

Umoja wa Mataifa unasema:"Kila mtu ana uwezo na jukumu la kuibadili dunia kuwa bora. Siku ya Mandela ni fursa kwa kila mtu kuchukua hatua na kuhimiza mabadiliko."

Kwanini umuhimu wa Mandela? Alipokuwa kijana, watu weupe na watu weusi walikuwa hawaishi pamoja chini ya mfumo wa ubaguzi wa rangi. Weupe walikuwa ni idadi ndogo ya raia walioidhibiti nchi.

Ilikuwa marufuku kwa weusi kwenda shule, hospitali na hata maeneo ya 'kubarizi' kama katika fukwe za bahari sawa na watu weupe. Kimyume chake, hali ilikuwa imeimarika zaidi katika shule na hospitali za watu weupe.

Weusi pia walinyimwa haki za msingi, kama vile kushiriki katika uchaguzi mkuu. Katika mtazamo huo, Nelson Mandela aliamini kwamba kila mtu anastahili kuchukuliwa kwa usawa.

Mandela alijiunga na chama cha kisiasa cha African National Congress (ANC) na baadaye kuidhinisha tawi la vijana la chama hicho. Aliongoza maandamano kupinga utawala wa ubaguzi wa rangi.

Mara nyingine nyingine kulizuka ghasia, katika maandamano mwaka 1964 na Mandela alihukumiwa kifungo cha maisha gerezani, alikohifadhiwa katika kisiwa cha Robben.

Wakati Mandela akiwa gerezani, picha zake zilipigwa marufuku na ilikuwa ni kinyume cha sheria kumnukuu hadharani.

Hiyo iliamsha hamasa kubwa, watu wengi duniani walifanya kampeni kutaka aachiliwe, kwa namna ya kipekee nchi ya Tanzania, chini ya Rais Juluis Nyerere, ina mchango wake katika msukumo huo.

Nyimbo ziliimbwa na matamasha makubwa yaliandaliwa katika kulalamikia kufungwa kwake.

Hatimaye mafanikio yalifikiwa mwaka 1990, Rais wa Afrika Kusini, Frederick de Klerk aliidhinisha aachiwe huru, tukio lililopokewa kwa sherehe kubwa.

Utawala wa ubaguzi wa rangi ulifutiwa mwaka 1991 na miaka mitatu baadaye, Afrika Kusini, iliandaa uchaguzi wa kwanza mkuu, ambao watu weusi waliruhusiwa kupiga kura sawa na weupe.

Rais Mandela, alichaguliwa kuwa Rais, akianza kuleta umoja baina ya watu wa rangi tofauti.

Mnamo mwaka 1993, alipewa tuzo ya Nobel ya Amani - ya kiwango cha juu ya aina yake, kwa jitihada zake. **BBC**

# HASHIM RUNGWE AFUNGUKA YAKE KISIASA NDANI NA NJE

• Aamini chama chake imara, umoja katika uchaguzi mkuu



Hashim Rungwe, Rais wa Chaumma, katika picha tofauti ofisini na nyendo zake za kisiasa. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Enock Charles**

***JINA Hashim Rungwe ni maarufu katika siasa za nchini, alikojikita katika kambi upinzani, ingawa chama chake cha Chaumma, hakijawahi kushika kupata nafasi ya kuwa na mbunge. Uchaguzi Mkuu kitaifa uko njiani, Amejiandaaje na maoni aliyo nayo? Mwandishi wa Nipashe alimtafuta na yafuatayo ni mazungumzo yao ya Ana kwa Ana. Fuatiliia:***

**Swali: Rais ameahidi kuwa mwaka huu uchaguzi utakuwa huru na haki. Je, wewe kama mmojawapo wa viongozi kutoka upinzani, unasemaje?**

**Jibu:** Sisi tunategemea kama angefanya yale mambo ambayo ni muhimu kuanzia sasa, angeondoa lile zuio kwanza la mikutano ya kisiasa...

**Swali: Wewe mtazamo wako ungependa mgombea mmoja au kila chama na mgombea wake?**

**Jibu:** Mimi nasema hivi, kuwa umoja ni nguvu si ndio wanasema waswahili? Kwa hio tuache hivyo.

**Swali: Unafikiri nini kifanyike ili kuing'oa CCM madarakani?**

**Jibu:** Wananchi wapate haki ya kuchagua, wananchi wenyewe ndio wenye mamlaka, wananchi ndio msingi wa mamlaka yote ya nchi hii na sisi tunawaambia wananchi kuwa, wao ndio msingi wa mamlaka wasikubali kunyang'anywa haki yao.

Unajua huko nyuma, kina (mwanafalsafa) Plato kina Aristotle, Warumi wenyewe walishapita huko walishaona kuwa hivi haifai kuendesha 'ki -monarchism' (sura ya kifalme) waliona tufuate utaratibu unaofaa na tangu wakati huo, silaha zilinyamaza wananchi wakawa ndio wanaamua kiongozi.

> Hata wakati ule nilikuwa NCCR, chama kikanipa nafasi na hata nikipewa utayari wa kugombea au kutogombea, utategemea na afya yangu wakati huo, nikiwa na afya njema na sina vipingamizi, mimi sina matatizo.




Haya yanayotokea huko Angola, ni baadhi tu ya mifano tu za kuonyesha ala, kumbe hawa wanasema kweli akishinda CCM na aendelee CCM, atashinda chama kingine kiendelee, kama utashinda umoja wa vyama viendelee.

Ili wananchi waseme basi wewe tunakupa na tukishakupa tunakuangalia kwamba sasa mbona unafanya hivi? Si umesikia huko Liberia wamemgeukia Rais wao? Wao si ndio walipigana, sisi tunamtaka huyu. Si waliachiliwa wakachagua kwamba tunamtaka huyu kwa kura, wakachagua wenyewe wananchi sasa hivi wanasemaje?

Eeeh wananchi wanaona maana yake ni watu wenye kuona kwamba, ala huyu bwana mbona hivi na mwananchi hana urafiki na mtu kama utampa uhuru.

**Swali: Chama cha Umma kwa sasa kina wanachama wangapi?**

**Jibu:** Sisi tuna wanachama wengi, kule kuandikishwa tu unatakiwa uwe na wanachama 2000, kwa hiyo sasa hawa wengine wanaozidi ni more than (ni zaidi ya) 5000, 6000 wapo tu, lakini hiyo sio 'issue' (jambo).

Kwa sababu hapa tunazungumzia uchaguzi mkuu na uchaguzi mkuu, watu hawachaguliwi kwa sababu ya chama, wanaweza kupiga kura kinyume na chama maana sisi tunasimamisha mgombea na ndiye anayebeba kofia ya chama. Mtu anaweza akaona mimi sim-

# HASHIM RUNGWE AFUNGUKA YAKE KISIASA NDANI NA NJE

pendi huyu, akapiga kura chama kingine, si ipo hiyo? utajuaje?

**Swali: Mmejipanga vipi na mnategemea kufanikiwa kwa kiasi gani?**

**Jibu:** Kufanikiwa au kutofanikiwa, kunategemea nafasi ya mgombea urais, tuchukue mfano wa Congo (DRC), yule aliyekuwa akitawala ametawala miaka pale zaidi ya miaka mitano sita kumi na zaidi Bwana Kabila na tumeona kwenye uchaguzi kilichotokea.

Wananchi hawataki, wamechagua mtu mwingine na yeye (Rais Kabila) alichagua mtu wake. Wewe unajua alimchagua wa chama chake akawekwa pale, lakini wananchi wakasema, huyu hatufai si basi? Kama hawafai sasa wewe utafanyaje? ila uchaguzi uwe 'free' (huru) na wananchi wawe na roho ya kuamua .

Unaona wananchi sasa hivi Kongo hawakufanya fujo. Kuna fujo? Hakuna fujo. Wananchi wakasema sisi huyu hatufai tunamtaka (Rais Felix) Tshisekedi sasa akaonekana kwamba, yeye kura zake hazikutimia sio wakafanya fanya maarifa wakaunganisha na kura, ikawa serikali imepatikana.

Kwa hiyo, sisi sasa hivi tunasema wananchi wawe na uhuru ikitokea kuna mkutano wa Chauma waje wanaotaka, kwani kuna mtu amelazimishwa? Mimi nitahutubia kwa kiasi nitakachoweza, kama ni wa Chadema waachie uhuru waende zao Jangwani au hata kama ni wapi waende wakasikilize......

**Swali: Ikitokea chama chako kikakupa nafasi utakuwa tayari kugombea tena mwaka huu?**

**Jibu:** Kugombea nafasi siwezi kusema mimi, watasema wanachama. Hata wakati ule nilikuwa NCCR, chama kikanipa nafasi na hata nikipewa tayari wa kugombea au kutogombea, utategemea na afya yangu wakati huo, nikiwa na afya njema na sina vipingamizi, mimi sina matatizo.

**Swali: Ikiwa vyama vya upinzani mtaamua kushirikiana, ni yupi katika upinzani unayeona anafaa kugombea nafasi ya urais?**

**Jibu:** Aaah! Mimi siwezi kumjua sasa hivi inategemea tu.

**Swali: Kuna madai yanayokaririwa kwamba, kuna vyama vipo kwa ajili ya ruzuku tu na wala havina nia ya dhati ya kushika dola, je unaielezaje hilo?**

**Jibu:** Kila chama kikiingia ni haki yake kupata ruzuku, sasa unataka apate nani? Kama imewekwa ruzuku na serikali, huyo mtu anapata hela za nchi yake.... silaumu kuwa iko hivyo, ni haki yake wamepewa wale wanao haki ya kupata na wengine pia wana haki hiyohiyo.

Sasa ruzuku sio suala la kuzungumzia, kwamba hiki chama kimekaa kwa sababu ya ruzuku wewe kwani hupati ruzuku? Sheria tulizo nazo zinataka uingie bungeni kwanza, sasa bungeni hatujaingia sasa mimi nitadai ruzuku?

**Swali: Wewe ni mwanasiasa, pia ni mfanyabiashara. Je, unawezaje kutenganisha biashara na shughuli za kisiasa?**



Hashim Rungwe, Rais wa Chaumma, katika mikutano ya kisiasa. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> Ni jambo la kusikitisha, nataka vile vyombo vifanye uamuzi wa haraka, hasa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, iwe na haraka ya kuendesha kesi, waondoke hao watu.



**Jibu:** Hiyo inawezekana. Hata hivi sasa, nimetenganisha mimi nafanya zangu shughuli zangu na muda unapofika wa siasa, nafanya shughuli za siasa na nilishakubali kwamba, mimi naingia katika siasa na nitafanya biashara zangu.

Kwa hiyo, mambo ya siasa na mambo ya biashara ni tofauti, lazima kuwapo mgawanyo. Kuna marais wangapi dunia hii wana biashara zao na wanaingia, mfano mzuri ni Marekani tu. Ukishakuwa mfanyabiashara unakuwa mzuri tu sio mwizi wala nini.

**Swali: Ni kipi unachoweza kusema ni kizuri kilichofanywa na serikali hii?**

**Jibu:** Yaani mimi unaniuliza maswali magumu, sana lakini mepesi tu kwa wewe ukishakuwa baba ndani ya nyumba, unatarajia kufanya kitu kizuri sana kitu gani ? Unahudumia tu, kama unaweza kumpa mtoto gari unampa na wala hupigi 'vikofi' 'because you're supposed to do that' (kwa sababu unapaswa kufanya hivyo) na wale unaotakiwa uwafanyie wala wala hawakuomba.

**Swali: Ukipata fursa ya kukutana na Rais ni jambo gani unaloweza kumwambia?**

**Jibu:** Aah! Nitakuwa nalo wakati huo, sitakosa la kumwambia.

**Swali: Wewe ni wakili, Je, kwa nafasi yako umewasaidiaje wananchi au hata viongozi wenzako wa upinzani wanaokumbwa na kesi mbalimbali?**

**Jibu:** Kwanza mimi nilikuwa naomba mashauri yao yapelekwe haraka sana, watu kwenda sana mahakamani. Ni jambo la kusikitisha, nataka vile vyombo vifanye uamuzi wa haraka, hasa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, iwe na haraka ya kuendesha kesi, waondoke hao watu.

Kwa sababu, kuna mtu amedai hivi unajua 'trial' (mashitaka) yaani ni kwamba, kuna mtu anadai hivi, lakini anayedai hivi kwa sababu ya upande huu mmoja tu, maana yake kuna mtu anayedai...kwa huyu anadai upande huu tu, huyu mtu akiamua kwamba huyu ni basi, basi inakuwa ni basi. Tumeona mfano mzuri hapa, hivi karibuni Rais alikwenda Mwanza kwenye gereza, akasema huyu atoke, huyu atoke na watu walitoka si ndio?


**Swali: Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 mpaka sasa, wapo viongozi wengi wa upinzani waliohamia chama tawala, Je hamuoni hili linawakatisha tamaa wananchi kuendelea kuamini upinzani?**

**Jibu:** Unajua kwenye demokrasia hiyo ni haki ya mtu, wale wana haki na wananchi wana haki ya kulalamika kwamba huyu mtu mbona tumemchagua, halafu tena kitu kilekile anakwenda kukiomba huko maana uanakwenda kuomba ubunge wakati ubunge ulikuwa nao na kama ulikuwa utaka 'ku-challenge' ungefanya hivyo ukiwa kule.

Kuna vitu vingi vinavyochangia watu wahame kama vile kukata tama na upande fulani na watu kuwa na hofu na wanahamia sehemu ambavyo kuna mamlaka na hayo yanacheza jinsi anavyotaka yeye na akishahamia huko hawezi 'ku- challenge' au kulalamika tena maana kule kupo shwari tu kule ni kuzuri, kule hakuna tabu yoyote sasa kama mtu hapendi tabu anaenda huko, lakini sisi tunaona ni yale yale tu.

RAIS UHURU VS MAKAMU RUTO

# Kilichojificha katika historia kuu, hatima kuelekea uchaguzi 2022



Rais Uhuru Kenyatta (kushoto), akiwa na Makamu wake, William Ruto. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Ani Jozeni**

***JUMATANO iliyopita, ilikuwa sehemu uya kwanza ya makala hii kujadili siasa za Kenya, chimbuko lake na nini kimejificha nyuma ya pazia kati ya Rais Uhuru Kenyatta na Makamu, William Ruto. Endelea:***

SIASA za Kenya za leo ni Makamu wa Rais wa Kenya, William Ruto, yuko katika malumbano yasiyoisha na Rais Uhuru Kenyatta, aliyeunda umoja wa kisiasa na kiongozi wa upinzani Raila Odinga, kuielekeza Kenya katika hatua nyingine ya mabadiliko ya kikatiba.

Ni mpango unaowagawa wabunge waliounga mkono tiketi ya Uhuru na Ruto uchaguzi mkuu uliopita, nwaka 2017.


Kwa mpangilio wa kawaida wa kisiasa nchini humo, Uhuru alitakiwa aendelee na Ruto kama Naibu wake, halafu Ruto atafute mgombea mwenza mwingine.

Sasa wafuasi wa Ruto wanaona 'inatosha' kidemokrasia, inaanza kuleta mgawanyiko katika maeneo mawili.

Kwanza, picha ya mgombea kutoka Ukanda wa Kati na mwenza wa Bonde la Ufa, wanabadilishana. Halafu ina maana kuwa, maeneo ya ziada wanaweza kushinda tu kama upinzani, hali ambayo si rahisi.

Kielelezo kuwa mpangilio huo umefikia mahali haukidhi mahitaji halisi ya maeneo mengine kujihisi kuwa wao, ni sehemu mahsusi ya nchi ni mzozo wa hitilafu ya matokeo ya uchaguzi mkuu uliopita, 2017 ambako ilifikia mahali kuna

> “Ruto alikuwa kiongozi wa Umoja wa Vijana wa KANU wakati huo, yaani bingwa wa siasa za kutunisha misuli, ambazo alizitumia kuwa upande wa Odinga wakati wa machafuko ya 2007.



mpasuko wa wazi.

Upinzani ulianza kuwataka wapiga kura wake kususia bidhaa zinazotoka kampuni ya Rais Kenyatta na washirika wake na baadhi ya makada wa ODM (chama cha Raila) walikamatwa.

Siasa za Kenya zimegubikwa na sintofahamu katika maeneo kadhaa, mojawapo ikiwa ni uwezekano wa kusambaratika umoja wa kisiasa uliomfikisha Uhuru na Ruto madarakani, usiweze kutumika tena kwenye uchaguzi ea mwaka 2022.

Upande mwingine, ni uhaba wa utii katika kundi la Raila, kwani washirika wake wanamwangalia kwa 'jicho kali' kama anataka agombee tena au anaadaa tu mazingira mazuri ya kupata mgombea ambaye atokea upinzani (wa sasa) ahakikishiwe nafasi kushinda. Si kazi rahisi.

Mkakati wa hivi sasa wa Ruto, ni kupambana na mpango wa mabadiliko kutaka mgombea anayepewa nafasi kubwa ya kushinda atoke maeneo mengine ya nchi na siyo ukanda wa Kati au Bonde la Ufa pekee.

Kwa vile Uhuru au Raila hawawezi kufika bungeni na muswada kama huo, kinachosukumwa sasa ni kubadilisha katiba kuhusu jinsi ya kupata mgombea, ili iwezekane kwa Rais Kenyatta kushiriki uchaguzi siyo kama mgombea wa urais.

Kuna uwezekano wa kuundwa nafasi ya waziri mkuu yenye nguvu, hali ambayo ilijitokeza katika muhula wa pili wa awamu ya tatu, ila si kwa ufanisi.

Wakati huo, katika kipindi cha pili cha Rais Mwai Kibaki, ambako machafuko makubwa yalifuata uchaguzi wa rais mwisho wa mwaka 2007, Raila alikuwa Waziri Mkuu kama kiongozi wa upinzani, na Kalonzo Musyoka (sasa mshirika wa Raila, kwa taabu kiasi fulani) akiwa Makamu wa Rais na mshindani wake kiserikali au kiprotokali.

Kuna jitihada ya kuwa na Waziri Mkuu Mtendaji anayechaguliwa na Bunge, wakati kura zinapigwa kumpata rais, hali inakinzana na katiba; labda wachague tu wabunge bila ya wagombea urais, halafu kiongozi wa chama kinachoshinda anakuwa Waziri Mkuu kama ilivyo nchi nyingi za Ulaya.

Katika mazingira hayo, ni sharti Rais hapo anachaguliwa na Bunge.

**MZIZI WA RUTO**

Uhusiano wa Ruto na hayati Mzee Daniel Moi, aliyezikwa jana, ulifikia kilele mwaka 1992, wakati marehemu Moi alipoitisha uchaguzi mkuu, baada ya kukubali siasa za vyama vingi (kutokana na mzozo na Marekani na nchi za Umoja wa Ulaya).

Ruto alikuwa kiongozi wa Umoja wa Vijana wa KANU wakati huo, yaani bingwa wa siasa za kutunisha misuli, ambazo alizitumia kuwa upande wa Odinga wakati wa machafuko ya 2007.

Kwa ile alishtakiwa yeye na Uhuru (akiongoza kampeni ya Kibaki upande wa chama tawala) wakafikia makubaliano kuwa wagombea wa pamoja, kujihalalisha kwa wananchi kuwa hapatakuwa na fujo tena.

Mzee Moi alikuwa anaonyesha kuafikiana na kundi la Uhuru na Raila, kwani baba yake Raila, Marehemu Mzee Jaramogi Oginga Odinga, ndiye alihakikisha kuwa Mzee Jomo Kenyatta anatolewa jela na aongoze nchi ili uhuru upatikane.

Kina Moi walikuwa tayari kupokea uhuru hata bila ya sharti hilo. Hivyo, kuna deni kwa upande wa Uhuru kwa familia ya Odinga.

Ila 'vijogoo' wa miaka ya baadaye kama Ruto hawana habari hizo.

Mbinu anazotumia Ruto ni kujaribu kuzuia suala hilo lisijadiliwe kwa upana miongoni mwa wananchi kama suala la kikatiba, ila lijadiliwe tu kisiasa kama suala la vyama, bungeni.

Wabunge wanaomuunga mkono Ruto walianza kuandaa mpango wa kukutana Mombasa kujadili ripoti ya 'Tume ya Kujenga Madaraja' ya kisiasa na uelewano miongoni mwa wananchi.

Lengo lilikuwa kuhakikisha kuwa masuala yote hayo yanajadiliwa bungeni, siyo kupelekwa kupigiwa kura ya maoni.



# TCRA yatoa mafunzo matumizi sahihi mtandao

**Na Nebart Msokwa, RUNGWE**

MAMLAKA ya Mawasiliano nchini (TCRA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini imetoa mafunzo ya matumizi sahihi ya mtandao kwa wanafunzi wa Chuo cha Ualimu Mpuguso kilichopo katika Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, huku ikiwataka wanafunzi hao kuzingatia sheria ya mtandao kuepuka adhabu.

Akizungumza na wanafunzi na watumishi wa chuo hicho, Mkuu wa Kanda wa TCRA, Asajile John, alisema lengo la kuendesha mafunzo hayo kwa wanachuo ni kuwawezesha kuzifahamu sheria na fursa zitokanazo na mitandao ya kijamii pamoja na kuhamasisha vijana matumizi sahihi ya mitandao.

John alisema kuwa mafunzo hayo pia yanalenga kuwaelimisha wanafunzi kutumia mitandao hiyo kupata maarifa na kuongeza ujuzi badala ya kufanya vitu ambavyo havina faida kwao.

Alisema kuwa kumekuwa na tatizo la watu kutumia mitandao kinyume cha sheria kwa kuandika taarifa za uongo, kutokana na matusi pamoja na mawasiliano yasiyofaa kwa mujibu wa sheria na maadili ya Mtanzania.

"Tumekuja kuwajengea uwezo hawa wanafunzi namna ya matumizi sahihi ya mitandao, lakini tunawafundisha kutambua fursa mbalimbali katika mitandao ya kijamii ikiwa ni pamoja na kupata taarifa na kuongeza ujuzi kupitia mitandao," alisema John.

Baadhi ya wanafunzi wa chuo hicho, walisema mafunzo hayo yatawasaidia kuitumia vizuri mitandao ya kijamii tofauti na ambavyo wamekuwa wakifanya kabla ya kupata mafunzo hayo na wakati mwingine walikuwa wanaishia kujadili vitu ambavyo havina tija kwao.

Mmoja wa wanafunzi hao, Elizabeth Pancras, alisema kabla ya mafunzo hayo walikuwa hawajui baadhi ya sheria zinazosimamia matumizi ya mitandao ya kijamii.

"Kupitia mafunzo haya nimejua kuwa kusajili kadi za simu kwa kutumia kitambulisho cha taifa na kuthibitisha kwa kutumia alama za vidole ni bure, kitu hiki awali wengi tulikuwa hatujui," alisema Elizabeth.

Naye Zefania Daniel, ambaye ni mwanafunzi wa mwaka wa pili chuoni hapo, alisema wanaishukuru TCRA kutoa elimu na kwamba wao kama walimu watarajiwa wanapaswa kuwa kioo katika jamii kwa kuwa na matumizi sahihi ya mitandao.

Alisema elimu waliyopewa itawasaidia kuchagua makundi sahihi kwenye mitandao ya kijamii na kwamba watakuwa walimu kwa wananchi wengine katika kuelimisha matumizi hayo ya mitandao ya kijamii.

# M/kiti aachia ngazi kupisha uchunguzi

**Na Nebart Msokwa, RUNGWE**

MWENYEKITI wa Kijiji cha Nzunda katika Kata ya Ndato, Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, Christon Tweve, amejiuzulu wadhifa wake ili kupisha uchunguzi wa tuhuma zinazoikabili serikali ya kijiji hicho za ubadhirifu wa zaidi ya Sh. 6,000,000.

Tweve alichukua uamuzi huo kwenye mkutano wa hadhara wa kusomewa mapato na matumizi ulioitishwa na Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo, Alam Swila, baada ya mkutano wa awali kuvunjika kutokana na wananchi hao kutokubaliana na taarifa za viongozi wao.

Wananchi wa kijiji hicho waliwatuhumu viongozi wa kijiji hicho kufanya ubadhirifu wa fedha hizo ambazo walizichanga kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo kati ya Julai na Novemba, mwaka jana kabla serikali za mitaa hazijavunjwa kupisha uchaguzi.

Mmoja wa wananchi hao, Omary Lackson, alisema viongozi hao walichota fedha hizo kutoka kwenye akaunti ya kijiji, lakini matumizi yake hayajulikani licha ya viongozi hao kudai zilifanya kazi kwenye kijiji hicho.

Alisema fedha hizo zingetumika kujenga vyumba vya madarasa kwa ajili ya wanafunzi, lakini hazionekani na kutokana na maelezo ya fedha hizo kutoeleweka ndio maana mkutano wa awali ulivunjika.

"Walichota fedha zote kutoka kwenye akaunti ya halmashauri ya kijiji na zikabaki Sh. 10,000.40 mpaka walipoanza kurejesha fedha hizo kwenye akaunti baada ya kukodisha mashamba ya kijiji, sasa maelezo ya matumizi ya fedha walizochota hayaeleweki," alidai Omary.

Naye, Uswege Kiangalilo, alisema wakati Mwenyekiti wa awali alipokuwa anakabidhi madaraka kwa mrithi wake alikabidhi Sh. 100,000 ambazo kwenye taarifa iliyowasilishwa kwenye mikutano yote miwili ya kusomewa mapato na matumizi haionekani.

Alisema fedha hizo pamoja na zilizochangwa na wananchi zote zimepingwa japokuwa zingine taarifa yake haiaminiki kutokana maelezo ya viongozi kutoeleweka.

Hata hivyo, katika hali ambayo siyo ya kawaida, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Ndato, Swila alimzuia Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho kujibu tuhuma zilizokuwa zinaelekezwa kwake na badala yake akawa anazijibu mwenyewe.

Alisema yeye hatakiwi kujibu tuhuma ambazo awali zilikuwa hazijawasilishwa ofisini kwake na badala yake anatakiwa kusikiliza na kujibu zile zilizowasilishwa.

"Mimi siwezi kuanza kuchokonoa mambo ya kijiji chenu, haya maswali mlitakiwa muulizane kwenye mikutano yenu ya kijiji na sio kulazimisha mambo ambayo hamkuyaweka kwenye barua yenu yajibiwe hapa," alisema Swila.

Baada ya serikali yake kutuhumiwa kwa ufisadi huo, Mwenyekiti wa kijiji hicho, Tweve, alitangaza kujiuzulu huku akiomba uchunguzi ufanyike na wahusika wachukuliwe hatua.



Baadhi ya wananchi wa Wilaya ya Kyela, mkoani Mbeya, wakitumia usafiri wa mtumbwi kama nyenzo ya usafiri wakati wakivuka katika moja ya mito jirani na Bandari ya Itungi juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# TFS yatoa eneo la shamba kwa wananchi

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WAKALA wa Hifadhi za Misitu nchini (TFS), imetoa sehemu ya eneo la shamba la miti la Kiwira lenye ukubwa wa hekari 12 na kuwakabidhi wananchi wa Kata ya Igoma wilayani Mbeya kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Mkurugenzi wa Rasilimali za Misitu kutoka TFS, Zawadi Mbwambo, alikabidhi rasmi eneo hilo kwa wananchi baada ya mchakato wa kuliondoa kwenye himaya ya serikali kukamilika.

"Kuanzia leo nakabidhi rasmi eneo hili lenye ukubwa wa hekari 12 kwa wananchi ili walitumie kwa shughuli zao za kimaendeleo, lakini kabla hawajaanza kulitumia tumeamua tuvune kwanza miti yote iliyopo ili libaki huru na tayari kwa matumizi ya wananchi," alisema Mbwambo.

Alisema kuwa uamuzi wa kutoa eneo hilo umetokana na ushirikiano mzuri uliopo baina ya shamba la miti la Kiwira, wananchi na uongozi wa Wilaya ya Mbeya, ambapo wananchi pia wamekubali kutoa eneo lao lenye ukubwa wa ekari tisa kuwa sehemu ya shamba la miti la Kiwira.

"Sio kwamba tumebadilishana, isipokuwa ni utamaduni uliopo wananchi wanapokuwa na shida na eneo wakiomba kwa ajili ya shughuli za maendeleo, tumekuwa tukitoa bila masharti yoyote, lakini hapa wananchi nao walikuwa na eneo ambalo lipo mbali na makazi yao, lakini jirani kabisa na shamba letu hivyo na wao wameamua kulitoa liwe sehemu ya shamba hili," alisema Mbwambo.

Akizungumza wakati wa kukabidhiwa eneo hilo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Mwazazi, Anderson Mussa, alisema eneo hilo ambalo limetolewa kwa wananchi lina manufaa makubwa ikiwamo kutumika kwa ujenzi wa miradi ya maendeleo yenye maslahi mapana kwa wananchi wote.

Alisema eneo hilo litapangiwa matumizi ambayo yatawanufaisha wananchi wote, ikiwamo ujenzi wa kituo cha mabasi, kituo cha Polisi, mahakama na kituo cha afya, taasisi ambazo walishindwa kuzijenga kutokana na ukosefu wa eneo.

Baadhi ya wananchi walishukuru kupewa eneo hilo kwa madai kuwa wakati eneo hilo likiwa na misitu lilikuwa likichangia kuwapo kwa matukio ya uhalifu ikiwamo vijana kulitumia kuvuta bangi, wizi na matukio ya ubakaji.

Mmoja wa wakazi wa Kata ya Igoma, Tulia Reuben, alisema uwapo wa msitu jirani na makazi yao ulisababisha vitendo vya uhalifu kufanyika, baadhi ya vijana walikuwa wakiwavizia wanawake wanaopita eneo hilo hasa nyakati za jioni na kuwabaka.

"Tumefurahi kuona msitu huu unaondolewa na eneo hilo litakuwa wazi kwa kujengwa majengo, maana lilikuwa likihatarisha usalama wetu kutokana na vitendo vya uhalifu ambavyo vilikuwa vifanyike humo hasa nyakati za usiku," alisema Tulia.

Kwa upande wake Mhifadhi Mkuu wa Shamba la Miti Kiwira, Lucas Sabida, alisema kutolewa kwa eneo hilo kwa wananchi ni matokeo ya ushirikiano mzuri baina ya shamba hilo na wananchi, ambapo wananchi pia walikubali kutoa eneo lenye ukubwa wa ekari tisa ambazo zimeingizwa kuwa sehemu ya shamba.





# Watendaji Mahakama watakiwa kutumia teknolojia

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

JAJI Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Prof. Hamis Juma, amewaagiza wafanyakazi wa mahakama kutumia teknolojia ili kupata mbinu mpya za utendaji kazi zitakazoleta ufanisi.

Kauli hiyo aliitoa jana alipokuwa akifungua Baraza la Wafanyakazi wa Mahakama jijini hapa.

Alisema wanapaswa kuwa na uelewa wa juu kuhusu masuala ya mtandao na kujenga utamaduni wa kutafuta maarifa na taarifa ili kufanya kazi kwa ubunifu katika kuhudumia wateja wao.

"Ukijua teknolojia ya mtandao itawasaidia kujua maarifa na mbinu mpya za ufanyaji kazi hasa ukizingatia hivi sasa teknolojia inakua," alisema.

Aliongeza kuwa "Ninawaomba watumishi tuisome dunia kwani kila kukicha teknolojia inakuwa na watu wanajifunza."

Jaji Mkuu alisema kuwa hivi sasa kuna mabadiliko makubwa katika mahakama na wataalamu wengi hali inayorahisisha utendaji kazi.

Alisema kwa sasa Mahakama ina utaalamu wa Tehama ambao unawapa jaji au hakimu urahisi wa kufanya kazi.

Vile vile, alisema hakuna sababu ya kuwaficha kuhusu mabadiliko ya bajeti na miradi inayotekelezwa na watumishi wa mahakama.

Alisema maboresho yanapaswa kufanywa ili watumishi wajue nini wanatakiwa kufanya.

Pia majadiliano na mapendekezo ya wafanyakazi katika baraza hilo yatasaidia kuendeleza mpango mkakati wa mahakama.

Aliwataka kufanya kazi kwa bidii na kwa ushirikiano ikiwamo kuwashirikisha wafanyakazi na watumishi wa ngazi za chini ili kuleta tija katika kuwahudumia wananchi.

**"Ukijua teknolojia ya mtandao itawasaidia kujua maarifa na mbinu mpya za ufanyaji kazi hasa ukizingatia hivi sasa teknolojia inakua," alisema.**

# Wadau wa kilimo washauri kuhusu nzige

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imeshauriwa kuwekeza kwenye utafiti na mifumo ya utoaji taarifa kwa haraka ili kukabiliana na uvamizi wa nzige kwa kuwa ni hatari kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Ushauri huo ulitolewa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Jukwaa la wadau wa kilimo wasio wa kiserikali (ANSAF), Audax Rukonge, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kongamano la sita la sera za kilimo linalotarajiwa kuanza leo jijini hapa.

"Kuna kila sababu ya kuwekeza kwenye mifumo ya utoaji taarifa mapema, tafiti, ili kukabiliana nao na tahadhari zake zichukuliwe mapema kabla ya tishio," alisema.

Alihimiza utunzaji wa vyakula vilivyopo na maandalizi ya vifaa vya kuangamiza nzige.

"Lakini tunatakuwa na swali la kujiuliza Watanzania tumezalisha vya kutosha ili kutumia fursa kutokana na nchi za Kenya na Uganda kuvamiwa, lakini je, watakapohitaji chakula sisi tutakuwa na cha kutosha," alihoji.

Akizungumzia kuhusu kongamano hilo, Rukonge alisema litajikita katika maeneo saba ambayo ni sera ya kilimo, biashara na uwekezaji, uzalishaji katika sekta binafsi.

Pia alisema litajadili upatikanaji wa pembejeo na matumizi yake, upatikanaji wa fedha na huduma saidizi, ardhi, maliasili na mazingira pamoja na usalama wa chakula na lishe.

"Tutajadili kwa kina masuala haya saba kwa kuwa idadi ya watu duniani inaongezeka Tanzania na barani Afrika kwa ujumla, Tanzania ni asilimia 2.8 kwa mwaka huku uchumi ukikua kwa asilimia saba kwa mwaka, kumekuwa na hoja nyingi kwanini uchumi unakua, lakini watu ni maskini," alisema.

Alisema kinachoonekana ni sekta zinazogusa watu wengi hazikui kwa kiwango kinachotakiwa kama uchumi unavyokua.

"Sekta ya kilimo ambayo inategemewa na wananchi wengi haikui kwa kiwango kinachotakiwa na ngazi ya uzalishaji ipo chini, kilimo bado hakijamwezesha mtu ajitegemee," alisema.

Kadhalika, alisema uchakataji wa bidhaa bado ni mdogo na viwanda vilivyopo vinategemea asilimia 65 ya mazao yanayotokana na sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi.

"Hatuwezi kuongelea sekta ya viwanda bali kuzungumzia uchakataji, huduma bado hazijawa nzuri na imara, kero za miundombinu ya barabara, upatikanaji mikopo kwa wakulima, yote yanazuia upatikanaji wa tija kwenye kilimo," alisema.

Kwa upande wake, mchambuzi wa sera ya kilimo, kutoka shirika lisilo la serikali la ASPIRES, Prof. Isaac Minde, alisema kuna umuhimu wa sekta binafsi na umma kushirikiana ili kutengeneza faida na kuhakikisha kila mwananchi anahudumiwa kikamilifu.

Alisema kongamano hilo litakuwa na watu 270 na miongoni mwa makundi yatakayokuwapo ni pamoja na wawakilishi wa wakulima, viongozi wa serikali, watafiti, wajasiriamali na asasi za kiraia.



Naibu Waziri wa Kazi, Vijana na Ajira, Athony Mavunde (mwenye kofia katikati), akiwa pamoja na viongozi wa Jiji la Dodoma, kampuni ya mabati ya Dragon na wafanyabiashara wa soko kuu jijini humo jana, katika hafla ya makabidhiano ya mabati 400, kwa ajili ya ujenzi wa paa la soko kuu la Majengo. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# DC atoa wiki wanafunzi kuripoti shule

**Na Mwandishi Wetu, KONDOA**

MKUU wa Wilaya ya Kondoa, Sezaria Makota, ametoa wiki moja kwa wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2020, wilayani humo kuripoti shule ili kuanza masomo yao.

Agizo hilo alilitoa jana wakati wa kikao cha wadau wa elimu ambacho kilikuwa kinajadili mafanikio na kero za elimu kwenye wilaya hiyo.

Alisema kuna wanafunzi bado hawajaripoti katika shule walizopangiwa na kuwataka kuripoti kabla hawajachukuliwa hatua za kisheria.

Alibainisha kuwa wanafunzi 1,240 walichaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza, 145 wameenda shule binafsi na hadi sasa wameripoti wanafunzi 1,068 huku 31 hawajaripoti hadi sasa.


"Wazazi ipo shida kwenu mwanafunzi haendi shule na haumuulizi anapaswa kupigwa fimbo au mwanafunzi mtoro anakuja kumchongea mwalimu kwa mzazi badala yake mzazi anakuja juu kwa mwalimu hii si sawa tuache kulea watoto kama mayai tutawaharibu," alisema.

Aliwataka Maofisa Elimu Kata kufanya kazi zao kwa weledi kwa kuwa baadhi yao wameonekana wazembe kwa kutotimiza majukumu yao.

Naye, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Kondoa, Hamza Mafita, alisema ili kuondokana na matatizo ya elimu katika halmashauri ni vyema kuanzisha Mfuko wa Elimu ambao utapunguza kero zinazoikabili sekta hiyo na kila kata itapewa fedha kulingana na walivyochangia.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa, Msoleni Dakawa, alisema kuanzia sasa walimu wakuu na wakuu wa shule hawataitwa kukumbushwa kutekeleza majukumu yao.

"Kuanzia sasa ni marufuku walimu wakuu na wakuu wa shule kuitwa wilayani mara kwa mara kwa kuwa kunasababisha washindwe kusimamia majukumu yao iwapo idara ina maagizo wafuateni huko huko shuleni ikiwa ni pamoja na walimu wote na viongozi kufuata sheria, taratibu na kanuni za utumishi wa umma na kushirikiana na viongozi, wazazi na wanafunzi wote ili kuinua elimu," alisisitiza.



# Sababu ongezeko taka za plastiki baharini yatajwa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KUONGEZEKA kwa taka za plastiki baharini kunatokana na udhibiti usioridhisha wa taka kwenye maeneo mbalimbali ya mjini na vijijini Zanzibar.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mihayo Juma Nhung'a, alisema hayo wakati akijibu swali katika kikao cha Baraza la Wawakilishi aliloulizwa na Mwakillishi wa Jimbo la Paje, Jaku Hashim Ayoub.

Katika swali lake la msingi, Jaku alitaka kujua serikali imejipanga vipi kudhibiti uchafu wa bahari kutokana na ongezeko la taka za plastiki.

Alisema katika kudhibiti hali hiyo serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwamo kujenga dampo la kitaalamu katika eneo la Kibele ambalo litatumika kuteketeza taka zote zinazozalishwa zikiwamo za plastiki.

Alisema pia wameandaa mkakati wa kitaifa wa usimamizi wa taka ambao unategemea kuwasilishwa kwenye ngazi za serikali kwa ajili ya kuridhiwa kwenye robo nne ya mwaka 2019/2020.

Alisema wamekuwa wakitoa elimu kwa jamii kuhusu usimamizi na udhibiti wa taka kwa kupitia njia mbalimbali ikiwamo mikutano na kuendesha kampeni za usafi wa mazingira katika maeneo ya fukwe.

Katika swali lingine Mwakilishi huyo wa Paje alitaka kujua serikali ina mpango gani wa kiwanda cha kugeuza matumizi ya taka za plastiki katika kukabiliana na athari za kimazingira.

Akijibu swali hilo Naibu Waziri Nhung'a, alisema kiwango cha taka za plastiki kinachozalishwa Zanzibar ni kidogo kuwezesha kuanzisha kiwanda cha kugeuza matumizi ya taka za plastiki.

Alieleza uanzishwaji wa kiwanda kama hicho unahitaji kuingiza kiwango kikubwa cha taka za pastiki kutoka nje ya nchi jambo ambalo ni hatari kwa ustawi wa afya na mazingira ya wananchi.

Alisema pia ni hatari kwa sekta ya utalii ambayo imekua ni nguzo muhimu kwa uchumi wa Zanzibar hivyo serikali haioni busara kuanzisha kiwanda cha kugeuza matumizi ya taka za plastiki kitakachosababisha kuingiza taka kutoka nje ya nchi.

Alieleza kuwa serikali inatambua na inathamini juhudi zinazofanywa na baadhi ya wajasiriamali ambao wanakusanya baadhi ya taka za plastiki na kuzikata kwa ajili ya kutumika kama ni malighafi ya shughuli nyingine za uzalishaji wa viwanda.



Mwakilishi wa Jimbo la Paje, Jaku Hashim Ayoub (kulia), akizungumza na Naibu Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Mihayo Juma Nhung'a, nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ yaweka mikakati kuvutia uwekezaji

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Balozi Mohamed Ramia amesema serikali imeweka mkazo maalum wa kuvutia na kufanikisha uwekezaji binafsi.

Alisema tangu miaka ya 1980 serikali imeruhusu uwekezaji binafsi na kufanikiwa kuvutia miradi mingi na mikubwa katika sekta zote za uchumi.

Alisema katika miradi hiyo ni ujenzi wa hoteli za kitalii, usafiri wa anga, baharini na nchi kavu na maeneo mengine ya kiuchumi.

Alisema hayo wakati akijibu swali aliloulizwa na Mwakilishi wa Jimbo la Mgogoni, Shehe Hamad Mantar, aliyetaka kujua hatua zilizochukuliwa kuwalinda na kuwatetea wageni wawezekezaji katika kuimarisha uwekezaji.

Balozi Ramia alisema siku zote serikali inalinda uwekezaji binafsi ikiwa ni utekelezaji wa matakwa ya kifungu cha 17 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1964 kinachoweka kinga dhidi ya kudhulumiwa mali ya mtu yeyote.

Alisema sheria za uwekezaji zilizotungwa katika kipindi chote hicho ikiwamo namba 14 ya mwaka 2018, kifungu cha 33 zinakataza mali za mwekezaji kuchukuliwa kwa nguvu.

Alieleza kuwa kwa upande mwingine Zanzibar ikiwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni sehemu ya Taasisi ya Kimataifa ya Multilateral Investment Guarentee Agency (MIGA), inayotoa kinga dhidi ya kuchukuliwa kwa nguvu kwa mali binafsi.

"Mheshimiwa Spika siku zote haki zinajulikana na wajibu...pamoja na haki hiyo ya ulinzi wa uwekezaji na mali zake, wawekezaji wana wajibu wa kutii sheria za nchi," alisema Balozi Ramia.

Alieleza kuwa wawekezaji pia wanawajibu wa kufuata masharti waliyopewa kwa uwekezaji wao ikiwamo kwa matumizi sahihi ya ardhi, kujenga mradi ulioidhinishwa na kwa muda uliokubaliwa, ulipaji sahihi kwa wakati kamili wa kodi za serikali.

# Rais Shein awafunda maofisa ununuzi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amewataka maofisa wa ununuzi na uagizaji katika taasisi za serikali kuwa wakweli, weledi, wawazi na waaminifu.

Akizungumza baada ya uwekaji wa jiwe la msingi la Mahakama Kuu mpya huko Tunguu, Mkoa wa Kusini Unguja, katika hafla ya shamra shamra za Wiki ya Sheria, aliwataka watendaji hao wasifanye mizengwe katika shughuli zao za kazi na wafuate sheria za ununuzi.

Aliwataka watendaji hao kutofanya yaliyowahi kusikika ambayo yamesababisha kuzorotesha miradi kadhaa na kwa sasa serikali haitosita kuwachukulia hatua za kisheria pale watakapogundulika kufanya hivyo.

Dk. Shein alisema serikali inawaandalia wafanyakazi wake na kuwawekea mazingira mazuri na yaliyo salama ya kufanya kazi ili wananchi waweze kupata huduma kwa urahisi na bila ya usumbufu.

Alisema kuwa ndio maana majengo kadhaa ya baadhi ya taasisi za serikali yaliyokuwa na ufinyu wa nafasi au uchakavu mkubwa yamefanyiwa matengenezo na mengine kujengwa upya katika uongozi wa awamu zilizopita na iliyopo.

Alieleza kuwa uamuzi uliochukuliwa wa kujenga jengo jipya la Mahakama Kuu umezingatia mambo mengi ikiwa ni pamoja na kutekeleza dhamira ya serikali ya kuimarisha mazingira bora na salama ya kufanyia kazi.

Alisema siku za nyuma lilikuwa linatosha kwa kutoa huduma kwa wakati huo wa karne iliyopita kulingana na mahitaji, mazingira na teknolojia iliyopo hivi sasa shughuli zimekua zikiongezeka.

Rais Dk. Shein alisema kuwa jengo la Mahakama Kuu ya Vuga lililojengwa miaka 100 iliyopita lilikidhi haja ya shughuli zake zilizokusudiwa kwa siku za nyuma kwa sababu wakati huo idadi ya watu wote wa Zanzibar ilikuwa ndogo na kwa mujibu wa sensa zilizofanyika katika miaka tofauti hapa Zanzibar zinaonyesha idadi ya watu imekuwa ikiongezeka.

"Kwa upande wa sekta ya sheria, serikali imefanyia matengenezo makubwa majengo yetu ya mahakama pamoja na kuimarisha miundombinu ya Wizara ya Katiba na Sheria na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, ili pawe na mazingira mazuri ya kutolea huduma kwa wananchi," alisema Dk. Shein.

Alieleza kwamba katika eneo hilo la Tunguu, mbali ya kujenga jengo jipya la mahakama, vile vile serikali itajenga Shule ya Sheria na kuitaka wizara husika kuhakikisha ujenzi huo unafanywa hatua kwa hatua katika Bajeti ijayo ya mwaka 2020-2021.

# Shinyanga yapigwa jeki vifaa afya, elimu

Na Mwandishi Wetu

SEKTA ya elimu na afya mkoani Shinyanga imepigwa jeki baada ya kupatiwa msaada wa vifaa tiba, madawati, mbao, mabati, vitanda na magodoro vyenye jumla ya Sh. milioni 35.

Vifaa hivyo vilitolewa na Benki ya NMB na kukabidhiwa na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, kwa zahanati ya Old Shinyanga Manispaa ya Shinyanga iliyopokea vitanda vitano vya wagonjwa, magodoro matano na mashuka 62 pamoja na Zahanati ya Usule iliyopo Halmashauri ya Shinyanga iliyopokea vitanda vinne, magodoro manne na mashuka 57, huku wakikabidhi pia madawati 100 kwa Shule ya Msingi Mwenge.

Imeelezwa kuwa lengo la msaada huo ni kuhakikisha inasaidia na kutatua baadhi ya changamoto zinazoikumba sekta ya afya na elimu mkoani humo.

Akizungumza wakati wa kukabidhi vifaa hivyo, Telack alisema mahitaji ya miundombinu katika sekta ya elimu na afya ni makubwa, hivyo akaishukuru benki ya NMB kwa msaada huo na kuwaagiza watendaji kuandaa maombi ya halmashauri zote za mkoa huo yanayohusu mahitaji ya madawati, ukamilishaji maboma na ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa ajili ya kuyapeleka katika benki hiyo yafanyiwe kazi.

"Tumepokea kwa mikono miwili msaada huu, pamoja na NMB kutushika mkono, lakini vyumba vyetu vya madarasa havitoshi lazima tuendelee kuhamasisha wananchi kujenga maboma ili serikali ije ikamilishe.

"Tangu tumeanza utekelezaji wa elimu bure kasi ya uandikishaji wanafunzi wa darasa la kwanza ni kubwa kwa hiyo tunahitaji upanuzi wa miundombinu ya ufundishaji mara tatu kuendana na kasi hii...mwaka huu maombi tutakayoleta kwa NMB yatahusu sekta ya elimu sababu ndiko tulikoelemewa," alisema Zainab.

Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Magharibi, Sospeter Magesse, alisema kila mwaka wanatenga zaidi ya Sh. bilioni 1 kusaidia jamii, ambapo ameahidi kuendelea kushirikiana na serikali kama mdau wa maendeleo kuzishika mkono zahanati, shule na vituo vya afya kwa mahitaji mbalimbali.

Magesa pia alieleza kwamba kwa mwaka 2019 NMB ilitoa jumla ya Sh. milioni 110 kwa mkono wa Shinyanga katika kusaidia mahitaji mbalimbali katika sekta ya elimu na afya, huku akiahidi kusogeza huduma za benki hiyo karibu na wananchi ambapo wanatarajia kufungua tawi katika eneo la Iselamagazi zilizohamia ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga.

"Msaada huu unahusisha madawati 100, magodoro 10, mbao 630, mabati 360, vitanda 10 vyenye jumla ya Sh. milioni 30 na mwaka 2020 tutatoa zaidi ya hapa najua kuna maboma ambayo hayajapauliwa sisi tuko tayari...Wananchi tunawakaribisha kujiunga na benki yetu hasa wakulima tunatoa akaunti bure zitakazotumika kwa malipo pale mtakapouza mazao yenu hasa pamba," alisema Magesa.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Dk. Amosi Mwenda, alisema kuwa msaada huo utasaidia kupunguza mahitaji makubwa waliyonayo hususan kwa kinamama wajawazito, ambapo wako kwenye ujenzi wa hospitali ya halmashauri inayohitaji vifaa mbalimbali.

# Tanesco yawapa angalizo wavuvi, wafugaji, wakulima

Na Romana Mallya

SHIRIKA la Umeme Tanzania (Tanesco), limewataka wavuvi, wafugaji na wakulima wanaofanya shughuli hizo pembezoni mwa mkondo wa maji yatokanayo na mabwawa ya kufua umeme na mitambo yao kuacha kufanya hivyo.

Kwa mujibu wa tangazo la shirika hilo lililotolewa jana, limewataka kuacha kufanya shughuli hizo kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha.

Tanesco imeeleza katika tangazo hilo kuwa kutokana na taarifa za Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), kuwa bado mvua zinaendelea kunyesha na zipo juu ya wastani, wanafanya tathmini iwapo siku za usoni maji yahamie upande wa pili kwa ajili ya usalama wa mabwawa na mitambo.

"Tanesco inatoa tahadhari hii muhimu kwa wananchi wanaofanya shughuli zao pembezoni mwa mabwawa, mitambo, madimbwi, mkondo wa mto, kuacha kufanya hivyo kwa kipindi hiki ambacho mvua za vuli zikiwa zinaendelea kunyesha," lilisema.

Shirika hilo lilisema kuwa ufuaji wa umeme katika mabwawa ya Mtera na Kidatu unaendelea vizuri kwa asilimia 100.

Kiwango cha maji kimeongezeka kutokana na mvua hizo zinazonyesha kuanzia mita 691.22 juu ya usawa wa bahari kuanzia Desemba Mosi mwaka jana hadi kufikia mita 698.40 juu ya usawa wa bahari Februari 10, mwaka huu katika bwawa la Mtera," tangazo hilo lilieleza.



Diwani wa Ifulifu, Musoma Vijijini mkoani Mara, Manyama Meru (kulia), akikagua maendeleo ya ujenzi wa madarasa ya sekondari mpya ya kata hiyo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadau wa misitu wapewa somo

Ná Elisabeth Zaya

MKUU wa Wilaya ya Njombe, Ruth Msafiri, amewataka wadau wa mazao ya misitu kutambua thamani ya misitu hiyo na kushirikiana katika kupambana na matukio ya moto misituni.

Aliyasema hayo wakati akifungua warsha ya siku mbili ya wadau wa misitu Nyanda za Juu Kusini iliyoandaliwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) mkoani Njombe.

Aliwasisitiza wadau kuwa na mipango madhubuti katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na kuweka sheria ndogondogo ambazo zitawalazimu wananchi kuzifuata kwa ajili ya kuondoa majanga ya moto ambayo yamekuwa yakijitokeza mara kwa mara.

Bakari Mohamed ambaye ni Ofisa Misitu kutoka TFS alisema lengo la warsha hiyo ni kuendelea kukumbushana juu ya kupambana majanga ya moto ya misituni na namna ya ushiriki wa wananchi pindi majanga hayo yanapojitokeza.

Bakari aliongeza kuwa ni vyema kutambua changamoto zilizopo ili kutafutiwa ufumbuzi ikiwa ni pamoja na kujua vyanzo, athari zilizojitokeza na namna ya kukabiliana nazo na jinsi ya kuungana katika kupambana na majanga ya moto.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Mufindi, Jamhuri William, alisema kuwa suala la matumizi sahihi ya moto liwekewe mikakati madhubuti sambamba na utoaji wa taarifa za matukio hayo kwa wakati na sheria zilizowekwa za uanzishaji wa moto kusimamiwa na viongozi wa maeneo husika.

Katika warsha hiyo, wadau waliweka msisitizo katika suala la utoaji elimu kwa jamii lipewe kipaumbele hasa katika msimu wa kiangazi ambao umekuwa na matukio mengi ya moto.

HABARI KIMATAIFA

# Mkapa asoma hotuba ya JPM maziko Moi

**NAIROBI,** Kenya

MARAIS wastaafu wa Tanzania, Benjamin Mkapa na Jakaya Kikwete jana walimwakilisha Rais John Magufuli kwenye ibada ya mazishi ya Rais mstaafu wa Kenya, Daniel Arap Moi aliyefariki wiki iliyopita.

Katika hotuba yake Rais John Magufuli ambayo ilisomwa na Rais mstaafu Mkapa katika Uwanja wa Nyayo akiandamana na Rais mstaafu Kikwete alisema uhusiano mzuri kati ya Kenya na Tanzania umeendelea kuwapo kutokana na uongozi wa Moi.

Mkapa alisema uwapo wa marais hao wawili wastaafu katika hafla hiyo ni dhihirisho tosha kwamba mataifa hayo mawili yana ushirikiano mkubwa.

Mkapa alisema licha ya kufanya kazi na Moi alimtaja pia kama mshauri wake mkuu. Halfa hiyo ilihudhuriwa pia na viongozi takribani 12 kutoka Afrika wakiongozwa na Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta katika Uwanja wa Nyayo.

**licha ya kufanya kazi na Moi alimtaja pia kama mshauri wake mkuu. Halfa hiyo ilihudhuriwa pia na viongozi takribani 12 kutoka Afrika wakiongozwa na Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta katika Uwanja wa Nyayo.**

**UHURU KENYATTA**

Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta akiongoza maelfu ya Wakenya waliokusanyika katika mazishi hayo alisema anamsherehekea Moi kama kiongozi na mwanahistoria.

Alisema Moi alikuwa kiongozi aliyeweza kutabiri hali ya siku zijazo ya kisiasa.

"Tunakumbuka aliyekuwa Makamu wa Rais wa kwanza wa taifa hili akisema kamba Moi alikuwa twiga wa kisiasa," alisema Kenyatta.

Kenyatta alisema uongozi wake wa kutaka kuleta amani ulipita mipaka.

**WILLIAM RUTO**

Makamu wa Rais wa Kenya, William Ruto akihutubia umati uliofika katika mazishi hayo alisema Moi anapaswa kuheshimiwa kwa kuleta makabila yote serikalini.

Alisema japokuwa hakuwa kamili kama mwanadamu mwingine miaka mitatu iliyopita alikuwa akilitakia mema taifa hili.

**RAILA ODINGA**

Katika hotuba aliyoitoa kwenye mazishi hayo, aliyekuwa Waziri Mkuu wa Kenya, Raila Odinga alisema japokuwa Moi alikuwa na makosa lakini alisaidia katika kutengeneza katiba mpya mbali na kuleta elimu kwa wote pamoja na maziwa ya Nyayo.

Raila alisema Moi anafaa kukumbukwa kwa mazuri aliyotenda badala ya mabaya anayohusishwa nayo.

**MWAI KIBAKI**

Akizungumza katika hafla hiyo Rais mstaafu wa Kenya, Mwai Kibaki ambaye hotuba yake ilisomwa kwa niaba yake alisema Moi aliliongoza taifa la Kenya kama kiongozi thabiti.

Alisema aliwahudumia Wakenya kwa kipindi kirefu mbali na kukabidhi mamlaka kwa mrithi wake kwa njia ya amani alipostaafu.

**PAUL KAGAME**

Naye Rais wa Rwanda, Paul Kagame alimsifu Moi kama kiongozi aliyeunganisha makabila tofauti nchini Kenya na kuleta amani katika eneo zima la Afrika Mashariki.

**YOWERI MUSEVENI**

Naye Rais wa Uganda, Yoweri Museveni ambaye alialikwa kuhutubia hafla hiyo kama mzee wa boma la Afrika mashariki na mwenyeji wake Uhuru Kenyatta alisema licha ya kifo kuwa ni lazima kwa mwanadamu yeyote, kila mtu atakumbukwa na alichokifanya duniani.

Alisema Moi atakumbukwa kwa mazuri aliyoleta Kenya na eneo la Afrika mashariki kwa ujumla. Alisema Moi alikuwa dawa ya kenya kwa kuwa aliweza kuliongoza taifa hili bila ya migogoro.

Alisema hatua yake ya kukiongoza chama cha KADU kufanya muungano na KANU ilikuwa dhihirisho tosha kwamba ni kiongozi aliyetaka mshikamano wa nchi.

Jana, mwili wa Moi uliondolewa katika chumba cha kuhifadhi maiti cha Lee mapema alfajiri chini ya ulinzi mkali. Msafara wa jeneza lake uliendа hadi katika Ikulu ya rais.

Baadaye uliondoka katika Ikulu ya rais na kuelekea hadi Uwanja wa Nyayo majira ya saa tatu asubuhi na kwamba Wakenya walisubiri kuwasili kwa mwili wake kabla ya ibada hiyo.

**HALI ILIVYOKUWA**

Kuanzia majira ya saa 11 alfajiri, watu walikuwa wamepanga misururu mirefu kuingia katika uwanja huo.

Mabasi ya shule kutoka maeneo mbalimbali yaliotumika kusafirisha watu hadi katika uwanja huo yaliegeshwa katika maeneo tofauti ya mji huku watu wakitakiwa kushuka na kupanga foleni karibu na barabara ya Bunyala.

Mwili wake ulipitishwa ndani ya uwanja huo polepole na kusindikizwa na wanajeshi kutoka Jeshi la Kenya.

Mwili wake uliokuwa ndani ya jeneza ulibebwa na gari maalumu na nyuma ya gari hilo kulikuwa na gari lingine ambalo liliwabeba watoto wa kiongozi huyo akiwamo mtoto wake wa kike aitwaye June Moi, Raymond Moi ambaye ni Mbunge wa Rongai na Gideo Moi Seneta wa Baringo.

Rais Uhuru Uhuru Kenyatta na mkewe Margaret Kenyatta waliwasili katika uwanja wa Nyayo kwa ibada ya mazishi ya kitaifa majira ya saa tatu. **BBC**

## Watano wafariki shambulio la kujitoa mhanga

**KABUL,** Afghanistan

WATU wasiopungua watano wameuawa katika shambulio la kujitoa mhanga Magharibi mwa mji wa Kabul.

Shambulio hilo lililotokea jana na kwamba mamlaka imesema ni mlipuko wa kwanza baada ya miezi miwili ya utulivu katika mji mkuu wa Afghanistan.

"Mapema asubuhi, mshambuliaji wakujitoa mhanga, alijilipua na kuua watu watano wakiwamo raia wawili na askari watatu," alisema Nasrat Rahimi Waziri wa Mambo ya Ndani.

Alisema shambulio hilo pia limewajeruhi watu 12 wakiwamo raia watano na kuongeza kuwa idadi hiyo inaweza kubadilika.

Wizara ya Ulinzi imesema watu watano wameuawa, raia mmoja na wanne kutoka vikosi vya usalama - na sita wamejeruhiwa.

Hakuna kundi ambalo limedai kuhusika na tukio hilo, ambalo lilitokea kwenye eneo la kwanza la ukaguzi kwenye lango la Chuo Kikuu cha Jeshi.

Mkuu wa Polisi wa Kabul amethibitisha shambulio hilo na kudai kuwa yeye ndio alikuwa amelengwa. **RFI**



Mwili wa Rais wa zamani wa Kenya, Daniel Arap Moi ukiwa umebebwa na askari wakati ukiingia katika Uwanja wa Nyayo kwa ajili ya ibada ya mazishi. **PICHA: REUTERS**

## Idadi waliofariki na corona yafikia 1,000

**BEIJING,** China

IDADI ya vifo vinavyosababishwa na mlipuko wa ugonjwa wa corona imefikia 1,000 hadi jana.

Wakati huohuo, Shirika la Afya Duniani (WHO), limesema idadi kubwa ya matukio ya maambukizi nje ya nchi hiyo inaweza kuzidi na kusambaa zaidi kwa ugonjwa huo duniani.

Hivi karibuni Shirika la Afya Duniani (WHO) lilipeleka ujumbe wa wataalamu nchini China kushirikiana na maofisa wengine wa afya kudhibiti kusambaa kwa ugonjwa huo.

Kifo cha kwanza kilichotokana na virusi vya 2019-nCoV, ambavyo viligunduliwa Desemba katika mji wa katikati mwa China wa Wuhan, vilitangazwa Januari 11.

Mwezi mmoja baadaye, ugonjwa huo sasa umeua watu 1,016 kwa China pekee (ukiondoa Hong Kong na Macao), kulingana na ripoti rasmi iliyochapishwa hivi karibuni.

Maofisa wa afya nchini China wameripoti vifo vipya 108 ndani ya saa 24 ikiwa ni idadi kubwa zaidi tangu kuzuka kwa ugonjwa huo, wakati kesi za maambukizi zikifikia zaidi ya watu 42,000.

Kwa upande mwingine, tangu wiki iliyopita, idadi ya matukio mpya ya kila siku (2,478) imepungua ikilinganishwa na siku iliyopita.

Jumatatu wiki hii Rais wa China, Xi Jinping alitoa wito wa kuchukuliwa hatua kali zenye maamuzi ili kudhibiti kuenea kwa ugonjwa huo baada ya kutembelea eneo la makazi la Beijing kuzuru hospitali.

Rais Xi Jinping alionekana kwa mara ya kwanza amevalia kitambaa cha kufunika uso kwa ajili ya kujikinga na pia alipima afya yake. **RFI**

# Waziri Ummy ahimiza uwekezaji afya watoto

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amewataka wazazi kuwekeza kwa watoto katika kupata huduma bora za afya ili kuwawezesha kupata elimu bora itakayowasaidia watoto kutimiza malengo yao.

Mwalimu aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizindua akaunti za watoto na vijana zinazojulikana kama Malaika, Janja, Kizazi Kipya na Hazina za Benki ya UBA ambazo zimetengenezwa kulingana na umri wa watumiaji.

"Nitumie fursa hii kuwahimiza walezi na wazazi wa watoto kuwa na utaratibu wa kuweka akiba kwa elimu ya watoto wetu. Hii itasaidia kufikiwa kikamilifu kwa haki ya kuendelezwa mtoto," alisema.

Waziri aliiomba UBA kuunganisha huduma za akaunti za watoto na huduma ya Bima ya Afya ili kuwezesha Watanzania walio wengi kupata huduma za afya hasa kwa watoto ambao wamekuwa na changamoto nyingi za kiafya hasa katika ukuaji wao.

"Nawapongeza kwa ubunifu wa kuwa na akaunti hizo za watoto kulingana na rika, lakini nawaomba muunganishe akaunti hizi na bima ya afya kwa watoto itakuwa msaada mkubwa kwa wazazi na walezi," alisema.

Pia aliutaka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kuona namna ya kuunganisha huduma za akaunti hizo na bima ya afya kwa sababu watoto chini ya umri wa miaka 18 wanaweza kujiunga kwenye huduma ya watoto afya kadi ambayo inaweza kuwafikia watoto wengi.

Aidha, aliipongeza Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya UBA Tanzania kwa kubuni huduma hizo mpya zinazoendana na umri wa watoto kwa sababu itachangia maendeleo ya watoto na vijana.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa UBA Tanzania, Usman Isiaka, alisema huduma hizo ni mwendelezo wa falsafa ya benki hiyo ya kutoa huduma kulingana na uhitaji wa wateja, mahali wanapotaka na kwa njia wanayotaka kuipata huduma hiyo.

"Benki ya UBA Tanzania tuna mtazamo wa kutoa bidhaa na huduma mbalimbali kulingana na teknolojia na zilizo bora kwa wateja kwa lengo la kuboresha soko letu na ushindani katika sekta ya kibenki nchini Tanzania," alisema.

Katika uzinduzi huo Waziri Mwalimu alizindua huduma za akaunti ya Malaika ambayo inalenga watoto kuanzia umri wa siku moja mpaka miaka 12, akaunti Janja kwa watoto kuanzia miaka 13 mpaka 17 ambao wanakuwa kwenye shule za msingi na sekondari, akaunti ya Kizazi Kipya inayolenga wanachuo na vijana wenye miaka 18 mpaka 25 na akaunti ya Hazina kwa watu wote wenye nia ya kujiwekea akiba kwa lengo la kutimiza lengo husika.




Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, akikata utepe na watoto kuashiria uzinduzi wa akaunti za watoto na vijana zinazojulikana kama Malaika, Janja, Kizazi Kipya na Hazina za Benki ya UBA, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: WIZARA YA AFYA**

## DC aangazia msako walevi, wazururaji

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKUU wa Wilaya ya Babati, Elizabeth Kitundu, ametangaza kuanza kwa kamatakamata ya makundi ya wazururaji na walevi wanaotajwa kuwa sehemu ya watu wanaochangia kushamiri kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Akizungumza na Nipashe jana, Kitundu alisema tayari amemwagiza Mkuu wa Polisi wa Wilaya (OCD), kuanza mara moja kwa utekelezaji wa operesheni hiyo.

"Ulevi ni chanzo kikubwa sana cha ubakaji na ulawiti katika wilaya yetu, na tayari nimeishaagiza Polisi kuwakamata wazururaji na walevi ambao wana nafasi kubwa ya kushiriki matukio haya ya ukatili," alisema Kitundu.

Takwimu za Mkoa wa Manyara zinaonyesha kuwa matukio 226 ya ukatili wa kingono dhidi ya watoto yaliripotiwa mwaka 2019 wakati katika Wilaya ya Babati, watoto chini ya miaka minane waliobakwa ni zaidi ya 20.

Alisema wanaobaka inaonekana si watu wa kawaida, akiwatuhumu walevi na wazururaji kwamba ndio watuhumiwa wanaoweza kuangaliwa katika matukio hayo, kwa kuwa haiwezekani mtu mwenye akili timamu akawabaka watoto wadogo.

Licha ya kutangaza msako huo, alisema hautakuwa mwarobaini kwa wabakaji badala yake anasema watajikita kutoa elimu kupitia idara ya elimu.

"Katika elimu ambayo tutaitoa kwa watoto ni kuwafundisha kujitambua na wakatae watu watakaowaita watakapokuwa wanatoka shuleni ili waepuke kufanyiwa ukatili huo," alisema Kitundu.

Kuhusu polisi kuwaachia watuhumiwa wa matukio ya namna hiyo, alisema inabidi polisi waangalie wananchi wasije kujichukulia sheria mkononi kwa kuwa haiwezekani mwathirika bado yuko hospitalini halafu mtuhumiwa aachiwe hata kama ana haki ya kupata dhamana.

Mkazi wa Babati, Kato Isaya, aliishauri serikali kuwasaka kwa gharama yoyote watuhumiwa wa ubakaji wa watoto maana kuwaacha ni kuhalalisha uovu huo.

# Chanzo ongezeko mirathi, matunzo watoto bayana

**Na Dege Masoli,** TANGA

MRATIBU wa Chama cha Wanasheria Wanawake Mkoani Tanga (Tawla) Wakili Latifa Mwabondo, amesema sababu za ongezeko la mashauri yanayohusu mirathi na matunzo kwa watoto linatokana na kuvunjika kwa uhusiano baina ya wazazi.

Mwabondo alisema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusiana na ongezeko la mashauri ya mirathi na madai ya kutelekezwa kwa watoto ambayo alisema yamekuwa tishio kwa kipindi hiki.

Alisema mashauri ya mirathi na yale ya kudai matunzo ya watoto, wameshika kasi kipindi hiki kutokana na kinamama wengi kuzalishwa na kutekelezwa wakiwa na watoto kwa sababu mbalimbali, ikiwamo kuvunjika kwa uhusiano na kiuchumi.

Mwabondi alisema lililoathirika sana kuwa ni wasichana wadogo ambao wameanza kuwalea watoto au kuzaa wakiwa na umri mdogo hali ambayo alisema ni tishio kuwa na idadi kubwa ya ongezeko la watoto wa mitaani kama hali hiyo haitadhibitiwa mapema.

Licha ya vitendo hivyo kupigwa vita kama ukatili, alisema hali inatisha na kwamba endapo hakutakuwa na mipango madhubuti ya kukabiliana na ndoa za utotoni au masuala ya mimba za utotoni kwa Mkoa wa Tanga, athari zake zitakuwa kubwa zaidi.

Alisema baadhi ya maeneo kunaripotiwa matukio ya ukatili lakini wanawake wanashindwa kujitokeza kutoa ushirikiano kutokana na kuona aibu, kuogopa au kuonekana na jamii kuwa ni watu waliyofanyiwa mambo mabaya.

Kuhusu wanavyolishughulikia tatizo hilo, Mwabondo alisema kwa mara ya kwanza walianza na wananchi wachache na kadri wanavyoendelea, wamepata mafanikio makubwa kutokana na ushirikiano wao na wenyeviti wa mitaa.

"Wenyeviti wa mitaa wengi walikiri maeneo yao kuwapo kwa matendo ya kikatili na hayo yalikuwapo kwa mkoa mzima wa Tanga, hivyo tukawaomba waende wakatoe msaada katika maeneo yao lakini kinachowanashangaza wananchi hawajitokezi kama walivyoelezwa," alisema.

Akizungumzia suala la mirathi, alisema kwenye familia kumekuwa kukiibuka uvamizi wa mali za marehemu kutoka kwa ndugu wakiwamo mashemeji na madada ambao wanahodhi mali zilizoachwa na hatimaye kusababisha walengwa kushindwa kunufaika nazo.

Wakili huyo alisema hali hiyo imesababisha ongezeko la migogoro huku wahusika wakishindwa kupeleka mrejesho mahakamani unaofaa na mwisho wake kutokea mateso makubwa kwa jamii.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NYUMBA INAUZWA MIL 70 ARUSHA NGULELO:,** SELF VYUMBA 3 KIMOJA MASTER, SITTING, JIKO NA STORE, INA UMEME NA MAJI INAFAA KUISHI, FINISHING NA FENSI UNAIMALIZIA.MWENYE NYUMBA 0757 804 970


*NIPASHE NI JIBU LAKO*

NJOO UTANGAZE NASI

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RODRICK KAILEMBO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 516 CJH TOYOTA VITZ.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **DAR/OST/R-B/298752/2019.**

215626001

## 'SEALING PLIER' IMEPOTEA

**JUMA MASHAKA KALUTA** Anatangaza kupotelewa na **'SEALING PLIER'** yenye namba 035 ambayo ni mali ya wakala wa Vipimo iliyotolewa na Kamishna wa Vipimo tarehe **06/01/2014.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa Polisi.

Taarifa ya Polisi: **MWA/NY/RB/125842/2020**

Au apige simu namba **0767-050377 au 0717-050377**

115625802

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ANNA ERNEST SHAYO**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba ya usajiri **T 639 CPN TOYOTA NOAH**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo Cha Polisi

Taarifa ya Polisi

**ARU/ARU/RB/434841/2019**

215624802

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Ndg. Gervansio Kamore Mbuthia** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 701 ABU** Toyota Corolla rangi ya Silver. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

TAARIFA YA POLISI : **MBE/MBE/RB/482510/2019.**

115625202

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**PRAYGOD ALETAULWA MUNUO,** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 476ATJ.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **SJ/RB/845/2019.**

115625102

## KUPOTEA KWA VYETI



**Yahaya Saidi Jumanne** anatangaza kupotea kwa chati cha kidato cha nne chenye index namba **S.3972/0021** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2012, katika shule ya Sekondari Pohama na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0129/0685** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2015 katika shule ya Sekondari Mara. Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **MWA/NY/RB/230853/2019**

115625002

## CHETI KIMEPOTEA



**Askrit Laurent Mkonge** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **P0328-0502** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa Mwaka 2015 katika shule ya Sekondari Mawenzi. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kwenye kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi: **IRI/IRI/RB/132725/2020**

215625602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No; 28/2020**

**Ombi la SAID ABDALAH MALANGE**
**Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu**
**HAMZA SAID MALAMLA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 24/02/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 10/02/2020.

Tarehe 10/2/2020

Sahihi ya Hakimu

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO MJINI MOROGORO

115625702

## KUPOTEA KWA KADI

**JIAXING JIANG** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **T/CRUISER** yenye usajili wa namba **T357 DEW** iliyotolewa na Mamlaka ya mapatao Tanzania.Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: **DAR/KJN/RB/130321/2020**

115624902

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MICHAEL MUINDE GAMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 237 DDF MITSUBISHI PAJERO.** Chassis namba **V454504847.** Engine namba **6G74EAA4847.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/KIJ/RB/133144/2020.**

115625302


**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# OZIL HAJUI HATIMA YAKE KIKOSINI




**LONDON,** England

MESUT Ozil amedai hana uhakika na majaliwa yake ya baadaye licha ya kwamba ana furaha kwa wakati huu kuendelea kucheza Arsenal.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 ameanza mechi zote za Ligi Kuu England kwa Arsenal tangu kutua kwa Mikel Arteta, Desemba mwaka jana, akitoka kuwa na wakati mgumu chini ya kocha, Unai Emery.

Huku akiwa amebakiwa na mwaka mmoja kwenye mkataba wake, Ozil amekuwa akihusishwa na mpango wa kwenda kwenye klabu ya DC United inayoshiriki Ligi Kuu Marekani, MSL, pamoja na Fenerbahce ya Uturuki.

"Baada ya msimu huu nina mwaka mmoja zaidi na baada ya hapo sijui nini kitatokea, siyaoni majaliwa yangu," amesema akiwaambia waandishi wa habari wakati wa mazoezi ya Arsenal mjini Dubai.

"Ninachoweza kufanya ni kujitoa kila kitu kwa timu, kwangu mwenyewe na kuwa na mafanikio na baadaye tunaona nini kitakachotokea."

Arsenal ipo nafasi ya 10 kwenye msimamo wa Ligi Kuu, ikipitwa pointi 10 kutoka nafasi ya nne, ikiwa imeshinda mchezo mmoja tu kati ya nane kwenye Ligi Kuu England tangu kutua kwa Arteta Desemba 20 mwaka jana.

Hata hivyo, Ozil amesisitiza kuna ishara ya kuimarika kwa timu ni ya kocha huyo msaidizi wa zamani wa Manchester City na anaamini bado wana nafasi ya kufuzu michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.



## *Mourinho afurahia kuwapo Spurs*

**LONDON,** England

JOSE Mourinho anafurahia msimu wake wa kwanza pale Tottenham ingawa inadaiwa kwamba anajutia kuchukua uamuzi wa kuwa kocha wa klabu hiyo.

Mourinho alichukua nafasi ya Mauricio Pochettino Novemba mwaka jana, lakini amejikuta hana wakati mzuri zaidi hapo Spurs. Ameshinda mechi 10 kati ya 19 tangu alipochukua mikoba hiyo, huku Tottenham wakiwa nafasi ya sita kwenye msimamo, wakipitwa pointi nne na klabu yake ya zamani ya Chelsea katika mbio za nne bora.

Raia huyo wa Ureno amesema kwamba, anafurahia wakati mzuri akiwa kwenye klabu hiyo, licha ya kukabiliwa na changamoto kadhaa.

"Kuna watu ambao wanataka kuwa kwenye habari kila siku na kuongea vitu ambavyo sio vya kweli, lakini nina furaha kubwa kuwa kwenye klabu hii," alisema Mourinho akiiambia Sky Sports. "Magumu? Ndio, lakini hakukuwa na magumu mengi ambayo yangenifanya nishindwe kutimiza wajibu wangu.

"Nawapenda wachezaji. Napenda sana mahusiano yao. Ukiona sura mbaya kwangu ni kwa sababu ya matokeo mabaya."

## Emery awatupia dongo mastaa Arsenal

**LONDON,** England

UNAI Emery anahisi Arsenal walikuwa "wameshuka kiwango kwa miaka miwili" kabla ya kutua pale na amelaumu mtazamo wa wachezaji nyota.

Emery alifukuzwa Novemba mwaka jana baada ya kukaa hapo kwenye dimba la Emirates kwa miezi 18 ambapo miamba hao wa London walikuwa na rekodi mbaya zaidi ya kutoshinda mechi tangu mwaka 1992.

Kocha huyo wa zamani wa Paris Saint-Germain alisisitiza alichukua nafasi ya Arsene Wenger wakati timu hiyo ikiwa kwenye kiwango kibovu na anaamini mtazamo wa baadhi ya wachezaji nyota uliifanya timu hiyo kushindwa kupata matokeo mazuri.

Emery anahisi kwamba angeweza kuibadilisha Arsenal kama angepewa nafasi zaidi ya kuendelea kuwapo pale.

"Arsenal ilishuka kiwango kwa miaka miwili kabla ya mimi kutua pale," alisema kocha huyo raia wa Hispania.

"Tulimaliza tatizo hilo kwa kuweza kutinga fainali ya Kombe la Europa na kumaliza ligi tukiwa nafasi ya tano kwenye msimamo nyuma ya Tottenham, ingawa tulipata pointi moja tu katika mechi tano za mwisho.

"Tulikuwa na nafasi ya kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini mambo yalikwenda tofauti mwisho kabisa. Lakini ulikuwa msimu mzuri na tulikuwa na mpango wa kuendelea.

"Lakini tuliwapoteza manahodha wetu wanne: (Laurent) Koscielny, (Petr) Cech, (Aaron) Ramsey na (Nacho) Monreal."



## HABARI MICHEZO

# ‘Fernandes kama ana miaka miwili Man United’

**MANCHESTER,** England

BRUNO Fernandes ameimarika vizuri pale Manchester United na kuonekana kama amekaa hapo kwa zaidi ya miaka miwili, kwa mujibu wa mchezaji mwenzake, Diogo Dalot.

Fernandes alianza kuichezea United kwenye sare ya bila kufunga dhidi ya Wolves Februari Mosi, akiwa amejiunga na klabu hiyo ya Ligi Kuu England akitokea Sporting CP mwezi uliopita. Dalot alisema raia huyo mwenzake wa Ureno amejiimarisha vizuri hapo United, ambao wako nchini Hispania kwa likizo fupi ya mapumziko.

“Anaonekana kama vile yupo hapa kwa miaka miwili tayari,” alisema beki huyo wa pembeni akinukuliwa na tovuti ya klabu yake.

“Anacheza vizuri na yuko poa kabisa, ni jambo zuri sana kuwa naye hapa, ni jambo zuri kwa upande wangu, jambo zuri kwa timu na anaonekana kufurahia kukaa hapa.

United imekuwa na msimu mbaya na sasa wapo nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu, lakini bado wako kwenye michuano ya Kombe la FA na Ligi ya Europa.





# HIERRO AFAGILIA KIWANGO CHA RAMOS

**MADRID,** Hispania

FERNANDO Hierro amemtaja nahodha wa Real Madrid, Sergio Ramos kama “mchezaji wa kipekee” na amemsifia beki huyo kwa rekodi yake ya kufunga mabao.

Ramos alimpita Hierro katika nafasi ya tano baada ya kuweka rekodi ya kucheza mchezaji mechi nyingi zaidi za Ligi Kuu Hispania, LaLiga, kwa Real Madrid wakati wa mchezo wa ushindi dhidi ya Osasuna Jumapili na sasa amefikisha mechi 440.

Mlinzi huyo alifunga bao lake la sita msimu huu wakati wa ushindi huo wa 4-1 kuwawezesha Madrid kuendelea kukaa kileleni mwa msimamo na kuongoza kwa tofauti ya pointi tatu.

Hierro, gwiji wa Madrid, alisema kile ambacho amekifikia Ramos ni cha kufurahisha na kumtaja kuwa ni mchezaji wa kipekee.

“Sergio Ramos bila shaka yoyote ni mchezaji wa aina yake,” alisema Hierro akinukuliwa na mtandao wa LaLiga.

“Miaka iliyopita sisi walinzi tulikuwa na nafasi kubwa ya kufunga, mara kwa mara tulikuwa tunacheza nafasi ya kiungo. Lakini kwa maisha ya sasa ya soka katika karne hii ya 21 Sergio ni mchezaji wa kipekee.

“(Gerard) Pique huwa anafunga mabao machache pia, lakini Sergio ni wa aina yake.”

# Klinsmann aamua kuitosa Hertha Berlin

**BERLIN,** Ujerumani

KOCHA Jurgen Klinsmann ameamua kuachana na Hertha Berlin ikiwa ni siku 76 tangu atue katika kikosi cha timu hiyo na kuiongoza kwenye michezo 10.

Kocha huyo wa zamani wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, ambaye alishinda mechi tatu kati ya michezo 10 akiwa kocha wa timu hiyo, amebainisha kukosekana kwa uaminifu na ushirikiano ndio kumepelekea achukue uamuzi huo.

Kilnsmann alisema: “Kama kocha mkuu, ninahitaji watu waaminifu na wawajibikaji wakati wote.

“Hasa mkiwa katika harakati za kujinasua na janga la kushuka daraja, umoja, kujituma na kuwa na malengo ya msingi ni vitu muhimu kwenye vita hii.

“Kama hakuna ambaye anawajibika, siwezi kuendelea kuwa hapo kama kocha na kukamilisha majukumu yangu.”

Klinsmann ameiacha timu hiyo ikiwa kwenye nafasi ya hatari kwenye msimamo huo wa Bundesliga, iko pointi sita nyuma ya timu zilizoko katika mstari wa kushuka daraja, nafasi ya 14 baada ya kushuka dimbani katika mechi 13.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# JUVENTUS YAJIPANGA KUMNG'OA GUARDIOLA

●●● Yamtaka Mhispania huyo kusema kiasi chochote cha fedha anachotaka ili...

**TURIN,** Italia

KLABU ya Juventus inajipanga kumwajiri Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola na iko tayari kumruhusu Mhispania huyo mwenye umri wa miaka 49 kutaja dau lolote analolitaka ili aweze kutua kwenye Uwanja wa Allianz.

**Vigogo hao wa Italia wamesema fedha si kikwazo kwao na wako tayari kutumia kiasi kikubwa ili kuhakikisha Guardiola anatua Turin na kufundisha katika Ligi ya Serie A kwa mara ya kwanza.**

Juve ilimwajiri Maurizio Sarri katika majira ya joto, lakini tayari imeshaanza mchakato wa kumwajiri Guardiola kama kocha mzoefu, imeandika gazeti la Sun.

Rais wa Juve, Andrea Agnelli amesema wanatarajia kumshawishi Guardiola ambaye siku za nyuma waliwahi kumkosa.

Kwa sasa Juve wako katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Serie A kwa tofauti ya mabao, wakiwa nyuma ya vinara Inter Milan.

Inter, ambayo inaongozwa na Kocha Antonio Conte, imetumia kiasi kikubwa cha fedha ili kuhakikisha wanarejea katika ufamle wa soka barani Ulaya.

Sarri amekalia kuti kavu katika kikosi hicho huku akiwa na jukumu la kuhakikisha wanashinda taji la tisa la Serie A mfululizo.

Mkataba wa Guardiola na City kwa sasa unamfanya aweke kibindoni kiasi cha pauni milioni 15 kwa mwaka ingawa msimu huu ameshindwa kufanya vema kutokana na mahasimu wao Liverpool kufanya vizuri zaidi kwenye Ligi Kuu England.

Kikosi cha Jurgen Klopp ambacho kinawania ubingwa wa ligi kiko mbele kwa tofauti ya pointi 22 na tetesi za kuondoka kwa Guardiola zimekuwa zikisema kwa wiki za hivi karibuni.

Baada ya City kutwaa taji la Ligi Kuu England Mei mwaka 2018, Guardiola alisisitiza haendi kokote ingawa Juve imeonyesha nia ya kuhitaji huduma yake.

Tangu kocha huyo raia wa Hispania alipokiri City ina kikosi imara na uwezo wa kufanya vema hata asipokuwapo, tayari alianza kuzivutia klabu mbalimbali kuanza kufuatilia saini yake.

## ZISIKUPITE

### COUTINHO AGOMBEWA

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Brazil, Philippe Coutinho (27), anaweza kuondoka Barcelona endapo klabu inayomhitaji italipa ada ya pauni milioni 77 katika majira ya joto, huku Manchester United, Chelsea, Manchester City, Tottenham na pamoja na timu yake ya zamani Liverpool pia ikimwania. ***(Express)***

### HAALAND KUMRITHI AGUERO

MANCHESTER City imemtaja straika wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya Norway, Erling Braut Haaland (19), anaweza kuwa mrithi wa straika wa Argentina, Sergio Aguero, ambaye ana umri wa miaka 31. ***(90min.com)***

### AKE, DIAS WANUKIA SPURS

KOCHA wa Tottenham, Jose Mourinho amesema anataka kumsajili beki wa kati wa Bournemouth na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Nathan Ake (24) pamoja na beki wa Benfica na Timu ya Taifa ya Ureno, Ruben Dias (22), katika majira ya joto. ***(Express)***

### SANCHEZ SOKONI

MANCHESTER United inatafuta klabu ambayo inaweza kumnunua Alexis Sanchez (31), ili kufanikisha mchakato wa kumwondoka klabuni hapo mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Chile ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Inter Milan. ***(Manchester Evening News)***

### MKHITARYAN HAKIJAELEWEKA

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Armenia, Henrikh Mkhitaryan (31), atarejea Arsenal katika majira ya joto akitokea katika timu yake ya mkopo ya Roma isipokuwa Gunners wakikubali kushusha bei ya nyota huyo ambaye sasa thamani yake ni pauni milioni 20. ***(Sun)***

### DOUCOURE AFUNGUKA

KIUNGO wa Watford Mfaransa Abdoulaye Doucoure, ambaye ana umri wa miaka 27, anataka kucheza mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na anaumia kuona klabu hiyo maarufu Hornets haina nafasi ya kutimiza malengo yake. ***(Mail)***

### CHELSEA, VILLA VITANI

CHELSEA, Aston Villa na Newcastle United zote zimeonyesha nia ya kumsajili beki wa kushoto wa Wigan, Antonee Robinson (22), baada ya Mmarekani huyo kushindwa kukamilisha usajili wa kujiunga na AC Milan katika dirisha dogo la Januari. ***(Mirror)***

### WILLIAMS MAMBO SAFI

LIVERPOOL inajipanga kumpa mkataba mpya beki wake wa kulia raia wa Wales, Neco Williams, ambaye ana umri wa miaka 18. ***(Express)***

### CORONA KUIKIMBIZA UNITED

MANCHESTER United imesimamisha mpango wake wa kwenda China kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa 2020/21 kwa sababu ya uwapo wa virusi vya ugonjwa wa corona baada ya kupanga ziara hiyo tangu mwaka jana. ***(ESPN)***

### ITALIA YAMBEBA ERIKSEN

KIUNGO wa zamani wa Tottenham, Christian Eriksen (27), ambaye sasa yuko katika kikosi cha Inter, amesema hakuwahi kufikiria vuguvugu lolote kuhusiana na 'dabi' la Milan alipokuwa anacheza katika Ligi Kuu England. ***(Goal)***

## HABARI MICHEZO

# KOCHA SINGIDA UNITED AAHIDI MAMBO MAZURI

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Singida United, Ramadhan Nsanzurwimo amesema licha ya kupitia katika kipindi kigumu, bado ana imani na kikosi chake hakitashuka daraja msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nsanzurwimo alisema wanapambana na changamoto mbalimbali zilizopo katika timu hiyo ili kuhakikisha wachezaji wao wanapata ushindi kwa michezo inayofuata.

Nsanzurwimo alisema mbali na changamoto walizonazo lakini pia ushindani ndani ya ligi ni mkubwa jambo linalowafanya wawe na wakati mgumu katika kutimiza malengo yao.


**"Kwa sasa mambo kwetu bado ni magumu kwasababu matokeo tunayopata sio yale ambayo tu nayatarajia, matumaini yetu ni kwamba muda wa haya yote utakwisha na tutarejea kwenye furaha upya, mashabiki watupe sapoti," alisema Nsanzurwimo.**

Hata hivyo kocha huyo alisema wanalazimika kupambana kushinda mechi zao zote za ugenini na nyumbani ili kunusurika na 'janga' hilo la kushuka daraja.

"Sasa hivi tuna mechi mbili za nyumbani, tayari wachezaji wangu wameniahidi kupambana kushinda mechi hizo pia kupigania kuinusuru timu katika nafasi iliyopo sasa," alisema Nsanzurwimo.

Singida United yenye pointi 11 jana ilitarajia kuikaribisha Namungo FC kwenye Uwanja wa Liti mkoani Shinyanga, ilihitaji ushindi ili kutoka mkiani.

Jumla ya timu nne zitazoshika mkia katika msimamo wa ligi, zitashuka daraja moja kwa moja wakati nyingine mbili zikicheza mechi ya mtoano.




Mshindi wa Jackport SportPesa, Yassin Ridhiwani (Kushoto), akipokea mfano wa hundi ya Sh. milioni 437. 6 kutoka kwa Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas (kulia). Katikati ni mke wa mshindi huyo, Rehema Omary. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Mshindi Jackport akabidhiwa kitita*

**Na Mwandishi Wetu**

YASSIN Ally ambaye aliibuka mshindi wa Jackpot ya SportPesa amekabidhiwa zawadi yake ya hundi ya Sh. milioni 437.6 kwenye hafla fupi iliyofanyika katika ofisi za kampuni hiyo jijini Dar es Salaam jana.

Yassin mkazi wa Ubungo jijini amepata zawadi hiyo baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 13.

Akizungumza mara baada ya kuwakabidhi mfano huo wa hundi ya zawadi hiyo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas alimpongeza kwa ushindi huo.

Tarimba alisema kuwa wao SportPesa ni kampuni isiyobahatisha katika katika michezo hiyo na ndiyo maana wamekuwa namba moja hapa nchini huku akitoa shukrani kwa Watanzania kuwafikisha hapo walipo.

"Sh. milioni 437, siyo ndogo kwa Mtanzania wa kawaida, lakini kama SportPesa tunafarijika tukiona maisha ya Watanzania yakibadilika baada ya kushinda na SportPesa hivyo niwatake Watanzania waendelee kubashiri nasi kwani kila wiki SportPpesa itakuwa ikitoa mamilionea.

Alisema SportPesa inatoa zawadi kwa kila mshindi anayeshinda bila kuangalia mazingira anayotokea ili mradi awe na umri kuanzia miaka 18.

"Tunachukua fursa hii kuwashukuru washindi wetu wa wiki hii na kuwaomba watumie vema pesa walizojishindia kwa ajili ya kuendeleza maisha yao, pia ni faida kwa serikali ambayo kwa kupitia ushindi wake kumeinufaisha kwa kukatwa Sh. milioni 87 iliyokatwa kwenye kodi."

"Kuna washindi wengine pia waliojishindia mechi 10, 11 na 12, hivyo SportPesa tunawazawadia hata wale ambao hawakufanikiwa kubashiri mechi zote 13 kwa usahihi"

Naye Yassin alisema alianza kubashiri na SportPesa takribani miezi mitano iliyopita na alipata hamasa zaidi baada ya kuona washindi wa Jackpot wa kitita cha Sh. milioni 825.

"Nilianza kucheza na SportPesa miezi mitano iliyopita baada kuwaona Magabe na Kingslay wakikabidhiwa cheki yao, niliamini na kuanza kucheza. Nashukuru Mungu leo nimeibuka kuwa mshindi."

Naye Mwakilishi wa Michezo ya Kubahatisha Kitengo cha Ilala, Haule Philip alisema: "Ushindi unaopatikana wa SportPesa unakuwa wa uwazi na ndiyo maana Yassin ambaye mshindi leo hii yupo hapa mbele kwenye vyombo vya habari.

"Ushindi huu wa Yassin umeongeza mapato serikali ambaye yeye anakatwa Sh. Mil 87 ambazo zote zinaingia serikalini, kikubwa ni kumtaka mshindi huo aendelee kuzitumia pesa hizo vizuri, alisema Philip.

Elibariki Sengasenga, Mwakilishi wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania, alisema SportPesa ni sehemu ya michezo ya ambayo serikali inaratibu, hivyo tuwapongeza kwa hatua waliyofikia katika michezo hii.

## Mlipili arejea kuibeba Simba

**Na Saada Akida**

BEKI wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba, Yussuf Mlipili amewaondoa hofu mashabiki wa timu hiyo na kueleza kuwa amerejea kambini tayari kutekeleza majukumu yake.

Mlipili amerejeshwa katika kikosini baada ya Kocha mkuu wa timu hiyo, Sven Vadenbroeck kumuondoa ndani ya timu hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Mlipili alisema amerejea ndani ya kikosi cha timu hiyo na kuhakikisha anafanya vizuri endapo atapata nafasi ya kucheza.

Beki huyo alisema mashabiki wake wawe na imani na benchi la ufundi pamoja na wachezaji wao katika kuhakikisha wanapata pointi muhimu kila mechi.

"Mashabiki wawe na imani na timu yao, wote tuna malengo ya kupata matokeo mazuri katika mechi kila mechi ya ligi ili kutetea taji la ubingwa," alisema Mlipili.

Aliongeza kuwa ana imani atafanya majukumu yake katika kiwango cha juu kama ambavyo alivyoonekana katika mechi za msimu uliopita.

## Wushu wapata kocha Mchina

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha mchezo wa Wushu Tanzania kimeingia mkataba wa miaka miwili na kocha Hujin Chao kwa ajili ya kukiandaa kikosi kinachotarajia kushiriki Michezo ya Olimpiki itakayochezwa nchini Japan baadaye mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa chama hicho, Mwarami Shaweji alisema wanaamini kocha huyo ataleta mabadiliko katika kikosi kitakachokwenda kupeperusha bendera ya Tanzania kwenye michezo hiyo.

Shaweji alisema Chao ameletwa maalumu kwa ajili ya kufundisha wachezaji vijana wenye umri kati ya miaka 10,12 na 16.

"Tumefarijika kupata kocha ambaye ana uzoefu wa kutosha, ni matarajio yetu atatutengenezea timu ambayo itakuwa nzuri na endelevu," alisema Shaweji.

Aliongeza ili kufikia malengo yao ya kurudi na medali, chama kilifikiria kuwekeza katika kumleta kocha huyo ambaye ana rekodi nzuri hapa barani Afrika. Aliwataka Watanzania kujiunga na mchezo huo ambao kwa sasa unazidi kukua na vipaji vya wachezaji chipukizi vinaonekana.



# Michezo

Jumatano Februari 12, 2020

Nipashe




Juve yajipanga kumng'oa Guardiola UKURASA 30



Mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere akiwania mpira dhidi ya beki wa Mtibwa Sugar, Kibwana Shomary (kushoto), katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri, Morogoro jana. Simba ilishinda 3-0. **PICHA: ISAAC KIJOTI**

# SVEN ANYAMAZISHA MASHABIKI SIMBA

## ●●● Kombinesheni ya Kagere na Bocco yambeba, huku Dilunga na Tshabalala wakifanya yao kwa...

**Na Isaac Kijoti,** MOROGORO

BAADA ya Ijumaa iliyopita kujeruhiwa hatimaye Simba imeamka kwa hasira na kuisambaratisha Mtibwa Sugar kwa mabao 3-0 katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Jamhuri mjini hapa jana.

**Ikiwa katika Uwanja wa Uhuru Ijumaa, Simba ilianza mzunguko wa pili kwa kipigo cha bao 1-0 dhidi ya JKT Tanzania na mashabiki wa timu hiyo kuanza kulitaja jina la aliyekuwa Kocha Mkuu, Patrick Aussems.**

Hata hivyo, jana Kocha Sven Vandenbroeck aliwanyamazisha kwa kujibu mapigo kufuatia kubadili mfumo kwa kuanzisha washambuliaji wawili mbele, Meddie Kagere na John Bocco tofauti na mmoja kama ilivyozoeleka.

Mfumo huo uliisumbua Mtibwa Sugar na kulazimika kujilinda zaidi hivyo kukaribisha mashambulizi zaidi langoni mwao, ambapo kipindi cha kwanza walipata kona mbili dhidi ya tatu za Simba.

Simba ilikuwa ya kwanza kufika langoni kwa Mtibwa ambapo dakika ya pili tu Hassan Dilunga shuti lake lilionekana cha moto kwa kipa Shabani Kado huku dakika ya nne Mtibwa ilijibu shambulizi hilo na kufanikiwa kupata kona iliyogeuka kuwa tasa kabla ya dakika ya 12, Kagere kushindwa kuitendea haki krosi ya Dilunga kutoka wingi wa kulia.

Francis Kahata alimjaribu Kado katika dakika ya 15 lakini shuti lake lilikuwa mboga kwa Kado.

Kama si kipa wa Simba, Aishi Manula kuwa makini kwa kucheza shuti la Stamili Mbonde baada ya makosa ya Tairone Santos, Mtibwa ingeweza kuwa ya kwanza kuandika bao la kuongoza.

Kadhalika, Kagere dakika ya 40 alishindwa kuitendea haki krosi ya John Bocco baada ya shuti lake kutoka nje.

Faida ya washambuliaji wawili kwa Simba ilianza kuzaa matunda dakika ya 45 baada ya Bocco kuifungia bao la kuongoza akishirikiana vema na Kagere sambamba na Clatous Chama.

Kipindi cha pili Simba iliuanza mchezo kwa kasi na dakika ya 46 Mohamed Hussein 'Tshabalala' aliambaa na mpira wingi wa kushoto na kuachia shuti lililojaa moja kwa moja kushoto mwa nyavu za Mtibwa Sugar.

Simba iliendelea kuliandama lango la Mtibwa na katika dakika ya 58 Dilunga aliachia shuti kali lililomshinda Kado na kujaa nyavuni na hadi mwisho ilitawala mchezo zaidi huku ilipata kona tano na wapinzani wao wakitoka kapa.

Mtibwa ilifanya mabadiliko kwa kuwatoa Omari Hassani, Ismail Mhesa na Franck Kaholi huku ikiwaingiza Juma Luizio, Haruna Chanongo na Boban Ziruntusa wakati Simba iliwatoa Bocco, Kapombe na Chama na kuwaingiza Luis, Shiraff Shiboub na Haruna Shamte.

Matokeo hayo yanaifanya Simba kulipa kisasi cha bao 1-0 walichokipata katika fainali ya Kombe la Mapinduzi Januari 13, mwaka huu kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar. Lakini pia Simba imeendeleza ushindi wao dhidi ya Mtibwa kufuatia mzunguko wa kwanza kushinda 2-1 jijini Dar es Salaam.

Simba inaendelea kung'ang'ania kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 53 huku Mtibwa ikibaki na alama zake 37 baada ya timu zote mbili kushuka dimbani mara 21 msimu huu.

Katika mechi hiyo ya jana, Mtibwa ndiyo ilikuwa ya kwanza kuingia uwanjani majira ya saa 8:48 kabla ya dakika tatu baadaye Simba kuwasili. Kadhalika, Mtibwa ilitangulia kuingia kupasha uwanjani saa 9:16 na dakika moja baadaye Simba ikafuata.

## Ndayiragije atetea ratiba Ligi Kuu

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI wadau mbalimbali wa soka nchini wakilalamikia ratiba mpya ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Etienne Ndayiragije, amesema ratiba hiyo si mbaya ila changamoto iliyopo ni usafiri wa kutoka kituo kimoja kwenda kingine.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ndayiragije alisema endapo timu zitasafiri vema, wachezaji wanaweza kuonyesha viwango vizuri na ligi itaendelea kuwa na ushindani.

Ndayiragije alisema ili kuendana na hali hiyo, makocha wanatakiwa kuwapa wachezaji wao mazoezi maalumu huku pia wakitoa nafasi kwa wote waliowasajili.

"Hata ukiwapa muda mrefu wa kupumzika kati ya mechi moja na nyingine, bado wachezaji hao hawatapumzika, tunazijua tabia zao," alisema Ndayiragije.

## Twiga Stars yaenda Tunisia

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), imeondoka alfajiri ya leo kuelekea Tunisia kwa ajili ya kushiriki mashindano ya Kombe la UNAF ambayo yanashirikisha nchi tano za barani Afrika.

Mbali na Tanzania ambao ni wageni, nchi nyingine zinazotarajiwa kushiriki mashindano hayo ambayo yatakayoanza kufanyika kesho hadi Februari 22 mwaka huu ni pamoja na Morocco, Algeria, Mauritius na wenyeji Tunisia.

Kocha Mkuu wa Twiga Stars, Bakari Shime, alisema kuwa timu yake ilianza kujiandaa na mashindano hayo wiki iliyopita na wanatarajia kwenda kupeperusha vema bendera ya nchi kwenye michuano hiyo.

"Idadi kubwa ya wachezaji wa kikosi hiki walikuwa kambini kwa muda mrefu, isipokuwa wachezaji 11 ambao walikuwa nje ya timu, lakini wametoka katika klabu zinazoendelea na mechi ya ligi," alisema Shime.

Aliongeza kuwa sasa hivi Twiga Stars itatumia michuano hiyo ili kujiandaa kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika (AWC).


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042